# KANGA KAMA SAJILI MAALUM YA KISANII NA MAWASILIANO

**NA**

**WACHARO, JULIA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUKIDHI MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA MOI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**NOVEMBA, 2013**

## UNGAMO

### UNGAMO LA MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijawasilishwa kwa ajili ya shahada yoyote katika chuo kingine chochote. Hairuhusiwi sehemu yoyote ya tasnifu hii kutolewa bila idhini yangu na/au ya Chuo Kikuu cha Moi.

____________________________ ______________

JULIA WACHARO TAREHE

SSC/PGK/03/05

CHUO KIKUU CHA MOI

### UNGAMO LA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa mzamili.

___________________________ __________

PROF. NAOMI L. SHITEMI TAREHE

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MOI

_____________________________ __________

DKT. ISSA MWAMZANDI TAREHE

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MOI

## Tabaruku

Kwa Binti yangu mpendwa Dorian Dzame (Deedee) na marehemu mpenzi wangu Costa Mwangudza kwa kunifanya niitwe mama mtu. Costa, daima nitakumbuka na kuthamini wakati tuliokuwa pamoja.

## Shukrani

Kwanza kabisa namshukuru Maulana kwa upendo wake. Bila yeye nisingeweza kustahimili mawimbi makali niliyokumbana nayo mara kwa mara nilipokuwa nikifanya shahada yangu ya uzamili.

Pili, nawashukuru wazazi wangu Doreen Wanjala na Charles Atira (Bob) kwa kunifikisha nilipofika. Kwa Babangu – "Orio Bob nyasaye akhumete tsinyanga." Kwa mama – "Chawucha mao, Mulungu ukuneke matuku malazi." Pia namshukuru nyanyangu mpendwa Agnetta Marsha – mwanamke mwenye ari, aliyenifunza kuwa, penye mema Mungu huzidisha rehema. Kwake – "Anguo, nadakukumbuka toe."

Walivyosema wahenga ni kweli kuwa 'Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.' Ndugu zangu Victor, Marsha, Angella na Joshua ni thibitisho la msemo huo kwani wanne hawa walikuwepo kila nilipohitaji mtu wa kulia au kucheka naye.

Mwingine aliyechangia pakubwa katika uandishi wa tasnifu hii ni hayati mpenzi wangu Costa Mwangudza. Daima nitatambua mchango wake wa kifedha na ushauri alionipa. Kwa bahati mbaya, Costa aliaga dunia kabla ya kuona matunda ya jasho lake. Hata hivyo, furaha na msiba ndicho kidunia na namshukuru Mungu kwa miaka tisa niliyomjua mtu huyu wa kipekee aliyenipenda na kuniheshimu.

Sijui maisha yangekuaje bila marafiki wakiwemo Catherine Imbuka, Everlyn Karisa, Alice Nzalu, Gloria Shighadi, Winnie Ng'ang'a, Lilian Kemunto, Diana Mwango, Lydia Moraa, Corine Mbati, Fr. Boniface Ifire, Fr. Gabriel Charo, Baraka Kifalu, Dkt. Mulewa, Edna Koe, Agnes Muthoni, Violet Namai, Carol Msisi, Joyce Majanja, Sheila Wamboi, Geofrey Nzuki, Titus Wafula, David Muchunguh, Elijah Mulama, Mauya, Momanyi, Nyagilo na wengineo.

Aidha, siwezi kuwasahau marehemu rafiki zangu Lydia Mocheche (1983 - 2007) na Sinjiri Mukuba (1975 - 2008). Kwa kuwa ya Mungu hayakosolewi, namshukuru kwa kunipa fursa ya kuwajua japo kwa muda mfupi.

Kazi hii haingekuwa na umbo iliyonayo sasa kama haingefinyangwa chini ya uongozi wa wasimamizi wangu Profesa Naomi Luchera Shitemi na Daktari Issa Mwamzandi. Wawili hawa walinihimiza bila kuchoka. Vile vile, nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi hasa Mwalimu Njoroge Ngugi aliyenihimiza kila nilipolemewa na kupoteza mwelekeo. Wengine nisioweza kusahau ni Mwalimu Mannasseh Luganda na marehemu Daktari Hannington Oriedo wa Chuo Kikuu cha Masinde Muliro kwa kunipa ushauri kila tulipokutana.

Vile vile nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Falsafa Chuo Kikuu cha Moi wakiwemo Prof. Kahiga, Daktari Ntabo, Mw. Kanja, Mw. Abwire, Mw. Musi, Daktari Mary Wahome na Mw. Cheseto kwa upendo, usaidizi na ushauri wao.

Hatimaye, nawashukuru wafanyikazi wa jumba la makumbusho la Fort Jesus wakiwemo Bi. Saadu, Bw. Mubarak, Sheikh Nabhany na Bi. Khadija kwa kunipokea kama mmoja wao na kunisaidia kila nilipowahitaji.

## Ikisiri

Istilahi mawasiliano ni tafsiri ya neno la Kiingereza '*Communication'* ambalo lina asili ya Kilatini *'Com-uni-care'* linalomaanisha kujadiliana au kuwa na mazungumzo. Mawasiliano ni mchakato ambao kwao habari hupokezwa baina ya mtu na mtu kupitia kwa mfumo ulio sawa wa alama au matamshi au ishara. Mara nyingi, mawasiliano haya huzua hisia kama furaha, huzuni, mapenzi na matumaini. Nyenzo mojawapo ya mawasiliano miongoni mwa wapwani wa Kenya ni kupitia kwa Kanga.
Kanga ni kitambaa kipana chenye urefu wa sentimita 150 na upana wa sentimita 110 ambacho kwa kawaida huwa na maandishi ambayo hutumiwa kuwasilisha ujumbe fulani. Kanga hununuliwa na kuvaliwa mbili mbili (gora). Utafiti huu unafafanua uamilifu wa Kanga miongoni mwa wapwani wa Kenya kwa kuchunguza vazi hili kama makala maalum ya kusomeka. Utafiti wetu umeongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya simiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure (1857 -1913), Charles Pierce (1839 -1914) na Roland Barthes (1915 - 1980) wanaosisitiza kuwa kila ishara huwakilisha ujumbe fulani. Nadharia ya uamali inayosisitiza kuwa muktadha ni kipengele muhimu katika mawasiliano. Tumeibua data kwa kushirikiana na wanajamii katika shughuli zao za kila siku huku tukiwasaili kuhusu Kanga na matumizi yake. Aidha, tumewatembelea wauzaji na watengenezaji Kanga ili watupatie data kuhusu mikondo inayotumiwa na wanunuzi wa kanga. Isitoshe, tumesoma maandishi ya wasomi tofauti hasa yale yanayohusiana na mada yetu. Mbali na hayo, tumepata ushauri kutoka kwa wataalam waliofanya utafiti kuhusu kanga wakiwemo Sheikh Nabhany (shairi '*Utendi wa Ulimwengu wa* Kanga') Marie Beck (*Ambiguous Communication, kanga/leso*) na Clarrisa Vierke. Mawasiliano yetu yalikuwa ya njia ya simu, intaneti na ana kwa ana. Sampuli iliyotumiwa imeteuliwa bila utaratibu maalum. Sura ya kwanza inatoa utangulizi wa tasnifu hii ilhali sura ya pili inaelezea historia na dhima zingine za kanga. Sura ya tatu inafafanua mawasiliano kupitia kwa kanga huku sura ya nne ikijikita katika kuchunguza uhusiano baina ya muktadha mnamotokea mawasiliano na mawasiliano mahsusi. Sura ya tano inatamatisha utafiti huu kwa kutoa mapendekezo.

## Abstract

Communication is part and parcel of human experience achieved through songs, poetry, writings, signs etc. Etymologically, it is a compound word derived from the Latin *com-uni-care* which literally means "to confer or discourse". In this context it refers to the desire or intention of the communicator to make his/her feelings, thoughts and ideas known to his/her target group. It takes the form of invoking feelings of joy, sadness, love and hope by the speaker to his audience. Among the coastal people of Kenya, one way in which such communication is achieved is by the use of the 'Kanga' as a platform upon which communicative messages are in - scripted. A kanga is a rectangular cloth measuring 150 by 110 cm. It contains sayings which communicate social, cultural, religious, political and even messages that are sentimental in nature. The Kangas are normally bought and worn in pairs – called 'gora'. This research aims at explaining the functions of the Kanga among the coastal people of Kenya by examining this cloth as a special readable text. The research is guided by two theories: The semiotics theory by Ferdinand de Saussure (1857 -1913) Charles Pierce (1839 – 1914) and Roland Barthes (1915 - 1980) which is rooted in the fact that every sign is embedded with a signifier and a signified. It also states that every sign has a meaning. The effectiveness of the Kanga as a means of communication is therefore judged by critically observing all the components of this cloth. The second theory is the pragmatics theory. This is the study of language which focuses attention on the users and the context of language use rather than on reference, truth or grammar. The following methods were used to collect data: participatory observation, interviewing, library research and consultation. Our respondents were chosen through random sampling. Chapter one introduces the thesis while chapter two deals with the history and functions of Kanga. Communication through the Kanga is explained in chapter three. Chapter four analyses the relationship between context and communication by Kanga as chapter five concludes the study by giving recommendations based on the findings.

# YALIYOMO

Ungamo ..... ii
Tabaruku ..... iii
Shukrani ..... iv
Ikisiri ..... vi
Abstract ..... vii
Yaliyomo ..... viii
**SURA YA KWANZA** ..... 1
**MISINGI YA UTAFITI** ..... 1
1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Usuli ..... 1
1.2 Suala la Utafiti ..... 3
1.3 Madhumuni ya Utafiti ..... 4
1.4 Nadharia tete za Utafiti ..... 4
1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 5
1.6 Upeo wa Utafiti ..... 5
1.7 Msingi wa Kinadharia ..... 6
1.7.1 Simiotiki ..... 6
1.7.2 Uamali ..... 10
1.8 Mbinu za Utafiti ..... 13
1.9 Uainishaji na Uchanganuzi wa Data ..... 16
1.10 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ..... 16
1.11 Hitimisho ..... 22
**SURA YA PILI ..... 23**
**HISTORIA NA DHIMA ZA KANGA ..... 23**
2.0 Utangulizi ..... 23
2.1 Kuhusu Watafitiwa ..... 26
2.2 Asili ya Kanga ..... 27
2.3 Chanzo cha Majina kwenye Kanga ..... 29
2.4 Dhima ya Kanga ..... 30
2.4.1 Vazi la Malezi ya Watoto ..... 33
2.4.2 Vazi la Ndoa na Unyumba ..... 34
2.4.3 Vazi la maombolezo ya Kifo ..... 35
2.4.4 Vazi kama mali ..... 36

2.4.5 Kifaa cha Burudani ............ 36
2.4.6 Kitambulisho cha hadhi Kijamii ............ 37
2.4.7 Kanga kama Zawadi ............ 37
2.4.8 Kanga kama vazi maalum la dansi ............ 37
2.5 Usawiri wa Maswala ya Kijamii yanavyojitokeza katika kanga ............ 38
2.6 Usawiri wa Maswala Ibuka kwa kutumia kanga ............ 39
2.6.1 Magonjwa ............ 40
2.6.2 Siasa ............ 41
2.6.3 Haki za Wanawake na Watoto ............ 42
2.6.4 Maswala mengine ............ 43
2.7 Hitimisho ............ 43
**SURA YA TATU** ............ 44
**MAWASILIANO KUPITIA KWA KANGA** ............ 44
3.0 Utangulizi ............ 44
3.1 Dhana ya Mawasiliano ............ 47
3.1.1 Wahusika katika Mawasiliano ............ 52
3.1.2 Diskosi katika Jinsia ya Kike ............ 55
3.2 Kanga kama Kioo cha Jamii ............ 57
3.2.1 Kukomesha Udaku ............ 60
3.2.2 Mapenzi ............ 61
3.2.3 Arusi ............ 63
3.2.4 Mawaidha ............ 65
3.2.5 Imani ............ 66
3.2.6 Kumuenzi Mama ............ 68
3.2.7 Msiba /maombolezi ............ 69
3.2.8 Kauli ............ 70
3.2.9 Usemi wa Jumla ............ 71
3.3 Kanga kama Makala ya Kusomeka ............ 71
3.4 Lugha katika Mawasiliano kupitia kwa Kanga ............ 75
3.4.1 Uwasilishaji Ujumbe kwa Njia ya moja kwa moja ............ 79
3.4.2 Ufumbaji katika Kanga ............ 79
3.5 Hitimisho ............ 82

**SURA YA NNE…………………………………………………………..…84**
**UAMALI WA KIJAMII KATIKA DISKOSI ZA KANGA** ..................................84
4.0 Utangulizi.........................................................................................................84
4.1 Dhana ya Muktadha ..........................................................................................84
4.1.1 Muktadha Kijamii ...........................................................................................85
4.1.2 Muktadha Kisaikolojia.....................................................................................85
4.1.3 Muktadha Kifalsafa..........................................................................................86
4.2 Mitagusano baina ya Washiriki wa Mawasiliano ..................................................88
4.3 Mitagusano baina ya Wauzaji na Wanunuzi wa Kanga.........................................89
4.4 Kanga kama Utanzu wa Fasihi ..........................................................................92
4.5 Hitimisho..........................................................................................................93
**SURA YA TANO……………………………………………………..…….94**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ....................................................................94
5.0 Utangulizi.........................................................................................................94
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ........................................................................................95
5.2 Mapendekezo ....................................................................................................97
5.3 Hitimisho..........................................................................................................98
**MAREJELEO** ....................................................................................................99
**VIAMBATISHO………………………………………………...……………103**
Kiambatisho I: Ratiba ya kazi............................................................................103
Kimabatisho II: Baadhi ya maswali yaliyoongoza usaili........................................104
KiambatishoIII: Nakala za baadhi ya Barua pepe Tulizotuma na Kupokea ..............105
Kiambatisho IV: Majina Yote Yaliyokusanywa........................................................110
Kiambatisho V: Majina Yaliyoainishwa Kimada......................................................116
Kiambatisho VI: Picha.........................................................................................122

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ni kitambulisho cha tasnifu nzima. Inajumuisha usuli, suala la utafiti na umuhimu wa utafiti. Aidha sura hii inashughulikia upeo wa utafiti, misingi ya kinadharia, mbinu za utafiti, uainishaji na uchanganuzi wa dat na yaliyoandikwa kuhusu mada.

## 1.1 Usuli

Mavazi ni kiungo muhimu cha utamaduni kwani ni kitambulisho maalum cha jamii husika. Kwa mfano, ni rahisi kutofautisha Mtugen, Mtaita, Msamburu, Mgiriama na Mmaasai kutegemea mavazi yao[1]. Wanawake Watugen huvaa nguo zenye shanga zinazoitwa *Sir* ilhali wanawake Wataita huvaa vazi liitwalo *Kidemu*. Wasamburu nao wana *Ligesana* na *Ukila* ambazo huvaliwa na wanawake walioolewa. *Nchapkur* na *elgela* huvaliwa na wanawali Wasamburu. Kwa upande mwingine, Wamaasai wana *olkila, osiasai ado sirat, osiasai pusi sirat* na *enkeresure*. Wagiriama nao hutambulika kwa vazi lao maarufu liitwalo *hando*.

Kanga ni vazi linalotumika sana miongoni mwa jamii ya wapwani wa Kenya. Tofauti na matumizi ya vazi hili katika jamii zingine nchini Kenya, kanga katika jamii hii hutumiwa sio tu kusitiri maungo bali pia kusambaza ujumbe mahsusi. Ingawa vazi hili hutumiwa na wake kwa waume, utafiti huu umejikita zaidi kwa wanawake.

Kanga, ni kitambaa kipana chenye urefu wa sentimita 150 na upana wa sentimita 110 ambacho aghalabu hutumika kama nguo ya kujitanda. Sifa kuu ya kanga ni kwamba

[1] Makabila yaliyotajwa yanapatikana nchini Kenya

ina maandishi ambayo hutumiwa kuwasilisha ujumbe fulani. Kuna namna nyingi za kutumia kanga, kwa mfano, kutandika kitandani, kujifunga na kujitanda kama vazi, kubebea mtoto mgongoni na kujipangusia baada ya kuoga. Kuna kanga za rangi tofauti tofauti na umaridadi wa aina mbalimbali. Mbali na kufafanua dhima zingine za kanga, utafiti huu umechunguza na kubainisha dhima ya kanga katika mawasiliano.

Kwa mujibu wa Hassan (2004) kanga nyingi Afrika Mashariki zina sehemu za pindo, mji na ujumbe/jina. Mji huchukua nafasi kubwa ya kanga na mara nyingi pindo huwa jeusi. Ujumbe/ jina huandikwa upande wa chini wa kanga kwa herufi kubwa kwa rangi inayoingiana na ile ya mji.

Utafiti huu umenuia kuchangia katika kukuza dhima za kiisimu-jamii za kanga ambapo vazi hili hutumiwa kama nyenzo ya mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Mbali na hayo, uchunguzi huu umeitambulisha kanga kama makala ya kusomeka na ambayo hutimiza dhima ya aina maalum ya kimawasiliano. Katika muktadha huu, utafiti unachangia katika kubainisha kanga kama sajili maalum ya kusomeka.

Halliday (1978) anafafanua sajili kama lugha inayotumika katika hali tofauti tofauti kutegemea kinachoendelea, wahusika na uamilifu wa lugha. Kanga tofauti hutumiwa kuwasilisha ujumbe kutegemea wahusika, ujumbe na hata wakati. Isitoshe, lugha na mtindo hutofautiana kutegemea hali tofauti.

Maneno mengi yaliyo kwenye kanga, hurejelea kunga za jamii na maswala mengine kama uke wenza, mawaidha, ujirani na maswala ya kidini. Ifuatayo ni mifano ya maneno yapatikanayo katika kanga:

- *Kuolewa ni sheria, kuzaa ni majaliwa*
- *Mme ni kazi, mke tabia*
- *Tutabanana hapa hapa*
- *Heri kumfadhili mbuzi, binadamu ana maudhi*
- *Umesema nimesikia, nikikujibu vumilia*
- *Id-mubarak*

Maneno yapatikanayo kwenye kanga huweza kuwa mafumbo, misemo, methali au maneno ya kawaida. Miongoni mwa istilahi zilizotumiwa katika tasnifu hii kuelezea maneno haya ni mafumbo, maneno, majina, methali, misemo na vitendawili. Katika tasnifu hii, istilahi 'jina/majina ' imetumiwa kuliko istilahi zingine kwa sababu hii ndio istilahi inayotumiwa sana na wapwani wenyewe.

Utafiti umebainisha waziwazi matumizi na dhima ya kanga miongoni mwa jamii za wapwani wa Kenya, hasa kwa kuzingatia maandishi yaliyo kwenye kanga, rangi na umaridadi na mitindo ya kuzitumia.

## 1.2 Suala la Utafiti

Jamii zetu zinakumbwa na matatizo mengi kama magonjwa, uraibu wa madawa ya kulevya, vita, ukabila, unyanyasaji wa wanawake na watoto, ukame na ajali. Ili kupambana na hali hizi ngumu ni muhimu kuwa na nyenzo za mawasiliano zinazoweza kutumiwa kufahamisha wanajamii jinsi ya kukabiliana nazo. Kanga ni mojawapo ya njia hizi kwani kupitia kwazo ujumbe tofauti unaweza kuwasilishwa.

Utafiti huu umelenga kubainisha jinsi vazi hili hutimiza mawasiliano na pia kuchunguza kama vazi hili linaweza kutumiwa kufaidi jumuia kubwa zaidi nchini Kenya katika kukabiliana na hali tofauti zinazoikumba jamii.

Tumeshughulikia vazi la kanga kwa kujikita katika kuchunguza utumiaji wa kanga na uamilifu wa maneno yaliyo kwenye kanga hizi, umaridadi wake na pia rangi zake. Fauka ya hayo, tumechunguza athari za kimtagusano za maneno, umaridadi na rangi kwa watumizi wa kanga husika.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kubainisha kanga kama sajili ya mawasiliano huku tukionyesha kuwa kanga inaweza kutumiwa katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii kuwasilisha maswala nyeti kama uraibu wa madawa ya kulevya, ugonjwa hatari wa Ukimwi na maswala mengine muhimu yanayohusu jamii husika. Madhumuni ya utafiti ni:

(i) Kuchunguza kanga kama makala ya kisanii inayosomeka na kufasirika.

(ii) Kutathmini dhima ya kanga katika mikakati ya ufumbaji.

(iii) Kubainisha dhima za kiisimu jamii za kanga katika miktadha ambamo wanawake wapwani huwa na mazoea ya kuzitumia.

## 1.4 Nadharia tete za Utafiti

Kanga ni vazi lenye maandishi linalotumiwa na wapwani wa Kenya kutimiza haja ya kuwasilisha ujumbe miongoni mwao. Katika misingi hii, nadharia tete za utafiti ni kama ifuatavyo:

(i) Kanga ni makala ya kisanii inayoweza kusomeka na kufasiriwa.

(ii) Maandishi yaliyo kwenye kanga huwa na maana fiche.

(iii) Hakuna jambo katika jamii lisiloweza kuwasilishwa kupitia kwa kanga.

*(iv)* Wapwani hutumia kanga zao kwa kuzingatia jina, rangi na umaridadi

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Kanga ni vazi linalotumiwa na watu wa asili tofauti nchini Kenya. Hata hivyo, uwezo wa vazi hili kutumiwa kama nyenzo ya mawasiliano haujatiliwa maanani katika sehemu zingine za Kenya kama unavyotambuliwa na kutumiwa na wapwani. Kwanza, utafiti huu unatumiwa kama changamoto kwa wanafasihi kutambua umuhimu wa kuanzisha tanzu itakayoshughulikia fasihi za Kiafrika.

Aidha, tasnifu hii inachangia katika kutambulisha umuhimu wa utamaduni mkongwe kama unavyobainika katika matumizi na mawasiliano kupitia kanga. Hatimaye, kazi yetu itachapishwa ili kuwafaidi wataalam watakaofanya tafiti za baadaye kuhusu kanga.

**1.6 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu unachunguza dhima ya maneno yaliyo kwenye kanga na utumiaji wa kanga hizi miongoni mwa wapwani wa Kenya. Pwani nzima imewakilishwa na Mombasa mjini ambapo sehemu zifuatazo zimetumiwa: Old Town, Mwembe Tayari, Bondeni , Mwembe Kuku, Tononoka, Sabasaba, Bombolulu, Kisauni, Majengo na Makaburini. Sehemu hizi zimechaguliwa kukiwa na matarajio kuwa data iloyokusanywa hapa inawakilisha matumizi ya kanga katika Pwani nzima ya Kenya.

Watafitiwa wamekuwa watumiaji wa kanga, watengenezaji na wauzaji. Sampuli iliyotumiwa imeteuliwa bila utaratibu maalum.

Ingawa tulitarajia kuwasaili watu 100, 10 kutoka kila sehemu, kuna sehemu kama Majengo, Kisauni, Sabasaba na Mwembe kuku ambapo tulisaili watu zaidi ya kumi kumi. Hali hii ilitokana na wepesi wa watu wa sehemu hizi kukubali na kutaka kushirikiana nasi. Katika sehemu zilizobaki tulisaili tu wale waliokubali kushirikiana nasi. Hata hivyo, sehemu hizi zilifidiwa na kule tulipopata watafitiwa zaidi ya kumi na idadi yetu ya awali 100, ikatimia.

Hatukufanikiwa kukusanya majina 150 kama tulivyokusudia kwani, kuna majina yaliyojirudiarudia kutokana na watu wengi kuwa na kanga zenye ujumbe sawa. Baadhi ya majina haya yaliyokuwa na watu wengi ni:

*Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa*

*Penye mema Mungu huzidisha rehema*

*Zawadi ni chochote kupokea usichoke*

*Pekepeke mwisho utabaki peke yako* na

*Nani kama mama*

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya simiotiki na nadharia ya uamali.

### 1.7.1 Simiotiki

Miongoni mwa waanzilishi wa nadharia ya simiotiki ni Ferdinand de Saussure(1857 -1913), Charles Peirce (1839 -1914) na Rolland Barthes (1915 -1980). Pierce (1958)

anafafanua simiotiki kama kanuni za ishara ambazo huwakilisha mtu au kitu katika hali fulani.

Kwa mujibu wa *wikipedia the free encyclopedia,* simiotiki ni elimu ya ishara. Ishara hizi zinaweza kuwa katika kundi au moja moja. Elimu hii inahusu vile ujumbe unavyosimbwa na kusimbuliwa.

Siegel katika mtandao wa intaneti (http://www.kristisiegel.com/theory.htm) anafafanua simiotiki kuwa sayansi ya ishara. Anadai kuwa, sayansi hii hujumuisha matambiko, mavazi, vyakula na utamaduni tunaoshiriki.

Utafiti wa kisimiotiki hunuia kuchunguza uhusiano baina ya **X = Y**. **X** ni kitu kilichopo (exists materially) kinaweza kuwa neno, riwaya, kipindi katika runinga ama kitu kilichobuniwa na binadamu. **Y** ni maana inayotokana na kitu hicho. Kuchunguza maana ya **Y** ndio simiotiki. Mchakato wa kuchunguza maana ya **Y** huitwa ufasiri. Mchakato wa kurekodi mawazo, ujuzi au ujumbe unaitwa uwakilishaji katika nadharia ya simiotiki. Danesi (2002).

Kama katika riwaya ambapo tunaisoma na kuikumbuka kama umbo moja X wala sio vijipande vya maneno, ujumbe ulio kwenye kanga pia huchukuliwa kama umbo moja X lenye maana Y. Katika kushughulikia kanga kisimiotiki, maswali haya yatatuongoza:

1. Tanzu ya kanga inahusu nini?
2. Je maana katika kanga hufasiriwa vipi na kwa kuzingatia nini?

Ellis na McClintock (1990) wanadai kuwa, wafuasi wa nadharia ya simiotiki hutilia maanani zaidi jinsi ujumbe unavyofasiriwa kuliko vile mchakato wa uwasilishaji wa ujumbe huu hufanyika. Katika uchunguzi wetu, tumezingatia zaidi jinsi ujumbe ulioko kwenye kanga unafasiriwa. Hapa, kanga inatumiwa kama makala na nyenzo ya mawasiliano yenye ishara zinazobeba ujumbe.

Kiashiriwa (Signified) + Kiashiria (Signifier) = Ishara (Sign)

Ishara ni kitu au alama yoyote ile inayowakilisha kitu kingine. Brown (1995) anasema kuwa, ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Ili watu waelewe kinachowasilishwa na ishara fulani, lazima watu hawa wawe na makubaliano fulani ambayo hutokana na kushiriki elimu, utamaduni, dini na mandhari sawa. Ishara hizi hujumuisha picha, rangi, maumbo mbalimbali na hata herufi zinazounda maneno.

Watu wa asili tofauti huweza kuelewa ishara sawa kwa njia tofauti kutegemea tajriba zao ilhali watu kutoka jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja na kushiriki utamaduni sawa huwa na ukubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake.


Nadharia hii ina misingi yake katika imani kuwa watu katika jamii moja wanaozungumza lugha moja na kuwa na utamaduni sawa huweza kuwasiliana kwa njia fiche. Ingawa hali hii ipo katika maisha ya kila siku, kuna nyakati ambapo watu huwasilisha ujumbe wao wazi wazi bila kufumba. Kwa hivyo ni muhimu kujua kuwa hata kanga huweza kuwasilisha ujumbe wazi (bila kutumia mafumbo).

Kwa mujibu wa wavuti (http://oak.cats.ohiou.edu/~mv537899/sc.htm) nadharia ya simiotiki husisitiza kuwepo kwa ujumbe kila mahali. Kwa hivyo, inatarajiwa kuwa kila ishara itaangaliwa kwa jicho la ndani ili kupata maana ya ujumbe fulani.

Katika kuchunguza athari za nadharia ya simiotiki kwa jamii, Krawsczyn (2006) katika mtandao wa intaneti, anadai kuwa nadharia ya simiotiki inaweza kuleta mabadiliko katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii kwa kuwa itawatia motisha wanajamii kuchunguza mazingira yao kwa jicho pekuzi huku wakizingatia kuwa kila ishara haikosi maana. Isitoshe, simiotiki itawafanya wanajamii kuwa makini zaidi wanapoelewa kuwa ishara ndogo au sahili ina uwezo wa kubeba ujumbe muhimu.

Kama mawasiliano ni mchakato wa kueneza habari kutoka kwa chanzo chake hadi kwa anayeipokea, basi nadharia hii ya simiotiki inahusu kueneza ujumbe uliosimbwa kwa kutumia ishara.

Mwananadharia wa Marekani, Pierce (1839 – 1914) amewasilisha nadharia ya simiotiki kwa kutumia umbo lifuatalo:



Katika umbo hili kuna uhusiano baina ya ishara, kitu / jambo linalowasilishwa na mfasiri anayeipa ishara maana. Mfasiri huweza kuwa aliyesimba ujumbe au atakayesimbua ujumbe huu.

Nadharia hii imetusaidia kufafanua miktadha ya uamilifu wa kanga kimawasiliano kwa kuzingatia upekee wa ishara zilizo kwenye kanga kama kipengele maalum cha mawasiliano. Hapa tumechukua majina na mtindo wa kutumia kanga kuwa ishara za kipekee za kisimiotiki na ambazo zinaweza kutolewa fasiri za kiisimu jamii. Mbali na hayo, nadharia hii imetusaidia kutathmini nadharia tete na kufikia hitimisho yakinifu.

Upungufu wa nadharia hii ni kuwa inachukulia kwamba ishara zote kila mahali na wakati wote zina maana. Inapuuza hali ambapo ishara zingine huwa hazijabeba ujumbe wowote. Alivyosema Griffen (1997: 118) ni kweli kuwa, simiotiki ina hatari ya kuwa juu ya kila kitu kiasi cha kupoteza uhalisia. Ingawa hivyo, nadharia hii bado ina mashiko na binadamu ana jukumu la kuwa makini kujua mazingira, utamaduni na lugha yake.

Nadharia ya simiotiki ni pana na yenye vitengo vingi mno. Kwa sababu ya utafiti huu tumetumia vijisehemu vya nadharia hii huku tukivifungamanisha na nadharia ya uamali.

### 1.7.2 Uamali

Haja ya kushughulikia mada yetu katika misingi ya kiuamali ilitokana na ugunduzi kuwa hatungeweza kufanya uchunguzi wa kina bila kuhusisha ishara za mawasiliano na muktadha mahsusi. Aidha, tuligundua kuwa watu tofauti hufasiri ishara kwa njia tofauti kutegemea tajriba zao.

Kamusi sanifu ya isimu na lugha inafasiri uamali kuwa ni sehemu ya taaluma ya isimu ambayo huchanganua lugha kwa kuihusisha na mtumiaji hasa kwa kuzingatia uchaguzi wa miundo ya maneno anaoufanya na vikwazo na athari za kijamii anazokumbana nazo katika kutumia lugha hiyo.

Kwa mujibu wa Morris (1938) uamali unahusu uhusiano baina ya ishara na wachanganuzi wa ishara hizi. Anazidi kueleza kuwa, uamali hujumuisha matukio ya kisaikolojia, kibayolojia na maswala ya kijamii yanayotokea katika uamilifu wa ishara.

Kaplan (1989) anafafanua uamali kama maelezo ya kwa nini neno linapewa maana fulani badala ya maana nyingine. Ilhali Kempson (1988) anasema uamali hufafanua jinsi sentensi zinavyotumiwa katika usemi kuwasilisha ujumbe kimuktadha.

Kwa mujibu wa Davies (1991) Uamali hujumuisha vipengele hivi:

i) Nia ya mwasilishaji ujumbe

ii) Matumizi ya lugha yanayolandana na nia yake

iii) Mikakati inayotumiwa na msimbuaji ujumbe kujua kusudi la mwasilishaji ujumbe.

Fotion (1995) anaona uamali kuwa uchunguzi wa lugha unaotilia maanani watumiaji lugha na miktadha ambamo lugha hiyo hutumiwa. Uamali haujihusishi na ukweli wala usarufi. Carston (1999) anaeleza kuwa ili kupata maana kiuamali ni sharti maswali kama kwa nini mwasilishaji ujumbe amesema hivi badala ya vile? Ni nini

kilichomsukuma kusema hivyo? Ni nini kinaendelea maishani mwake? Na kadhalika yaulizwe.

Lycan (1995) anasema uamali huchunguza matumizi ya lugha kimuktadha. Uamali huchunguza ni vipi sentensi moja sawa inaweza kuwasilisha ujumbe tofauti katika miktadha mbalimbali.

Bach (2004) anashereheshea kwa kusema kwamba, tunapozungumzia uchanganuzi wa kiuamali huwa tunajihusisha na maswala ya nje ya isimu. Uamali hujumuisha vipengele vyote vinavyohusu usimbaji na usimbuaji ujumbe kama mazingira, wahusika, kinachoendelea wakati huo na sababu zilizomfanya mtunzi wa ujumbe autunge.

Kutokana na fafanuzi tulizopata, uamali ni mtazamo wa kifalsafa unaochunguza matumizi ya lugha kwa kuzingatia muktadha ambamo lugha hiyo inatumiwa. Wasomi wote tuliorejelea wanasisitiza umuhimu wa muktadha katika uchunguzi wowote unaohusu matumizi ya lugha. Tunapochunguza mawasiliano kupitia kwa kanga, swala la matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali linaibuka. Majina yapatikanayo kwenye kanga yanaweza kufafanuliwa kwa njia tofauti kutegemea wahusika, sababu za kuwepo kwa ujumbe huo, mandhari mnamotokea mawasiliano, tamaduni za wahusika na uhusiano wa wahusika hao. Nadharia ya uamali imetoa mwongozo wa kushughulikia mawasiliano kupitia kwa kanga kwa kuzingatia maswala ya nje ya isimu. Ili kuyaelewa mawasiliano haya, imetubidi tusichunguze kanga kama kanga tu bali tuchunguze vazi hili kama nyenzo ya mawasiliano kwa kujikita katika jamii inamotumiwa.

Nadharia ya simiotiki na ile ya uamali zinaingiliana na kuchangiana. Nadharia ya uamali inarejelea uchunguzi wa ishara (lugha) na uhusiano wake na watumiaji ishara hizo. Katika utafiti huu, nadharia ya simiotiki imefungamanishwa na nadharia ya uamali ili kuchunguza jinsi wapwani wanavyomudu mawasiliano kupitia ishara zipatikanazo kwenye kanga.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Katika muda wa miezi mitatu tulifanya utafiti katika pwani ya Kenya. Kwa kuwa nia yetu ilikuwa ni kuona hali halisi ya matumizi ya vazi hili, utafiti huu ulifanywa katika makaazi ya wapwani. Hata hivyo, hatukuweza kufanya utafiti katika pwani nzima. Sehemu za Old Town, Mwembe Tayari, Bondeni, Mwembe Kuku, Tononoka, Sabasaba, Bombolulu, Kisauni, Majengo na Makaburini ndizo zilizotumiwa kuwakilisha sehemu nzima. Tulifanya utafiti kwa kuzingatia maandishi yaliyo kwenye kanga, umaridadi na rangi zake, miktadha ambamo kanga hizi zinavaliwa, jinsi kanga zinavaliwa, sababu za kuvaliwa na uhusiano wake na maisha ya wapwani.

Mbinu zifuatazo zilitumiwa katika kukusanya data.

a) Uchunguzi shirikishi: Tulitazama kwa makini matumizi ya vazi hili huku tukisikiza na kurekodi yale tuliyoambiwa na kuona. Tulifaulu kufanya hivyo kwa kujumuika na watafitiwa katika shughuli zao za kijamii kwa mujibu wa utamaduni, tajriba za kidini, kijamii, kiuchumi na kijiografia. Kwa mfano, tulikaa na wauzaji kanga katika maduka yao hasa katika eneo la Mwembe Tayari na katika barabara ya Biashara mjini Mombasa, kisha tukajumuika na watumiaji wa kanga kama vile kina mama katika makundi yao, tulihudhuria sherehe za matanga na arusi na tukashirikiana na wanawake wapwani katika

mapishi, maongezi na ususi. Hivi, tuliweza kuelewa mazingira na mifumo yao ya kijamii na pia tuliweza kuhusisha sajili ya mawasiliano ya kanga na matukio ya jamii ya wapwani.

Uchunguzi shirikishi ulituwezesha kuwajua watafitiwa wetu kindani zaidi. Tukaelewa maisha yao, miundo na mienendo ya jamii yao.

Weidman (1986) anashauri kuwa, ni muhimu kwa mtafiti kuingiliana na jamii anayotafitia. Ikiwa inaruhusiwa, basi mtafiti aishi katika makaazi yao, avae nguo zao, ale chakula chao na aige tabia zao. Tulipokuwa nyanjani, tulijitahidi kuheshimu na kuzoea tabia za wenyeji wetu. Hali iliyorahisisha kukubalika kwetu katika jamii hiyo. Tulivaa skati ndefu na tukajifunga kanga wakati wa kazi za nyumbani. Aidha tulihakikisha kuwa hatukuvaa suruali ndefu za kisasa wakati wa utafiti. Hata hivyo, hatukuweza kuvaa mabuibui ingawa yalikuwepo na watu walihimizwa kujaribu mavazi yote katika maonyesho ya mavazi ya Waswahili pale Fort Jesus ya mwezi Mei 2007 hadi Disemba 2007.

b) Usaili: Tuliwasaili watafitiwa huku tukirekodi yale tuliyopata kwa kutumia kalamu na karatasi. Miongoni mwa yale tuliyoandika ni misemo tuliyoambiwa na watu na ile tuliyoona kwenye kanga tofauti tofauti. Pia tulirekodi mazungumzo yetu na watafitiwa kuhusu matumizi ya kanga na umuhimu wa misemo inayopatikana kwenye kanga hizi.

Wengi wa watafitiwa walizungumza lahaja za Kiswahili kama vile Kiamu na Kimtang'ata na ingekuwa vigumu kwetu kunakili maongezi haya bila usaidizi

wa mtu aliyeelewa lahaja hizi. Ili kuzuia hali hii tuliandika maongezi yaliyofanywa kwa kutumia lahaja kwa kalamu na karatasi. [2]

Kinasa sauti kilitumiwa kurekodi maongezi na watafitiwa. Data iliyokusanywa kwa mbinu hii ilinakiliwa na kufasiriwa katika kuelezea mawasiliano kupitia kwa kanga. Hata hivyo, si kila mtu alikubali kurekodiwa. Katika hali kama hizi tulitumia kalamu na karatasi kuandika.

Aidha, tulitumia kamera ya kitarakimu na ile ya kawaida kupiga picha ambazo tumeziweka katika kiambatisho. Picha zingine hazikutoka kama tulivyotarajia lakini tumezitumia hivyo hivyo kwa kuwa hatukuwa na hifadhi nyingine ya picha.

c) Utafiti maktabani: Tulizuru maktaba mbalimbali zikiwemo za vyuo vikuu vya kitaifa vya Kenya vikiwemo Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo Kikuu cha Moi. Pia maktaba ya Jumba la Ukumbusho la Fort Jesus na maktaba za watu binafsi kama Sheikh Nabahany na Sheikh Mubarak ilinufaisha utafiti huu. Mbali na hayo, tulipitia maandishi mengine yenye uhusiano na mada hii kwenye mtandao.

d) Mashauriano na wataalam: Tuliwasiliana na wataalam wa uwanja huu kama Sheikh Nabahany, Clarissa na Marie Beck tangu tulipoanza utafiti hadi tulipokuwa katika awamu ya kuandika tasnifu. Aidha, tulinufaika kutoka kwa mawaidha ya wasimamizi wetu waliotupa mwongozo na kutuhimiza jinsi ya

[2] Wasaidizi wetu Julie Mkiwa na Fatma Mohamed (wazaliwa wa Mombasa) walitupa tafsiri pale tulipokosa kuelewa lahaja zilizotumiwa.

kukabiliana na hali mbalimbali tulizokumbana nazo katika utafiti na uandishi. Mawasiliano yetu yalikuwa aidha kwa njia ya simu, barua pepe au ya ana kwa ana (Tazama kiambatisho).

## 1.9 Uainishaji na Uchanganuzi wa Data

Baada ya kukusanya data, tulitengeneza kielelezo cha data tuliyokusanya kisha tukaainisha makundi kwa mujibu wa mada mbalimbali za ujumbe uliomo katika maandishi ya kanga kidhamira.

Tumechanganua kimaelezo makundi haya ya mada za kimawasiliano huku tukizingatia kuwa kila ishara ina maana fulani na ishara hizi hufasiriwa kwa njia tofauti kutegemea muktadha mnamotokea mawasiliano.

## 1.10 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Tulisoma tahakiki kadhaa zinazoshughulikia mavazi kama kitambulisho cha utamaduni wa wahusika. Kati ya hizi zipo chache zinazozungumzia kanga kama nyenzo ya mawasiliano. Nyingine zinaongea kuhusu upekee wa mawasiliano baina ya wanawake. Tahakiki hizi zimedhihirisha kuwa kanga ni vazi la kipekee kwani mbali na kusitiri uchi, vazi hili husambaza ujumbe.

Kwa mujibu wa Akong'a (1980) Waswahili wa pwani ya Kenya wametangamana kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii. Wameingiliana kwa kuishi katika mazingira sawa yenye utamaduni wa kipekee unaotilia maanani maadili ya kijamii. Ili watu waelewe ishara fulani lazima washiriki lugha, utamaduni na mandhari sawa. Hali hii inadhihirishwa katika matumizi ya kanga katika kuwasilisha ujumbe miongoni mwa wapwani.

Wanaanthropolojia wakiwemo Low (1979), Lurie (1981) na Alford (1996) wanaamini kuwa kujitambulisha na kujitofautisha katika jamii ni sababu kuu ya kuwepo kwa mavazi. Wanadai kuwa, sababu hii ni muhimu hata kuliko kuficha uchi. Kwa hivyo, mavazi ni kitambulisho cha utamaduni. Utafiti huu unafaidi kutoka kwa maoni ya wanaanthropolojia hawa, kwa sababu tunapochunguza dhima ya kanga na maneno yake tunajikita katika kuchunguza uhusiano uliopo kati ya utamaduni wa wapwani na utumiaji wa kanga miongoni mwao.

Luzbetak (1970) anadai kuwa utamaduni ni hali ya maisha ya watu fulani. Naye Eliot (1988) anasema kuwa dini, mila na desturi ya watu vinaenda sambamba, na haifai vigawanywe. Eliot (ibid) anazidi kudai kuwa, binadamu huzaliwa bila utamaduni. Kwa maoni yake, utamaduni hupokezwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Wasomi hawa wanatupa kielelezo kinachotilia shada msimamo wetu ya kwamba, utamaduni wa utumiaji wa kanga miongoni mwa wapwani ni tabia inayopokezwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine.

Mara nyingi, utamaduni umepewa sifa za kitu kinachoweza kununuliwa. Okot P'Bitek (1986) anapinga imani hii. Mshairi huyu analaumu serikali za Kiafrika kwa kurithi tabia za wakoloni kiasi cha kuamini kuwa utamaduni ni bidhaa au kitu kinachoweza kuhifadhiwa kwenye makavazi ya kitaifa. P'Bitek anaonya kuwa kufanya hivi ni kama kutenga utamaduni na jamii, jambo ambalo haliwezekani kamwe. Kwa maoni ya P'Bitek, utamaduni ni falsafa ya jamii fulani. Anaeleza kuwa, watu huishi katika mipangilio ya asasi za kifamilia, kiukoo na kiutawala. Watu hawa huwa na dini zao, mifumo yao ya elimu, imani zao na mbinu mahsusi za mawasiliano. Tunakubaliana naye katika muktadha huu. Katika kufanya utafiti, tulishughulikia kanga kama

kipengele cha utamaduni kinachofungamana na vipengele vingine katika jamii ya wapwani wa Kenya. Hata hivyo, hatukubaliani na P'Bitek kuwa utamaduni haufai kuuzwa. Siku hizi tunashuhudia mikakati ya kuimarisha sekta ya utalii na miongoni mwa mbinu zilizotumiwa kuwavutia watalii ni matangazo ya kibiashara yaliyoangazia utamaduni wa Wakenya.

Kulingana na Mazrui (1982), dhima ya utamaduni ni kumfanya mtu kuona mambo kihalisia; kutoa viwango vya kutathmini mazuri na mabaya; kumpa mtu ari ya kufanya au kutofanya mambo fulani na kugawanya jamii kulingana na hulka, dini au imani kwa jumla. Pia, utamaduni humpa mtu njia ya kujitambulisha katika jamii. Matumizi ya kanga hasa zile zenye majina, huwapa watumiaji kitambulisho katika jamii. Isitoshe, kanga hizi ni kama kipimo cha kutathmini na kueleza maadili ya jamii hii ya wapwani. Mwanamke anapojisitiri kwa kanga, huonekana kama mwanamke anayestahili kuheshimiwa.

Utamaduni wa Waswahili kama ulivyo Mombasa, Pemba, Kilwa, Pate, Lamu na Zanzibar, unafungamana na utamaduni wa Waislamu wabantu wa kimwambao. Dini ya uislamu haikushurutisha utamaduni wake, bali ilivutia ukuaji wa utamaduni wa Kiafrika kutokana na uzuri wake. Katika utafiti huu, utamaduni wa Kiislamu umerejelewa mara nyingi. Hii inatokana na athari za Uislamu kwa wakaazi wa pwani ya Kenya. Tabia, mienendo na hata utamaduni wa wapwani una uhusiano wa moja kwa moja na Uislamu.

Utamaduni ni mfumo wa kanuni zinazoongoza tabia za wanajamii kuhusu jinsi ya kuwasiliana, kushughulikia mazingira yao, na jinsi wanavyohusiana Levine (1973).

Poyatos (1983) naye anafafanua utamaduni kama tabia za kundi la watu wanaoishi katika eneo moja la kijografia. Tunapozungumzia utamaduni wa wapwani wa Kenya, tunajikita katika maelezo haya ya Levine na Poyatos.

Abdulaziz (1979) anasema kuwa miongoni mwa mavazi maalum ya wanawake wa Kiswahili yalikuwemo vipande vya nguo vya mraba vyenye rangi tofauti tofauti vilivyoitwa leso. Wanawake hawa walijifunga leso moja kiunoni na nyingine ikatandwa kwenye bega ikafunika kichwa isipokuwa sehemu ya macho tu. Maandishi haya ya Abdulaziz, yametufahamisha ujadi wa kanga na matumizi yake.

Chukwu (2002) anadai kuwa, ni lazima kuwe na mawasiliano, kwa sababu watu hawana budi kutangamana katika jamii. Madai haya ya Chukwu, yametuongoza katika kuchunguza dhima ya kimawasiliano ya maneno yaliyo kwenye kanga na jinsi mawasiliano haya yanavyofanyika.

Middleton (1992) anachangia kwa kusema kuwa, mavazi na urembaji ni miongoni mwa maswala muhimu katika jamii ya Waswahili. Anadai kuwa, mavazi hutumiwa kuonyesha hadhi ya mtu katika jamii, umri wake, kazi anayofanya na jinsia yake. Aidha, mavazi na urembaji huonyesha kiwango cha uadilifu cha wanajamii. Mara nyingi, mavazi yanapotajwa, kinachofikiriwa ni kuficha uchi. Middleton ameonyesha kuwa, dhima za mavazi ni nyingi mno na dhima muhimu ya mavazi ni kujitambulisha na kundi au hali fulani. Vivyo hivyo, kanga ni vazi lenye jukumu la kumtambulisha mtumiaji na jamii husika. Aidha, maneno yaliyo kwenye kanga humtambulisha mhusika na hali fulani; labda furaha, huzuni, mapenzi au maombi.

Mbali na kuficha uchi, kanga ina kazi ya kusimba na kusimbua ujumbe. Hanby na Bygott (1984), wanafananisha vitambaa hivi maalum na kadi zenye ujumbe wa heri njema zinazotumika sana katika nchi za kimagharibi. Hata hivyo, ujumbe katika kanga unaweza kutumiwa kwa muda mrefu ikilinganishwa na ujumbe wa kadi ambao mara nyingi huwasilishwa wakati mahsusi. Kwa mfano, ikiwa mtu ni mgonjwa, basi atatumiwa kadi ya kumtaka apone haraka. Kama ni kadi ya shukrani, basi ujumbe utakuwa wa shukrani. Aidha, kadi hutumiwa mtu binafsi tofauti na kanga ambayo ingawa huweza kulenga mtu/watu mahsusi katika miktadha fulani, kwa ujumla ni ya kijumuiya.

Hanby na Bygot (1984) wanazidi kudai kuwa, jamii zinazotumia kanga pia hutumia nguo hii katika kampeni za kisiasa na kampeni za afya na zile za miradi ya maendeleo kama watu wa nchi za kimagharibi wanavyotumia fulana (T-shirts). Wasomi hawa wanahimiza wanajamii wajaribu kutumia nguo hii katika kuelezea maswala nyeti na wangojee matokeo. Hanby na Bygot (ibid) wamemulika baadhi ya vipengele vya elementi ya uamilifu wa kanga ambavyo vinalengwa na watafiti. Aidha, wasomi hawa wamewajengea watafiti msingi imara wa kufanya utafiti.

Ingawa utafiti ulilenga wapwani wa Kenya kwa jumla, watafitiwa waliozingatiwa zaidi ni wanawake. Barbara na Pugh (1987) wanatupa mwongozo wa kushughulikia wanawake kama kundi la kipekee. Wanadai kuwa, wanawake hutoa maoni yao kama kundi. Wanazidi kusema kuwa, maisha ya wanawake kutoka maeneo tofauti tofauti yana uhusiano mkubwa. Mojawapo ya ule uhusiano ni vile wanawake hawa wanavyovaa. Uhusiano mwingine kulingana na Barbara na Pugh ni mawasiliano.

Wanasema kuwa, wanawake ni wepesi wa kusema na kujieleza ikilinganishwa na wanaume.

Maoni ya Barbara na Pugh yametusaidia katika kuchanganua data kwa kuhusisha maoni ya wanawake wachache kuhusu dhima ya kanga na maneno yaliyo kwenye kanga na kundi lote la wanawake wapwani.

Fairclough (1992) anadai kuwa, matini ni chochote kinachoandikwa ama kusemwa na hujumuisha ishara na maneno. Halliday (1978) naye anasema kuwa matini hujenga kitambulisho na kuwakilisha hali halisi ilivyo katika jamii. Madai haya ya Fairclough na Halliday yamechochea uamuzi wetu wa kushughulikia kanga kama matini kwani mbali na kujumuisha ishara ambazo ni majina ya kanga, huwa zinawasilisha maswala ya kijamii.

Beck (2005) anaeleza kuwa mawasiliano kupitia kwa kanga huchukua mikondo miwili:

1. Mwanamke huvaa kanga ili watu wengine waione na wapate ujumbe fulani
2. Kanga hutolewa kama zawadi ya arusi, kuomboleza, Idd ama zawadi ya kumuaga mtu anayesafiri.

Tunapozungumzia mawasiliano katika tasnifu hii, tutajikita katika ufafanuzi huu wa Beck. Hata hivyo hatukubaliani naye kuhusu maswala mengine. Kwa mfano, anadai kuwa wanawake waislamu hawakubali kuwa wanashiriki katika mawasiliano kupitia kwa kanga. Tulipokuwa nyanjani, wote tuliozungumza nao walikubali kuwa mawasiliano kupitia kwa kanga ni jambo la kawaida na hawakulionea haya. Labda

tofauti hii inatokana na athari za kiwakati kwani utafiti wa Beck ni wa kitambo kuliko wetu.

Wasomi wote tuliorejelea wametupa mwongozo wa kuchambua data na kuufanya utafiti wetu kwa jicho pekuzi zaidi. Pia tumefaidika kwa kuona yaliyoshughulikiwa na watafiti wa awali ili nasi tusiyarudie.

## 1.11 Hitimisho

Tumetoa habari za kimsingi kuhusu mada pana ya utafiti – kanga. Tumeelezea madhumuni yetu ya kuzamia utafiti huu kisha tukabainisha wazi umuhimu wa utafiti. Aidha tumefafanua nadharia tete zilizoongoza utafiti, tukaonyesha upeo tulimojikita na tukawasilisha misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti. Hatimaye tumefafanua mbinu za utafiti tulizotumia na kueleza yaliyoandikwa kuhusu mada hii.

# SURA YA PILI

# HISTORIA NA DHIMA ZA KANGA

## 2.0 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kuelezea asili ya kanga na jinsi matumizi yake yalivyoendelea kuimarishwa miongoni mwa Wapwani wa Kenya. Aidha, sura hii itarejelea dhima nyinginezo za kanga. Hata hivyo, kipengele cha mawasiliano ambacho ni dhima kuu ya kanga kitajadiliwa kwa kina katika sura ya tatu.

Kwa muda wa miezi mitatu (01/09/2007 – 30/11/2007) tulipiga kambi katika Pwani ya Kenya ili kuchunguza matumizi ya kanga kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Katika muda huu, tulishirikiana na wakaazi wa Pwani ya Kenya hasa wanawake ambao ndio hutumia kanga kwa jinsi mbalimbali pamoja na wafanyibiashara wa kanga. Tulitangamana nao katika shughuli zao za kila siku kama upishi, harusi, matanga, biashara na mazungumzo.

Licha ya kutangamana na wanawake na wafanyibiashara, tulishiriki pia katika maonyesho ya mavazi ya Waswahili katika jumba la Fort Jesus. Maonyesho haya yalianza mwezi Mei 2007 na yalitarajiwa kuendelea hadi mwezi wa Disemba 2007. Mada kuu ya maonyesho hayo ilikuwa '***Usiwache Mbachao'.*** Miongoni mwa mada ndogo zilizoshughulikiwa ni "The Swahili Attire" yaani vazi la Waswahili, ambapo Kanga ilikua vazi mojawapo lililopewa kipaumbele. Maandishi kuhusu historia ya mavazi ya Waswahili yalituwezesha kuelewa jinsi kanga ilivyoanza kutumiwa na maendeleo yake hadi sasa. Mbali na kanga, aina zingine za mavazi ya Waswahili pia zilionyeshwa. Miongoni mwa mavazi haya palikuwepo kaniki, buibui, hijab, ninja,

kanzu, kofia, debwani, joho na kikoi. Mavazi haya yalitandazwa kote na maelezo kuyahusu yakawekwa kwenye fremu karibu nayo.

Katika chumba cha maonyesho, kila aina ya mavazi ilitengewa sehemu yake ambapo mavazi haya yalitandazwa na mengine yakavishwa sanamu za kiuelelezo. Maandishi kuhusu mavazi haya yaliwekwa kwenye fremu karibu nayo. Katika sehemu ya ***"The World of the Khanga" (Ulimwengu wa Khanga)*** palikuwa na:

- Kanga 190 zilizofungwa kwa mianzi
- Warembo (models) waliojitanda kanga
- Kanga 29 zilizotandazwa kwenye vitambaa ukutani
- Kanga mbili kwenye fremu
- Video ya dakika kumi na tano kuhusu kanga
- Zaidi ya kanga 400 pembeni mwa chumba cha maonyesho (Tazama kiambatisho vii)

Maonyesho haya yalichangia msingi na upeo wa utafiti wetu kwani kwayo, tulipata picha pana na ya kina kuhusu matumizi ya kanga miongoni mwa Wapwani na uhusiano wa vazi hili na utamaduni wa Waswahili. Vilevile tulipata maandishi mbalimbali ya kufaa kuhusu mada hii yaliyowekwa kwenye fremu. Maandishi haya ni ya muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa yalitayarishwa na wataalamu wenye asili ya Kiswahili na wanaouelewa utamaduni wa Waswahili hasa kuhusu kanga. Miongoni mwa wataalamu hawa ni wafanyikazi wa Makavazi ya Kitaifa ya Kenya – Mombasa; Sheikh Mubarak Abdulqadir, Sheik Nabhany na Bi Rukia.

Chambilecho waandalizi wa maonyesho hayo, nia yao kuu ilikuwa kuonyesha ukwasi na urembo wa utamaduni wa Waswahili huku wakionyesha athari za maingiliano

baina ya utamaduni wa Waswahili na utamaduni wa wageni waliofika nchini Kenya. Watayarishi waliwahimiza washiriki wajisikie huru kuyajaribu mavazi hayo ili wawe na kumbukumbu za kipekee kuhusu maonyesho hayo.

Kwa mujibu wa mawasiliano baina yangu na Vierke, maonyesho kama hayo yalifanyika pia nchini Ujerumani katika kituo cha sanaa ya Kiafrika Iwalewa –Haus, Chuo kikuu cha Bayreuth chini ya usimamizi wa msomi Clarissa Vierke[3] na wenzake. Msomi huyu alikiri kuwa washiriki wa maonyesho hayo walivutiwa sana na umaridadi wa kanga. Aidha, washiriki walipata changamoto kutokana na uwezo wa vazi hili kusambaza ujumbe na mawasiliano, hali ambayo si ya kawaida katika jamii yao. Mchango huu wa Clarissa unadhihirisha wazi kuwa vazi hili sasa limevuka mipaka ya kijiografia na kueneza uamilifu wake. Ifuatayo ni sehemu ya barua pepe aliyonitumia kuhusu maonyesho haya:

*...Kwa kweli tulikuwa na maonyesho juu ya leso hapa Bayreuth katika kituo cha sanaa ya Kiafrika kinachoitwa Iwalewa-Haus. Watu walikuwa waliyapenda maonyesho hayo kwa sababu tofautitofauti: Kwa kwanza, kwa sababu ya "designs", mapambo ya leso, rangi zao na mitindo yao zilizo za kuvutia. Tena, leso, haswa leso zilizotoka kwa ukumbusho wa sherehe fulani, (anniversary fulani), ni kama shahada za kihistoria ama kioo cha matokeo katika jamii na historia yake. Tena, Watu walipenda majina ya leso: fikra ya kuwasiliana kwa njia hiyo ni kitu kigeni kwetu. Katika utamaduni wetu(na katika utamaduni wenu huko Kenya pia), siku hizi, watu wengi wanavaa Tshirts, Tshirts za football, Tshirts za chama fulani n.k. kwa ajili ya kijitumbulisha – ni swala la "identity" lililo muhimu sana.*

---

[3] Clarissa ni msomi wa Kiswahili na aliandika barua pepe hii kwa lugha ya Kiswahili. Ingawa alikuwa na makosa ya kisarufi hapa na pale, ung'amuzi wake wa lugha hii ni wa kustajabisha. Hali hii inatupa moyo kama wasomi wa Kiswahili kwani inaonyesha wazi kuwa lugha hii imevuka mipaka ya kijiografia na sasa inasomwa hata ulaya.

*Kwa hivyo, kwa kipengele fulani – unaweza kulinganisha leso na Tshirts. Lakini, vilevile ziko tofauti: Leso zinaingia na zinatumika katika mawasiliano ya kila siku; unaweza kutumia leso ikiwa una ujumbe fulani kwa mtu fulani. Kwa hivyo, a leso is often more _asha_ic (for a specific aim of communication) than a Tshirt. Halafu, leso zinatumia mithali zaidi. Kwa kusema la kweli, sina mengi ya kusema kuhusu mada hiyo mimi sikua na mchango katika maonyesho hayo. Yalikuwa maonyesho ya mtu kutoka mji mwingine anayependa leso na anayekusanya leso. Tena hakuna materials nyingine kuhusu maonyesho hayo: hakuna "catalogue"...*

Hoja kuu tunazopata katika barua pepe hii ni:

1. Kanga imevuka mipaka ya kijiografia
2. Hata wageni nje ya Afrika wanatambua uzuri wa kanga (umaridadi, rangi na majina tofauti tofauti ya kanga)
3. Kanga huhifadhi kumbukumbu za matukio katika jamii.
4. Kanga huwasilisha maswala yanayoikumba jamii (ni kioo cha jamii)
5. Kanga inaweza kufananishwa na fulana za mikono
6. Kanga huwasilisha ujumbe mahsusi na hutumika katika mawasiliano ya kila siku
7. Kanga hutumia methali

## 2.1 Kuhusu Watafitiwa

Ingawa tulinuia kulitafitia kundi la Waswahili pekee, ilitubidi tubadili nia tulipoingia nyanjani kwani sio wote tuliokumbana nao katika utafiti walikuwa Waswahili. Mathalan si wauzaji wala wanunuzi wote wa kanga walikua Waswahili. Pia ilidhihirika wazi kuwa kanga si vazi la Waswahili tu bali ni vazi la wapwani kwa jumla. Isitoshe, kanga pia hutumika kwingineko japo utafiti wetu uliwahusu wapwani tu.

Hata hivyo, tuligundua kuwa Waswahili hujumuisha sehemu kubwa zaidi ya jamii ya Wapwani na tabia zao zimeathiri pakubwa tabia na mienendo ya wakaazi wengine wa Pwani ya Kenya hasa katika matumizi ya kanga. Miongoni mwa athari zinazoonekana wazi ni utamaduni unaoonyesha upekee hususan katika aina za nyumba, mavazi, chakula, ushairi changamano pamoja na nakshi katika vitu mbalimbali. Vile vile wanatambulika kama jamii iliyojengeka kwa misingi ya nasaba ya mama na usambamba wa kiisimu katika lahaja zao. Pwani nzima iliwakilishwa na sehemu zifuatazo katika utafiti: Old Town, Mwembe Tayari, Majengo, Bondeni, Mwembe Kuku, Tononoka, Sabasaba, Bombolulu, Kisauni na Makaburini.

## 2.2 Asili ya Kanga

Kabla ya kuja kwa buibui, wanawake Waswahili walitumia kaniki, kanga na shiraa ili kujisitiri. Kaniki ni vazi lililoshonwa kwa pamba lililovaliwa na wanawake wanawali. Kipande kimoja kilifungwa kiunoni na ncha zake mbili zikaunganishwa kisha kupitishwa juu ya bega moja, kama wanawake wa Kiorma hivi leo.

Vazi lingine lililotumiwa kwa kujisitiri na wanawake Waswahili ni shiraa ambalo ni vazi lililoshonwa kwa kanga lililotumiwa kuwasitiri wanawake pindi walipokuwa wakitoka nje ya nyumba zao. Kulikuwa na aina mbili za shiraa: Ndogo iliyotumiwa na mwanamke mmoja na kubwa yenye pembe nne iliyotumiwa na kundi la wanawake kutembelea kwa pamoja nje ya nyumba. Ile kubwa ilikuwa kama hema na ilibebwa na wafanyikazi mbele na nyuma ili kuwasitiri wanawake kutokana na macho ya matamanio ya wanaume njiani. Katika karne ya 19, shiraa ambayo haikuwa changamano katika ushonaji wake ilizua buibui.

Katika utenzi wa Mwana Kupona, ubeti wa 46 shiraa inarejelewa. Utendi huu ni thibitisho kuwa, stara miongoni mwa Waswahili ni muhimu na ni jambo lililokuwepo tangu jadi.

Wala sinene ndiani  sifunue shiraani
Mato angalia tini  na uso utie haya

Asili ya kanga ni swala tata lisiloweza kushughulikiwa kikamilifu katika tasnifu hii. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa katika miaka ya 1800, mtindo mpya uliibuka Mombasa na Zanzíbar. Wanawake Waswahili walikuwa wakinunua vitambaa vikubwa vilivyopindwa nchani vilivyoitwa *'leso'* neno la Kireno kumaanisha kitambaa cha mkono. Wanawake hawa walianza kuunganisha vitambaa hivi kwa kuvishona ili kutengeneza vitambaa vipana zaidi walivyojitanda kwenye mabega na kujifunga viunoni.

Jina kanga lilizuka kutokana na kufananishwa kwa vazi hili na ndege mkubwa mweusi mwenye madoadoa meupe. Hii ni kwa sababu kanga za mwanzoni zilikuwa nyeusi au nyekundu zenye madoadoa meupe. Hanby na Bygot (1984).

Wafanyibiashara katika barabara ya 'Mwembe Kuku' mjini Mombasa Abdukader Kaderdina (Duka la Kaderdina Hajee Essak Ltd – Mali ya Abdulla)  na Mohamed Akram Abdulla Kaderdina (Duka la Tayari Lesso Ltd – Mali ya Mtoto), wanathibitisha haya wanaposema kuwa biashara ya kanga imekuwa katika familia yao tangu miaka ya 1800. Maongezi yetu nao yalituthibitishia kuwa, kanga imevuka mipaka na kuwa vazi la Wapwani wala sio vazi la Waswahili tu kama ilivyokuwa kitambo. Bwana Mohamed Akram alitujulisha kuwa ingawa wao si Waswahili,

desturi ya kutumia kanga imekuwa miongoni mwa jamii yao kwa muda mrefu. Tulipomdadisi zaidi, alitueleza kuwa, tamaduni za watu wanaoishi pwani zimeingiliana na kuathiriana kwa muda mrefu.

## 2.3 Chanzo cha Majina kwenye Kanga

Hapo awali, kanga hazikuwa na maneno hadi mfanyibiashara mashuhuri Bwana Abdulla alipoanzisha mtindo wa kuandika misemo kwenye kanga zake zilizokuwa na ishara “K.H.E mali ya Abdulla” mapema karne ya ishirini. Misemo hii ilikuwa katika hati ya Kiarabu hadi 1960 ilipoanza kuandikwa kwa Kiswahili na wakati mwingine, hasa hivi majuzi hata Kiingereza. Kuongezwa kwa misemo hii kwenye kanga kulilifanya vazi hili lipande ngazi na kuwa chombo cha kuwasilisha ujumbe. Mara nyingi ujumbe huu ulizua furaha na wakati mwingine ukachochea wivu. Misemo hii aghalabu ilitegemea wakati na majira na ilibadilika kadri wakati ulivyobadilika. Madai haya yalitokana na mahojiano yetu ya tarehe 12.9.2007 na wajukuu wa mtangulizi wa biashara ya kanga katika Pwani ya Kenya ambao bado wanaendeleza biashara hii.

Tofauti na leo ambapo misemo mingi inatokana na maswala ibuka, zamani maandishi yalichotwa kutoka kwa fasihi simulizi ya Waswahili hasa majigambo, unyago, nyimbo na ushairi. Maandishi haya yalikusudiwa kuelimisha, kuburudisha, kuonya, kupongeza na kufumba.

Kanga za zamani zilikuwa na maneno yaliyofuata mtindo wa kishairi uliofanya maneno haya yawe na mdundo na mahadhi maalum. Mfano wa maneno haya ni:

- Ewe Mola tunusu**ru** midomo ya watu isitudhu**ru**
- Kuchunguza ya jira**ni** ni kama kujilaa**ni**

- Sicha**gui** siba**gui** **a**takayenizika sim***jui***
- Si mzi**zi** si hiri**zi** bali ni moyo kupenda
- Twakuomba Mola we**tu** tuishi kama wenze**tu**
- Tabia zikilinga**na** daima tapenda**na**
- Tuishi kwa **amani** watuonao wat**amani**

Hanby na Bygot (1984) wanaorodhesha dhima mia moja na moja za kanga. Mbali na matumizi yaliyowasilishwa na Hanby na Bygot, kazi nyingine muhimu ya kanga ni kuwasilisha ujumbe. Ama kwa kweli, kwa mpwani la muhimu katika kanga ni maneno. Rangi na umaridadi si muhimu kama maneno yaliyoko kwenye kanga. Haya ni kwa mujibu wa Nabhany katika shairi ‘Utendi wa Ulimwengu wa Kanga’ ubeti wa nane.

## 2.4 Dhima ya Kanga

Sheikh Nabhany anachangia mjadala wa kufafanua dhima ya kanga kwa kutunga shairi lifuatalo. Shairi hili linachangia msingi wa kushughulikia mada yetu hasa tunapozingatia kuwa Sheikh Nabahany ni Mswahili mwenye ukwasi mkubwa katika maswala ya utamaduni wa Waswahili, historia yao na lugha ya Kiswahili kwa jumla.

Tutalirejelea shairi hili mara kwa mara katika muktadha wa kujenga tasnifu yetu, hasa katika kueleza dhima ya kanga na uhusiano baina ya vazi hili na maisha ya kila siku ya Mswahili.

## UTENDI WA ULIMWENGU WA KANGA[4]

1. Kanga kwa Waswahili * Kwao ni kitu jamali
   Tangu kale na awali * Maisha wazitumiya

2. Tangu mwana akizawa * Akisha kupokelewa
   Muda wa kuadhiniwa * Kwa kanga humtatiya

3. Na wake mama mzazi * Pamoja na mpokezi
   Hupambwa kwa hilo vazi * Na watu kusherekeya

4. Kibalighi mwana mwali * Ni ada ya Waswahili
   Atavishwa kanga mbili * Apate kuisitiriya

5. Afikapo kuolewa * Na kanga nyingi hupewa
   Kwa wingi hutunukiwa * Na watu kumshashiya

6. Mtu kifa hutumiwa * Kanga ndizo huoshewa
   Na maji kutakasiwa * Na kisha humtatiya

7. Kanga hupekwa zawadi * Kwa marafiki wa jadi
   Hutolewa kwa juhudi * Kwa furaha na kwa niya

[4] Shairi hili lilipatikana katika maktaba ya binafsi ya Sheikh Nabhany, Mombasa mji wa kale. Anahudumu katika Swahili Cultural Centre (kituo cha Utamaduni wa Waswahili) Mombasa

8. Kanga si kwa rangi yake * Bali ni kwa jina lake
Mswahili aipeke * Ndipo iwapo hidaya

9. Zina mafumbo adhimu * Mangine nimebakiza
Yataka mtalamu * Mafumbo ya kumweleya

10. Ni mengi tukieleza * Mangine nimebakiza
Ya ndani ya kushangaza * Somani yataweleya

11. Nimekoma kikomoni * Kwa niyaba ya Ngomeni
Ahamadi Nabahani * Kanga nae mechangia

Ubeti wa kwanza wa shairi hili unatujulisha kuwa, kanga si vazi geni katika maisha ya Mswahili – vazi hili limekuwepo tangu kale. Matumizi ya kanga yanayojitokeza katika shairi hili ni:

a) Kupokea na kuadhini mwana anapozaliwa
b) Kupamba mama na mpokezi mwana anapozaliwa
c) Kusitiri mwana mwali anapobalehe
d) Zawadi wakati wa kuolewa
e) Kuosha maiti
f) Zawadi kwa marafiki
g) Kuwasiliana kwa mafumbo

### 2.4.1 Vazi la Malezi ya Watoto

Vazi hili anavyoeleza Nabhany katika shairi lake, humwandama Mswahili tangu kuzaliwa hadi kufa. Mara tu mtoto anapozaliwa, hupokelewa kwa kanga laini (Tazama picha 8). Mama na mkunga wake pia hupewa zawadi za kanga zenye maneno kama: *Nani kama mama, Mama nilee vyema uepuke lawama* au *Raha ya dunia ni watoto*, ili kuwapongeza kwa kazi ya kumleta mwana duniani huku wakitoa ujumbe wa heri njema, dua na ushauri wa malezi. Mtoto huyu anapozidi kukua, kanga kuu kuu hutumiwa kama napi. Wenyeji huziita *'kibundo'*. Inaaminika kuwa napi za kanga ni nzuri zaidi ya napi za kawaida (za kununua) kwani 'hazimchomi' mtoto hasa inapozingatiwa kuwa mazingira ya Pwani ya Kenya ni ya joto jingi. Vazi hili pia hutumiwa kumbeba mtoto mgongoni huku mama akifanya shughuli zingine za nyumba. Isitoshe, kanga hutumiwa kumfunika mtoto anapolala. Swala lingine linalotiliwa maanani katika uwanja wa malezi ni umuhimu wa maziwa ya mama. Kanga imetumiwa kueneza ujumbe kuhusu umuhimu huu kwa kuwepo kwa maneno kama: *Maziwa ya mama ni tamu* na *Maziwa ya mama ni bora.*

Tofauti baina ya mtoto wa kike na mtoto wa kiume ni kwamba maisha ya yule wa kike hufungamana na kanga daima. Mtoto wa kike anavyozidi kukua, mamake ana jukumu la kumnunulia mwanawe kanga ili apate mazoea ya kulitumia vazi hili kwani pindi tu anapobalehe, ni lazima ajisitiri kwalo. Wakati huu kabla ya kubalehe, mtoto huyu hujifunga kishingoshingo au akajitanda nalo.

Wacharo (2003), anaeleza kuwa, msichana Mswahili anapovunja ungo, hupewa gora kadhaa za kanga kulingana na uwezo wa familia yake. Wakati huu ni muhimu katika

maisha ya mtoto huyu wa kike kwani sasa anaanza kufunzwa kazi za nyumbani kama kupika, kufua, kusafisha nyumba na kushona.

Kama anavyosema Nabhany katika ubeti wa tano wa shairi lake, mara tu msichana wa Kiswahili anapokuwa tayari kuolewa, jamaa na marafiki humpa kanga nyingi kama zawadi. Vilevile kungwi wake hupewa kanga kama shukrani kwa kazi yake.

### 2.4.2 Vazi la Ndoa na Unyumba

Katika ndoa, kazi ya kanga huanzia arusini na kuendelea hadi nyumbani kwa waliooana. Arusini, kanga hutolewa kama zawadi kwa bibi arusi na wakati mwingine, kanga hutandikwa chini ili bibi arusi na msafara wake wazikanyage wakitoka nyumbani kuelekea arusini (Tazama picha 9 na 10). Jamaa na marafiki nao huvaa sare za kanga zenye ujumbe wa heri njema kwa maarusi wakati wa sherehe ya arusi. Sare hizi huchaguliwa kwa makini na mara nyingi, maarusi hujitungia ujumbe mahsusi. Ifuatayo ni mifano ya ujumbe tuliosoma kwenye sare za arusi: *Pendo la dhati huwa ni la kila wakati*, *Siri ya ndoa aijuae ni mke na mme, ua langu la moyoni lanipa raha maishani* na *Arusi ni nguzo ya jamii.*

Maswala ya kimapenzi pia huwasilishwa kupitia kwa kanga ambapo wapendanao hutumia vazi hili kupitisha ujumbe kuhusu hisia zao. Mwanamke anaweza kujifunga kanga yenye ujumbe wa mapenzi kwa mpenziwe ama mwanamme akamnunulia mwanamke anayempenda kanga yenye ujumbe wa mapenzi. Marafiki wa dhati pia hununuliana kanga zenye maneno ya mapenzi. Vazi hili linachukua nafasi ya maua mekundu ya waridi yatolewayo kama ishara ya mapenzi katika nchi za kimagharibi. Tofauti ni kuwa vazi hili ni ishara ya kudumu kwa mapenzi ikilinganishwa na ua

linyaukalo baada ya siku chache. Ama kwa kweli vazi hili ni nguzo muhimu katika mapenzi kwani kwalo, watu huwasiliana na kufanya wawili wapendanao wajuane na waelewane.

Chumbani ni mahali muhimu katika maisha ya ndoa hasa inapozingatiwa kuwa ni hapa ambapo wawili waliooana huwa peke yao na hushiriki maisha ya ndoa kikamilifu. Kazi ya kanga hudhihirika hata chumbani. Mbali na kuvaliwa kama vazi la kulala ambapo mume hujifunga kipande kimoja na mke akajifunga kingine, vazi hili hutumiwa kupitisha ujumbe chumbani. Mara nyingi ujumbe huu huwa wa kukiri mapenzi, shukrani, kujieleza kuhusu maswala ya kuudhi na kufahamisha kuhusu hali fulani. Miongoni mwa mifano ya jumbe hizi ni: *Harufu yako yautuliza moyo wangu, Ukipenda waridi utavumilia miiba, Penzi ni jani hunawiri likiwa moyoni* na *Sauti yako yanipumbaza.* Kanga zenye ujumbe kama huu hutandikwa kitandani ili mume anapoingia ausome. Kanga hizi hubadilishwa mara kwa mara kwa kutegemea hali na mawasiliano katika ujumbe unaokusudiwa. Watafitiwa wetu walitujuza kuwa ikiwa mke alikuwa katika hali ya furaha na ya kumtaka mumewe kimapenzi, kanga 'ingemsemea' hata bila yeye kutumia mdomo wake. Mke huyu alihitajika tu kutandika kanga yenye maneno matamu, kisha ainyunyizie asmini au marashi ya kuvutia. Mwanamume yeyote mwenye kuuelewa utamaduni wa Kiswahili angeusimbua ujumbe huo na kufahamu alichotaka mkewe.

### 2.4.3 Vazi la maombolezo ya Kifo[5]

Maisha ya binadamu huishia kwa kifo. Vivyo hivyo, kazi ya kanga kwa Mswahili pia huishia kwa kifo. Katika jamii zingine, msiba unapotokea waathiriwa hunyoa nywele,

---

[5] Si Wapwani wote wanaoosha maiti zao na kuzifunga kwa kanga. Waswahili ndio wenye desturi hii.

wengine hujipaka matope meusi na wengine huvaa sare nyeusi ili kuashiria maombolezi. Katika jamii ya wapwani, mtu anapokufa (mwanamme au mwanamke) huoshwa kwa kanga. Kama ni mwanamke, kanga hufungwa katikati ya jeneza lake ili hata bila kuuliza, watu wote wajue kuwa aliyekufa ni mwanamke. Sheikh Mubarak[6] alihusisha tabia hii ya kufunga jeneza kwa kanga na kule kukosekana kwa kivumishi awali cha kuonyesha umaalum wa kijinsia katika lugha ya Kiswahili kwa hivyo kuleta utata hasa wakati wa kuombea aliyekufa kwani katika dini ya Kiislamu, wanawake na wanaume hufanyiwa sala tofauti. Wakati huu wa maombolezi, waombolezaji hujitanda kanga zenye maneno ya kuomboleza kama: *Umetuachia kilio na majonzi, Nasononeka moyoni kwa yaliyotufika* na *mpendwa wetu safiri salama.*

### 2.4.4 Vazi kama mali

Kadri vazi hili linavyozidi kukita mizizi ndivyo dhima yake miongoni mwa Wapwani wa Kenya inavyozidi kuimarika. Kwa mfano, wanawake wengi hutumia vazi hili kama akiba. Wao hukusanya gora nyingi kwa kuhakikisha kuwa hawakosi kununua kanga mpya kila inapotoka (kanga mpya hutoka mara mbili kwa mwezi). Kanga hizi huwafaidi wakati wa shida kwani wao huziuza na kutumia pesa hizo kusuluhisha shida zao. Wakati mwingine wao huzibadilisha na chakula au mali.

### 2.4.5 Kifaa cha Burudani

Aidha kanga ni njia mojawapo ya kujiburudisha (hobby). Bi Amina Abubakar wa Majengo ni mfano mmoja wa wanawake wanaokusanya kanga kama njia ya kujifurahisha tu. Mkongwe huyu alituonyesha kabati lililojaa kanga na akatueleza kuwa amekua akinunua angaa gora moja kila mwezi tangu alipoolewa mwaka wa

---

[6] Sheikh Mubarak Abdulqadir ni Afisa wa Elimu katika jumba la makumbusho la Fort Jesus na alikuwa mmoja wa watayarishi wakuu wa maonyesho ya *'Usiache mbachao'*

1955 na mumewe pia humnunulia kanga mpya kila mfungo wa ramadhani. Bi Amina alidai kuwa yeye ndiye alikuwa na kanga nyingi kushinda kila mtu mtaa wa Majengo. Dai hili huenda likawa la kweli kwani kabati hilo ni kubwa mno na imemchukua muda wa miaka 52 kuzikusanya. La ajabu ni kuwa, kanga nyingi katika kabati hilo bado zinaonekana mpya utadhani ziko dukani tayari kuuzwa.

### 2.4.6 Kitambulisho cha hadhi Kijamii

Mbali na kujifurahisha utafiti ulituonyesha kuwa, wanawake wengine walitumia kanga kuonyesha hadhi yao katika jamii. Mwenye gora nyingi alionekana kama mtu mwenye kujiweza kiuchumi. Kukosa kanga mpya kila mwezi kulifasiriwa kama kufilisika na kuishiwa na wagomvi wa mhusika. Hali kama hii ilizua kugoana na hata kununuliana kanga za maneno ya uchokozi.

### 2.4.7 Kanga kama Zawadi

Miongoni mwa Waswahili, zawadi ni kitu muhimu kwani inaaminiwa kuwa zawadi huimarisha uhusiano baina ya wanajamii. Zawadi hizi hujumuisha chakula, mapambo, pesa, mavazi na vitu vingine vya thamani. Kanga hutolewa kama zawadi kwa kungwi, mama mkwe, wifi, majirani, dada na marafiki. Wanaume wanaweza kuwapa jamaa na marafiki wao wa kike kanga lakini wao hawaruhusiwi na utamaduni wa Kiswahili kupelekeana waume kwa waume kanga kama zawadi.

### 2.4.8 Kanga kama vazi maalum la dansi

Kanga pia hutumiwa kama vazi maalum katika dansi za kitamaduni kama chakacha, lele –mama, vugo, shangani, chano, kirumbizi na chama.

## 2.5 Usawiri wa Maswala ya Kijamii yanavyojitokeza katika kanga

Kwa mujibu wa Fisher (1984), Mwafrika havai kujirembesha tu bali huvaa akiwa na kusudi la kuonyesha alikotoka, umri wake na hadhi yake katika jamii. Tunakubaliana naye kwani hali hii ilidhihirika wazi katika utafiti huu hasa wakati wa sherehe maalum kama arusi na matanga. Tuligundua kuwa, wanawake Wapwani hawavai kwa ajili ya kujistiri tu bali huvaa kuonyesha hadhi yao, imani yao, hali yao ya ndoa na matukio ya wakati fulani. Kwa mfano, ukimuona mtu na kanzu au buibui, utajua wazi kuwa mtu huyo ama ni Muislamu au anaiga Uislamu.

Mwanamme akionekana akiwa na kanga wakati wa kwenda kulala, basi hicho ni kitambulisho cha kuonyesha kuwa mwanamme huyo ameoa.[7] Kwa upande mwingine, msichana hujifunga kanga kishingoshingo (mtindo wa kujifunga kanga ambapo pembe za kanga hupitishwa mkingamo shingoni kisha zikafungwa) ilhali mwanamke aliyeolewa hujifunga kanga moja kifuani akajitanda nyingine kichwani au akajifunga moja kiunoni na kujitanda nyingine (mtindo unaoitwa matiti matiti). (Picha 11 – 15 )

Aidha, imani na utamaduni wa wahusika huweza kutambulika kutokana na matumizi yao ya lugha kwa mfano, kuna kanga yenye maneno: *Mme ni kazi mke ni tabia* Maneno haya yanasawiri imani na tabia za wapwani wa Kenya ambapo wanaume wanatarajiwa kufanya kazi na kugharamia maisha ya wanawake wao kwa kila hali (kimavazi, chakula, makaazi, mapambo na mahitaji yote kwa jumla). Wanawake nao wanatarajiwa kuonyesha mapenzi kwa kuwapikia na kuwahudumia waume zao

[7] Wanaume hawatoki nje na kanga bali hujifunga kanga nyumbani wakati wa kulala.

nyumbani. Hali hii ilidhirika wazi katika maduka ya Kiswahili [8]ambapo hakuna hata mwanamke mmoja aliyeonekana akiuza wala kuhudumu hapo.

Kutokana na utafiti wetu, wapwani hawanunui kanga kwa sababu ya maua ama rangi yake bali maneno yake. Hata hivyo, ili kufanya mavazi haya yawe ya kuvutia zaidi, watengenezaji na wauzaji hujaribu kutengeneza na kuuza kanga zenye rangi tofauti ili kila mnunuzi apate rangi inayompendeza. Kwa hivyo, kanga zenye maneno sawa huweza kuwa za rangi tofauti. Yaani, kunaweza kuwa na kanga nyeupe, nyekundu, ya kijani kibichi na nyingine ya rangi ya damu ya mzee na maneno katika kanga hizi zote yawe sawa. Labda; *Wajua tamu yaua sumu umenipeani.*

## 2.6 Usawiri wa Maswala Ibuka kwa kutumia kanga

Kadri mambo mapya yanavyozidi kuibuka ndivyo mada za kanga pia zinavyozidi kubadilika ili kusawiri hali ilivyo katika jamii. Mbali na siasa na uchumi, maswala ya kijamii kama ndoa, mavazi, dini na tabia za binadamu zinazidi kubadilika kutokana na athari za kiwakati na utangamano baina ya jamii zenye tamaduni tofauti.

Vizazi tofauti huja na mitindo tofauti hasa katika uwanja wa mavazi. Kwa mfano, kitambo kidogo, wanawake Waafrika walitakikana kuvaa marinda na skati. Leo, ni kawaida kuwaona wanadada na kila aina ya suruali ndefu (Long'i) Hali hii pia imeonekana katika mada zinazojitokeza katika kanga. Mada za kanga hubadilika kutegemea wakati na matukio ya wakati huo. Vazi hili hufanya kazi muhimu ya kueneza ujumbe kuhusu mambo mapya yanayokumba na kupitikiwa jamii.

[8] Maduka yanayomilikiwa na Waswahili

### 2.6.1 Magonjwa

Afya ya mwanadamu ni nguzo muhimu ya maisha yake. Hii ni kwa sababu, mara nyingi mtu mnyonge hawezi kujiendeleza wala kuiendeleza jamii. Maishani kuna magonjwa mengi yanayomsumbua binadamu kama; malaria, kupooza, kipindupindu na kifua kikuu. Hivi karibuni, kumezuka magonjwa mengine kama Ukimwi na kifua kikuu 'kisichosikia' dawa . Ili kukabiliana na magonjwa haya mapya, wadau wameibua njia za kujulisha na kutahadharisha jamii kuhusu magonjwa haya na jinsi ya kukabiliana nayo. Miongoni mwa nyenzo zinazotumiwa ni: mabango na vyombo vya habari. Wakati mwingine, ujumbe kuhusu magonjwa haya huenezwa katika mikutano ya hadhara. Kanga pia inatumiwa kueneza ujumbe kuhusu magonjwa.

Kabla ya kuzuka kwa ugonjwa hatari wa Ukimwi, hakuna kanga zilizozungumzia ugonjwa huu lakini sasa kuna kanga zenye ujumbe kama:

*i.* *Janjaruka uishi,*
ii. *Utamaliza bucha nyama ni ile ile*
*iii.* *Wamharakisha mwenzio kuzimu wewe utaenda wapi?*
*iv.* *Tuliza boli uwanja mdogo*
v. *Inua guu gongo laja*.

Misemo i, ii, iv na v ama inaonya au inatahadharisha dhidi ya mapenzi ya kiholela. iii nao unaonya dhidi ya kuwadunisha  na kuwafedhehesha wagonjwa wa Ukimwi bila kujua hali zetu.

Mazungumzo yetu na mfanyikazi wa shirika la Red Cross mjini Mombasa Bi Agnetta Masha, yalituonyesha kuwa mawasiliano ni kipengele muhimu katika kupigana na

janga la Ukimwi na magonjwa mengine katika jamii. Mwanadada huyu alisema, *"Ukimwi umekuwa nasi tangu miaka ya thamanini lakini bado watu wetu hawajauelewa na kuukubali. Kwa hivyo ni muhimu mashirika yanayoshughulikia ugonjwa huu yaihusishe jamii kikamilifu. Labda itafaa zaidi kama mashirika haya yatafungamanisha desturi zetu Wapwani na vita vyake dhidi ya Ukimwi. Mashirika haya yatumie misikiti yetu, madrasa, mabaraza ya machifu, kina kungwi, waimbaji wa taarab na bango na wauzaji wa kanga ili kuwafikia watu wengi zaidi na kuuwasilisha ujumbe wao kwa njia zinazoeleweka na wanajamii. Ni rahisi kumfikia mtu kwa kutumia lugha na nyenzo anayoelewa kuliko kutumia lugha na nyenzo mpya kwake."*

### 2.6.2 Siasa

Fairclough (1989) anasema kuwa lugha ndio msingi wa kueleza maswala ya kijamii, uongozi na utawala. Anashereheshea kuwa sera za serikali hufaulu au kutofaulu kutegemea lugha inayotumiwa kuziwasilisha.

Wanasiasa wa Pwani ya Kenya, wameonekana kutambua uwezo wa kanga nao wakaitumia katika kampeni zao za kisiasa hasa wanapoomba kura na kueneza sera zao. Kwa mfano katika kampeni za 2002, mwanasiasa Najib Balala alitumia kanga yenye jina *Sina siri bali nina jibu* kumpiga vita mwenzake Sharif Nassir. Ujumbe huu unaweza kufasiriwa kwamba, Najib Balala alikuwa na jibu kwa shida za Wamvita ilhali Nasir alikuwa na siri tu. Balala alichanganya majina yao kutunga ujumbe huo. Si Nasir (Sharif Nassir) bali ni Najib (Balala). Wanasiasa wa chama cha KANU nao walitoa kanga zenye picha ya jogoo na maneno *KANU chama cha raia* ili kuwavutia wafuasi wao.

Katika kampeni za 2007, mavazi yalifanya kazi muhimu ya kueneza sera za vyama mbalimbali. Mbali na hayo, mavazi yalitumiwa kujitambulisha na vyama fulani. Fulana za mikono, kofia na kanga za rangi zilizotumiwa kama kitambulisho cha kundi fulani zilitengenezwa. Kwa mfano, makundi ya ODM na ODM – Kenya yaliwakilishwa na rangi ya chungwa huku chama cha PNU kikiwakilishwa na rangi nyeupe, nyekundu na rangi ya samawati.

Kanga inaweza kufananishwa na kadi ama fulana za mikono (T- shirts) zinazotumiwa kueneza ujumbe kuhusu maswala tofauti. Kama fulana za mikono kuna kanga zenye nembo za vyama mbalimbali, miito ya vyama vya kisiasa na mahubiri ya makanisa. Hali hii pia ilidhihirika katika kampeni za 2007 ambapo miito kama *Kibaki Tena, Kazi iendelee, Kazi ianze na Raila* na *Chungwa moja maisha bora* ilitumiwa katika kanga za kampeni. Kanga , fulana fupi na kadi zina sifa sawa kiuamilifu hasa tunapozingatia swala la mawasiliano.

### 2.6.3 Haki za Wanawake na Watoto

Misimamo na mitazamo ya wanajamii kuhusiana na namna wanavyosawiri ulimwengu wao inaweza kudhihirika kutokana na jinsi wanavyotumia lugha teule kuwasilisha maswala tofauti yanayowakumba.

Pia kanga hutumiwa kueneza ujumbe kuhusu maswala kama haki za wanawake na watoto. Mbali na taarab na nyimbo za arusi wanawake wapwani hawana majukwaa (platforms) ya kutosha ya kujieleza. Kanga inawapa wanawake hawa fursa ya kusema yanayowakera huku wakielimishana, kushauriana na kuwasiliana.

Kanga nyingine iliyobeba ujumbe mzito wa kumzindua mwanamke au kutahadharisha wanaosisitiza hali na lazima ya kupata mtoto katika ndoa ilikuwa na maandishi:

*Kuolewa ni sheria kuzaa ni majaliwa.* Mara nyingi wanawake wasioweza kupata watoto hujilaumu kwa hali hii bila kujua kuwa mbali na kuwa majaliwa, ukosefu wa mtoto waweza kutokana na matatizo ya mwanamume au mwanamke. Haya ni kwa mujibu wa mtafitiwa aliyekuwa amejitanda kanga ya aina hii. Mtafitiwa huyu alituhadithia jinsi alivyovamiwa na wifi zake kwa kutopata watoto tangu aolewe. Ili kuwafunga midomo alinunua kanga yenye ujumbe huo. Ingawa hawakukoma mara moja, alikiri kuwa vita vilipungua na sasa ana amani.

### 2.6.4 Maswala mengine

Maswala mengine muhimu yanayoikumba jamii ni ukabila na maswala ya mazingira. Katika maeneo haya, majina kama: *penzi halina kabila wala mila* na *panda miti uzuie mmomonyoko wa udongo.* Kadri maswala mapya yanavyoibuka katika jamii ndivyo kanga zinazowasilisha ujumbe kuhusu maswala haya zinavyoibuka.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imefafanua asili na dhima za kanga. Utalii huu wa kuzama katika historia umekuwa muhimu kwetu kwani kwao, tumejenga msingi wa utafiti wetu. Kadhalika sura hii imetupa jibu kwa swali letu la kwanza: *Vazi la kanga lina dhima gani katika jamii ya Wapwani wa Kenya?* Kwayo, tumejua kuwa mbali na kusitiri uchi na kuwasilisha ujumbe, kanga ina kazi chungu nzima kuanzia kuzaliwa kwa mwana hadi kifo. Isitoshe, tumeonyesha kuwa mila na desturi za wapwani zina uhusiano wa moja kwa moja na matumizi ya kanga. Sura ya tatu imejikita katika dhima kuu ya kanga ambayo ni mawasiliano. Sura hii inafanya hivi kwa kuainisha dhamira mbalimbali 'zinazozungumziwa' katika kanga kwa kuhusishwa na miktadha maalum ya mawasiliano kiamali.

# SURA YA TATU

# MAWASILIANO KUPITIA KWA KANGA

## 3.0 Utangulizi

Sura ya pili imefafanua asili na dhima za kanga miongoni mwa wakaazi wa Pwani ya Kenya. Sura hiyo imethibitisha kuwa matumizi ya kanga hayajaanza leo bali yamekuwepo tangu enzi za mababu zetu. Tofauti ni kwamba matumizi ya vazi hili yanazidi kuimarika kadri wakati unavyopita na maswala kuibuka na kuchangamana. Aidha, sura hiyo imeonyesha wazi kuwa vazi hili linazidi kuimarika kiuamilifu.

Katika sura hii ya tatu tunaangazia kipengele cha mawasiliano hasa kwa kuzingatia kanga kama makala na zana iliyokita mizizi miongoni mwa wapwani wa Kenya. Mbali na kusitiri uchi, dhima nyingine kuu ya kanga ni kuwasilisha ujumbe.

Mbali na hayo, tunadai na kubainisha kuwa, hakuna jambo lisiloweza kuwasilishwa kupitia kwa kanga. Ili kuthibitisha haya, tumechanganua data ya kutokana na makundi tofauti ya watu wanaoshiriki biashara na matumizi ya kanga. Inavyotokea ni kuwa, katika maisha, kuna kupenda na kupendwa, kuchukia na kuchukiwa, kufurahi na kukasirika. Vilevile, inatokea kuwa kanga hutumiwa kujieleza katika maswala ya hasira, msiba, sherehe na hata ya furaha. Kwa mfano, ikiwa jirani atasikia kuwa mwenzake anamsema, basi jirani huyu anaweza kumkomesha umbea kwa kumvalia kanga ya yenye maneno: *Mgonjwa hupewa dawa je mdaku hupewa nini?* Ama *Yenu siyaulizi yangu mwayatakiani?*

Ili kuyafafanua madai yetu kuwa kanga hutumiwa kuwasilisha ujumbe kuhusu maswala ya kijamii, tutaainisha majina yote tuliyopata katika makundi kimada/

kimaudhui, kisha tufafanue misemo/maneno matano ya kwanza katika kila kundi. Orodha itakayotumiwa ni ile iliyotokana na utafiti nyanjani – hakuna marekebisho yaliyofanywa wala haijabadilishwa. Imenukuliwa sisisi. Majina yaliyobaki yamewekwa kwenye kiambatisho.

Ni muhimu itajwe mapema kuwa ni vigumu kuainisha kikamilifu majina ya kanga katika tasnifu hii hasa ikizingatiwa kuwa, maana hutokana na matumizi kimuktadha. Isitoshe, watu tofauti huweza kufasiri ujumbe mmoja kwa njia tofauti kutegemea tajriba zao, asili zao, mila na desturi zao na hata umri. Anavyosema Beck (2005) wakati mwingine majina ya kanga huwa na maana mbili au zaidi (equivocal). Nadharia ya uamali imefanikisha uchunguzi huu kwa kuonyesha ni vipi sentensi moja inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti kutegemea miktadha ya wanaowasiliana, mada na muktadha wa mawasiliano. Mifano mitatu ifuatayo inafafanua hoja hii kinagaubaga zaidi:

1. *Nyumba yenye upendo haikosi visiki*

a) Maneno haya yanaweza kuwa ushauri kwa mwana anayeolewa kutoka kwa mamake anayempa kanga hiyo kama zawadi arusini.

b) Vile vile yanaweza kuwa maneno ya kuomba msamaha; mke akamtandikia mumewe kitandani ili kuonyesha kuwa anajuta alichofanya au kusema.

c) Pia inaweza kuvaliwa na mwanamke anayesengenywa na majirani kutokana na shida zinazoikumba nyumba yake. Kanga hii ikatumiwa kuwaonyesha kuwa ingawa ana matatizo katika nyumba yake, anaelewa kuwa shida ni jambo la kawaida katika ndoa na anaweza kukabiliana nazo.

2. *Raha ya dunia ni watoto*

a) Kanga yenye maneno haya inaweza kutolewa kama zawadi kwa mama aliyejifungua ili kumpongeza.

b) Kanga hii pia inaweza kutolewa kama zawadi ya 'uchokozi' kutoka kwa wifi au mke mwenza kwa mwanamke tasa.

c) Aidha, kanga hii inaweza kutumiwa kupiga vita tabia ya kuavya mimba miongoni mwa wanawake.

3. *Nyumba hujengwa na mke*

Maana ya kanga hii inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti.

a) Kwanza, inaweza kuwa zawadi yenye mawaidha kwa mwanamke anayeolewa.

b) Pili, kanga hii inaweza kuvaliwa ili kumkejeli mwanamke anayeonekana 'kuibomoa' nyumba yake.

c) Kanga hii pia inaweza kutumiwa kuihimiza jamii kuwaheshimu wanawake kwani wao ndio hujenga jamii.

Mifano hii inadhihirisha madai yetu kuwa kanga moja inaweza kufasirika kwa njia tofauti kutegemea wahusika na muktadha wanamoshiriki mawasiliano.

Katika mawasiliano kupitia kwa kanga, lugha inayotumiwa inaweza kuwa ya moja kwa moja – yaani inayobeba maana wazi au iwe ya mafumbo. Aidha, mawasiliano yanaweza kuendelezwa kwa kutazama tu jinsi kanga ilivyovaliwa bila hata kusoma maneno yaliyo kwenye kanga.

### 3.1 Dhana ya Mawasiliano

Mawasiliano ni mchakato unaohusu kusambaza ujumbe kutoka kwa chanzo chake hadi kwa mpokeaji/wapokeaji ujumbe huo. Mawasiliano hutokana na haja ya wanajamii kuelezana mambo fulani kwa kutumia lugha na nyenzo inayoeleweka na kukubalika na wahusika.

Dhana ya mawasiliano si ngeni katika mandhari ya Kiafrika kwani, mawasiliano yamekuwepo tangu jadi. Mbinu za mawasiliano zilizotumiwa na Waafrika ni kama: Maongezi ya kawaida, nyimbo, ushairi, kupiga ngoma, kupuliza firimbi, kuwasha moto, kupiga mbiu ama kutoa sauti maalum ili kuwasilisha ujumbe fulani. Labda ndio kukazuka msemo wa Kiswahili, *'Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo'.*

Kutokana na athari za kigeni na maendeleo ya kiteknolojia, leo tuna mbinu kama kupiga picha, kupiga simu,  kutuma ujumbe mfupi, kutuma barua pepe na kutuma barua kwa njia ya posta. Mbinu nyingine ya mawasiliano katika pwani ya Kenya inayozidi kuimarika kadri miaka inavyozidi kwenda ni mbinu ya kutumia kanga kupitisha ujumbe. Katika utafiti huu, kanga imechukuliwa kama ishara maalum yenye kubeba ujumbe. Mwongozo wetu wa kinadharia unahimiza watu kuwa makini katika kufasiri maana kwani kila ishara ina maana na ishara moja inaweza kumaanisha vitu tofauti kwa watu tofauti kutegemea miktadha wanamoshiriki mawasiliano. Hapa swala la muktadha linajitokeza. Je, mawasiliano kupitia kwa kanga hufanyika katika muktadha upi?

Kwanza, lazima kuwe na sababu ya kusimba ujumbe fulani. Kwa mfano, kuwe na arusi. Pili, wahusika (msimbaji ujumbe na msimbuaji ujumbe) washiriki utamaduni

sawa au waelewane. Itakuwa vigumu kuwasiliana kama mhusika mmoja haelewi lugha inayotumiwa ama kama mhusika mlengwa (anayelengwa na ujumbe) haelewi kuwa kanga ina uwezo wa kuwasilisha ujumbe. Katika hali kama hii, huenda mtu akapewa kanga ya kumkejeli kama yenye 'kusema' *Dunia ni mapito binadamu acha maringo* na aipokee bila kujua kilichokusudiwa na aliyempa zawadi hiyo. Ikiwa mhusika mmoja hataelewa kilichomaanishwa na msimbaji ujumbe, basi mawasiliano yatakuwa hayajakamilika.

Tatu, lazima lugha inayotumika ikubalike. Kuna tofauti baina ya lugha inayotumiwa kuandika majina katika kanga za kuwasilisha ujumbe tofauti tofauti. Kwa mfano, kanga za arusi huwa na lugha ya kupongeza, kuhimiza na kukiri mapenzi. Lugha ya kanga za matanga nayo huwa ya kuomboleza. Itakuwa jambo la ajabu kwa mtu kununulia bibi arusi kanga yenye maneno *Nasononeka moyoni na moyo wazidi kulia.* Kanga hii itaeleweka kusema kuwa aliyempa zawadi hiyo hakufurahishwa na arusi.

Wakati mwingine kanga yenye jina sawa huweza kufasiriwa tofauti kutegemea wahusika, wakati na matukio ya wakati huo. Mfano mzuri wa kanga kama hii ni ile yenye maneno: *Mpendwa wetu safiri salama.* Tuliona kanga hii katika mojawapo ya matanga tuliyohudhuria. Katika matanga haya kifo kilifananishwa na safari – mtu aagapo dunia huwa amesafiri. Kanga yenye ujumbe huo huo inaweza pia kutolewa kama zawadi kwa mtu anayesafiri kwenda mahali pengine. Mfano huu unadhihirisha kuwa, muktadha ni kipengele muhimu katika mchakato wowote wa mawasiliano.

Ili kupata maana kiuamali, lazima maswala zaidi ya yale ya kiisimu yazingatiwe. Haya ni kwa mujibu wa Carston (1999). Katika mfano wetu wa awali *(Mpendwa wetu*


*safiri salama),* tunaona kuwa ni muhimu kuhusisha ujumbe na matukio ya wakati huo ili kupata maana iliyokusudiwa na msimbaji ujumbe. Kama kuna safari, basi kanga hii ni ya kumuaga anayesafiri na kumtakia safari njema. Kama kuna kifo, basi kanga hii ni ya kuomboleza na kumtakia mwenda zake ‘safari njema kwenda ahera’. Labda wahusika (wanaoomboleza) wanaamini kuwa kufa ni kusafiri kutoka duniani hadi ahera.

Harris (1993) anasema kuwa, kitovu cha mawasiliano ni ile haja ya kupasha ujumbe. Anazidi kudai kuwa, mara nyingi ujumbe unaweza kutungwa bila nia ya kumlenga mtu au hadhira mahsusi bali kumfurahisha tu mtunzi. Hali hii pia hujitokeza katika mawasiliano kupitia kwa kanga ambapo mtu hununua kanga iliyomfurahisha bila kuwa na lengo la ‘kusema’ lolote.

Utafiti huu uligundua kuwa tabia hii ni hatari kwani inaweza kufanya aliyenunua kanga fulani aeleweke visivyo. Bi. Amina ni mmoja wa wale walioeleweka vibaya baada ya kununua kanga iliyompendeza. Mwanamke huyu alitueleza kuwa alikuwa amemsindikiza rafiki yake kununua kanga aliposoma kanga moja iliyosema *‘Nimepata Ji<u>baba</u> lijualo ma<u>haba</u>’.* Ingawa hakuwa na jibaba lolote, majirani walioisoma kanga hiyo walimfitini kwa mchumba wake hadi akaachwa. Amina alikiri kuwa alijuta kununua kanga hiyo kwani ilimfanya ampoteze mchumba wake. Kisa hiki kilithibitisha ‘nguvu’ za kanga katika Pwani ya Kenya. Kama Amina angejua athari ya kanga hii kabla ya kuinunua, bila shaka hangeinunua. Badala yake, angenunua kanga isiyoweza kufasirika visivyo.

Vielezo I na II vya Harris (1993) vinatoa muhtasari wa mchakato wa vimiliki vya mawasiliano.

**Kielelezo I**





Kielelezo hiki kinajumuisha elementi zifuatazo:

- Ujumbe: Anachotaka mtumaji ujumbe kimfikie mlengwa wake.
- Mtumaji ujumbe: Huyu ni yule mtu anayetuma ujumbe. Katika muktadha wa utafiti huu, anayevaa au kutoa kanga kama zawadi ndiye mtumaji ujumbe.
- Njia: zana inayotumiwa kufikisha ujumbe. Hapa, kanga ndio zana.
- Mpokeaji ujumbe: Anayelengwa na ujumbe.

Nadharia na Mchakato wa mawasiliano kwa mujibu wa Harris (1993)

**Kielelezo II**



Kielelezo II kinafafanua zaidi mchakato wa mawasiliano. Katika mawasiliano kupitia kwa kanga, anayetunga ujumbe ni tofauti na anayeutuma ujumbe huo. Wauzaji hununua kanga kutoka kwa watengenezaji zikiwa na ujumbe. Kutokana na utafiti huu, tuligundua kuwa majina ya kanga 'huchotwa' kutoka kwa mashairi, nyimbo za taarab, bango, methali na wakati mwingine wanawake hubuni majina na kuwapa wauzaji ili watengenezewe kanga maalum. Tumeeleza hali hii kwa jedwali lifuatalo:

**Jedwali I**

| ***Mtunzi wa ujumbe*** | ***Mnunuzi wa kanga (kuvaa mwenyewe au kutoa zawadi)*** | ***Mpokea ujumbe*** |
|---|---|---|
| Hutunga ujumbe kwenye kanga | Husimba ujumbe,akachagua kanga fulani kama njia ya kuwasilisha ujumbe wake | Husimbua na kuchanganua ujumbe |

Tukitumia vielelezo I na II kueleza mawasiliano kupitia kwa kanga, mtumaji ujumbe hununua kanga yenye maneno yanayofaa haja yake, kisha akajifunga au kujitanda ama hata kuitandika kanga hiyo kitandani ili kuwasilisha ujumbe aliokusudia. Aliyelengwa na ujumbe huu naye akaisoma na kupata kilichokusudiwa. Kwa mfano kama ni jirani  sabasi, asomapo kanga 'aliyovaliwa' yenye maneno '*Ujirani naupenda lakini tabia zimenishinda'* atajua wazi kuwa jirani yake anamlenga kwa maneno hayo. Ujumbe utamfanya atafakari ni nini kilichomuudhi jirani yake kisha aamue la kufanya. Kama  yeye pia ni mchokozi ama anaona ameonewa na labda jirani yake

ndiye mbaya, basi atamjibu kwa kanga yenye maneno kama vile: *Heri kumfadhili mbuzi binadamu ana maudhi*.

Kwa upande mwingine, kama mume ataingia chumbani na kupata kanga iliyonyunyiziwa asmini na iliyoandikwa *'Harufu yako yautuliza moyo wangu'* basi ataelewa ujumbe wa mkewe na ili kumjibu, huenda akamkumbatia au kufanya chochote kuthibitisha penzi lake kwa mkewe. Huku kukumbatia na labda kumbusu mkewe, ndio mwitikio unaorejelewa na Harris (1993) katika kielelezo II.

### 3.1.1 Wahusika katika Mawasiliano

Maswali muhimu ya kujiuliza unapochunguza mchakato wowote wa mawasiliano ni:

1. Je ni nani wanaohusika?
2. Je, msimbaji ujumbe ana nia gani?
3. Iwapo kuna kitu kinachoendelea maishani mwao chenye kushinikiza mawasiliano kupitia kwa kanga, kinaathiri vipi mahusiano baina yao?
4. Je, ni mila na desturi zipi zinazotawala mawasiliano kupitia kwa kanga?
5. Kwa nini msimbaji ujumbe (mnunuzi au mtoa kanga kama zawadi) huchagua kanga kuwasilisha ujumbe wake badala ya kutumia mbinu nyingine?

Tunapojibu maswali haya katika muktadha wa kanga kama makala yenye diskosi maalum, tunajipata katika hali ya kukubaliana na wanauamali kuwa, maana ya ujumbe huweza kufasiriwa na kutimiza uamilifu wa kimawasiliano kama wahusika wanashiriki imani, lugha, mandhari, wakati na muktadha sawa wa kimtagusano.

Katika utafiti huu, kundi tulilozingatia ni lile la wakaazi wa Pwani ya Kenya hasa wanawake. Kundi hili ni tofauti na makundi mengine ya wanawake kwani wanashiriki imani tofauti, mila na desturi za kipekee na wanaishi katika eneo mahsusi la kijiografia. Aidha, tabia zao zimeathirika pakubwa kutokana na mila na desturi za Waswahili.

Nadharia ya simiotiki ina msingi katika imani kuwa watu katika jamii moja; wanaozungumza lugha moja na kushiriki utamaduni, mila na desturi sawa huweza kuwasiliana kwa njia yao ya kipekee kutokana na kuelewa kwao kwa ishara mbali mbali zinazopatikana katika jamii yao. Watu hawa huwa na ukubaliano kuhusu ishara hizi na maana zake. Vivyo hivyo, wapwani wa Kenya kama jamii zingine zote wana upekee unaowatofautisha na jamii zingine. Miongoni mwa tofauti hizi ambazo zinawafanya kuelewa ishara mbali mbali katika jamii yao ni: lugha, utamaduni, mila na desturi zao, chakula, makaazi yao na mavazi.

Tulichagua kundi la wanawake kwa kuwa katika Pwani ya Kenya, wanawake ndio hutumia kanga kuliko kundi lolote lingine. Wanawake wapwani ni kundi la watu linaloongozwa na kanuni na masharti aghalabu yenye misingi ya Kiislamu. Mavazi, tabia na mienendo yao kwa jumla huwa inaambatana na kanuni zilizotungwa na Koran tukufu. Kwa mfano, ni sharti mwanamke Muislamu ajistiri kutokana na macho ya wanaume wote isipokua mume wake. Kwa hivyo, kila anapotoka nyumbani lazima avae buibui na ajitande kwa hijabu au mtandio. Urembo wake usionwe na mwanamume mwingine. Ikiwa mwanamke huyu atakua ndani ya nyumba, basi ajifunike kwa kanga. Mbali na dini ya Kiislamu hali hii huchangiwa na sababu za kihistoria ambapo tangu jadi, Waswahili wamekua wakiishi katika koo na miji yenye

jamaa wa koo moja. Kwa kuwa jamaa hawa walichanganyika, yaani kulikuwa na wajomba, mababu, ami na watu wengine waliostahili kuheshimiwa, ilikuwa lazima kwa wanawake wote kuvaa kiheshima.

Katika mawasiliano kupitia kwa kanga, wahusika wakuu huwa wauzaji, jamaa, marafiki, majirani, wapenzi, wake wenza, maadui, viongozi na makundi yasiyo ya kiserikali. Mara nyingi, huwa kunazuka haja ya kupitisha ujumbe fulani kisha mtumaji ujumbe akaamua mbinu mwafaka ya kuutuma ujumbe wake. Ikiwa atachagua kutumia kanga, basi ataenda dukani na achague kanga inayoweza kuufikisha ujumbe wake kwa njia mwafaka. Kwa mfano, ikiwa ni jirani anayemlenga jirani yake sabasi, basi atachagua kanga yenye msemo kama: *Utabakia hayo ya barazani ya ndani huyapati*. Majibizano huenda yakazuka na jirani naye 'akamnunulia' mwenzake kanga yenye kusema: *Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa*. Kama ni kundi lisilo la kiserikali linalosambaza ujumbe kuhusu Ukimwi, basi kanga yenye maneno kama *Janjaruka uishi* itatumiwa.

Ingawa si anayevaa/anayenunua kanga ambaye hutunga maneno yapatikanayo kwenye kanga kama tulivyoonyesha katika jedwali I, kule kwenda dukani na kuchagua kanga yenye ujumbe fulani kunampa uwezo na mamlaka ya kusimba na kuutuma ujumbe huo kama wake. Hata hivyo, kuna ruhusa ya mtu kujitungia ujumbe na kuupeleka kwa watengenezaji ili atengenezewe kanga yenye ujumbe maalum. Hali hii inamtoa muuzaji katika mchakato huu. Jedwali II linafasiri hali kama hii.

**Jedwali II**

| ***Mtumiaji ujumbe (Mnunuzi wa kanga)*** | ***Mpokeaji ujumbe*** |
|---|---|
| Husimba ujumbe kisha akauwasilisha kwa kuvaa au kutoa kanga hiyo kama zawadi | Husimbua na kuuchanganua ujumbe |

Mara nyingi, watu hujitungia majina ya sare za arusi na zile za maombolezi. Makundi ya kufanya kampeni za kisiasa na za kueneza maswala maalum ya kijamii pia hutunga misemo yao na kuagizia kanga maalum yenye ujumbe kwa walengwa wao. Kanga hizi zenye ujumbe maalum huwa ghali kuliko kanga zingine.

### 3.1.2 Diskosi katika Jinsia ya Kike

Katika utafiti huu, tuligundua kuwa Barbra na Pugh (1987) hawakukosea walipodai kuwa wanawake ni wepesi wa kusema na kuwasilisha hisia zao ikilinganishwa na wanaume. Miongoni mwa mbinu zinazotumiwa na wanawake wapwani kujieleza ni kupitia nyimbo za taarab, kupiga gumzo nje ya nyumba zao na kuvaa au kupeana kanga zenye ujumbe mahsusi. Mara nyingi, mawasiliano yao huwa yenye ucheshi, matusi na kejeli. Mawasiliano haya huwa na sifa zifuatazo:

i. Kubadilishana zamu
ii. Kudakia mazungumzo
iii. Kujibizana

Sifa kuu inayojitokeza katika mawasiliano kupitia kwa kanga ni kwamba kuna hali ya kujibizana ambapo mtu akisikia jambo linalomkera ama neno linalomuhusu yeye

hutumia kanga kulijibu. Kwa mfano, kama jirani mmoja anamsengenya mwenzake na kusema kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na mumewe, basi jirani anayesengenywa huenda akanunua kanga yenye jina: *Simtaki bwanako wangu ni mtamu* ama azue uchokozi tu kwa kumvalia mwenzake kanga yenye kusema *Kama unaweza mtie kamba mumeo.* Jina la kwanza linatoa hakikisho kwa jirani mwenye kulalamika kuwa, anayemshuku hana haja na mumewe kwani wake anamtosha ilhali jibu la pili linathibitisha kuwa ni kweli kuna uhusiano wa kimapenzi na mhusika anamwambia mwenzake amfunge mumewe ndio uhusiano huo uishe.

Wakati mwingine, majibizano hufanywa kwa kanga tu – hakuna majibizano yanayofanywa kwa  mdomo. Mathalan katika hali moja tuliyoelezewa, kuna mama aliyekaa na mumewe kwa miaka mingi bila kupata watoto. Kwa kuwa inatarajiwa kuwa watu wanapooana jamii inafaa kuendelezwa kwa watoto, mama mkwe alimnunulia mkaza mwanawe kanga ya kumchokoza yenye jina *Raha ya dunia ni watoto* kufikisha ujumbe kuwa amechoka kungoja wajukuu. Mkazamwana naye akanunua kanga yenye kusema: *Kuomba si kupata Mungu akitaka atakupa* kisha akavaa kipande kimoja na akampa mama mkwe kingine. Mama mkwe akajibu kwa kanga nyingine yenye jina *Si neno nitasubiri*. Hata hivyo, mama huyu alianza kumshawishi mwanawe aoe mke mwingine amzalie watoto. Jambo hili lilimsumbua sana mama huyu tasa na akaanza kudhoofika kiafya. Ili kumhakikishia mkewe kuwa hakuwa na nia ya kumuacha wala kuoa, mumewe alimnunulia zawadi ya kanga iliyosema: *Mimi na wewe hatuwachani.*

Mbali na wanawake kuwa wepesi wa kujieleza, wao hutumia lugha kisanii. Mifano ifuatayo ya majina ya kanga inadhihirisha kuwa wanawake wapwani huwasilisha ujumbe kisanii.

| Ujumbe uliotungwa kawaida | Ujumbe uliotungwa kisanii(jina la kanga) |
|---|---|
| *a)* Nina huzuni mwingi | *Nafuta machozi na bado moyo wazidi kulia* |
| *b)* Situmii uchawi kumpata | *Si mizizi si hirizi bali ni moyo kupenda* |
| *c)* Nilikupenda ukaringa | *Nilikupenda ukajishaua mwenzio yuala maua* |
| *d)* Nikome | *Usinitolee macho kilicho ndani si chako* |
| *e)* Usitegemee bahati ya mwenzako | *Usizime kandili yako kwa taa ya mwenzako* |

Katika mfano *a)* Mshiriki wa mawasiliano anaeleza kusikitishwa kwake na kifo au hali fulani. Badala ya kusema kwa njia ya moja kwa moja, anachagua kanga yenye jina lililoandikwa kisanii. Katika mfano huu mtindo wa kisanii wa kutumia tashihisi kuelezea hisia umetumiwa. Mbali na hayo, majina ya kanga huwa na sifa za kishairi kama mahadhi na midundo ya kuimbika na vina vyenye urari. Haya yanavyodhihirika katika mifano *b) c) d)* na *e)*

## 3.2 Kanga kama Kioo cha Jamii

Kila jamii ina mila, desturi na tamaduni zake. Ni rahisi kutofautisha mtu kutoka eneo moja na mwingine kutoka eneo lingine kwa kutazama mienendo yake, imani yake, lugha yake na mavazi anayotumia. Vivyo hivyo, mwanamke mpwani hutambulika kwa kanga. Kila aendapo hakosi angaa gora moja na mara nyingi maandishi yaliyo kwenye kanga hiyo huwa na ujumbe unaoeleza hisia zake za wakati huo. Kama safari hiyo ni ya kwenda kuomboleza basi bila shaka kanga yake itabeba ujumbe wa

maombolezi na kama ni safari ya furaha vile vile itabeba ujumbe unaoshabihiana na hali hiyo ya furaha.

Kanga kama tanzu zingine za fasihi, huchota dhamira zake kutoka kwa jamii. Majina ya kanga huwasilisha maswala yanayoikumba jamii na yanaweza kutumiwa kuchunguza mifumo ya jamii na kuielewa zaidi.

Majina ya kanga hayatoki katika ombwe tupu. Majina haya hurejelea filosofia, matarajio, imani, shida na maswala mengine ya jamii ya wapwani. Mtumiaji kanga hununua kanga  kwa kuzingatia haja yake ya wakati huo. Mathalan, kama anataka kumshukuru jirani basi kanga hiyo itakuwa na ujumbe wa shukrani na kama anataka kuonya mwenzake kuhusu jambo fulani basi kanga hiyo itakuwa na ujumbe wa kuonya.

Kama katika jamii zingine zote, wapwani hurekebishana, hushindana, huchokozana, husengenyana, huchocheana na huathiriana kwa njia moja au nyingine katika shughuli zao za kila siku. Kanga kama vazi maalum katika jamii hii huchangia katika maingiliano haya na hivyo kulifanya vazi lenye umuhimu mkubwa katika maisha ya wapwani.

Katika mawasiliano kupitia kwa kanga, mtumaji ujumbe huchagua jina la kanga kulingana na haja yake, kisha akachagua mbinu faafu ya kufikisha ujumbe huo kwa mlengwa/walengwa wake. Katika muktadha wa tasnifu hii, mbinu hii ni kanga. Mara tu ujumbe unapomfikia mlengwa, anatarajiwa kuusimbua na kuuchanganua kisha akaamua kujibu au kutojibu.

Mara nyingi maswala yanayozungumziwa katika kanga ni mambo ya kawaida yanayowakumba wanajamii. Kwa mfano, majina ya kwanza kumi tuliyokusanya wakati wa utafiti yaliwasilisha matukio tofauti katika jamii ya wapwani na imani ya wanajamii. Majina haya ni:

*a) Hii ni bahati yangu si makombe si hirizi*

*b) Ulijuaje kama si umbea*

*c) Jirani mwema ni asiye kusengenya*

*d) Usinitolee macho kilicho ndani si chako*

*e) Pendo la dhati huwa ni la kila wakati*

*f) Moyoni nina huzuni waniumiza mwendani*

*g) Mgonjwa hupewa dawa je mdaku hupewa nini?*

*h) Yenu siyaulizi yangu mwayatakiani*

*i) Mungu ni mwingi wa rehema*

j) *Nimepata jibaba lijualo mahaba*

Imani, tabia na desturi za wahusika wa mawasiliano zinaweza kujulikana kwa kuchunguza lugha wanayotumia kuwasilisha ujumbe na jinsi wanavyokabiliana na hali za kijamii. Kwa kutazama majina a) – J) yafuatayo yanaweza kusemwa kuhusu jamii ya wapwani:

- Kuna uganga
- Tabia ya umbea ipo miongoni mwa wapwani
- Majirani wanatarajiwa kuishi vyema bila kusengenyana
- Kuna mapenzi ya ukweli na uongo
- Wapwani wengi wanaamini kuwepo kwa Mungu
- Umri si neno panapo mapenzi

Ili kueleza madai haya, tumetoa ufafanuzi wa makundi mbali mbali kutegemea muktadha wa mawasiliano huku tukijikita katika maingiliano yetu na watafitiwa.

### 3.2.1 Kukomesha Udaku

Kundi hili liliwasilishwa na herufi **A** wakati wa uchanganuzi. Mara nyingi majina ya kukomesha udaku hutumiwa kuwalenga wagomvi na washindani wa msimbaji ujumbe. Sifa kuu ya kundi hili ni kuwa majina huwa yenye kejeli na humwacha aliyelengwa akijiuliza maswali.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* inafasili udaku kama tabia ya kutafuta na kutaka kujua habari za watu; kilimilimi; umbeya. Wengi waliokiri kutumia kanga kukomesha udaku walishinikiza kuwa tabia ya watu kuchunguza maisha ya wenzao si ngeni miongoni mwa wapwani. Tulipodadisi zaidi tulijulishwa kuwa, mara nyingi wanawake ndio wenye tabia hii. Labda hii ndio sababu ya kuchagua kanga kama nyenzo ya kukomesha tabia hii kwani wanawake ndio hushiriki sana mawasiliano kupitia kwa kanga.

Katika hali ambapo mtu amekerwa na tabia ya mwenzake ya kusengenya na kuchunguza maisha ya watu, basi mdaku huyu huweza kukabiliwa kwa kanga yenye ujumbe mahsusi wa kufaa hali hiyo. Kwa mfano, ikiwa jirani fulani ataeneza fununu za kuwakosanisha majirani wenzake, basi anaweza kuvaliwa kanga yenye jina: *Ulijuaje kama si umbea* ama *Mgonjwa hupewa dawa je mdaku hupewa nini?* Mbali na kuaibisha, maneno haya humfanya anayelengwa ajue wazi kuwa alichosema kimejulikana. Katika hali kama hii, mlengwa huona haya na hujaribu kujirekebisha.

50 % ya wanawake tuliokutana nao nyanjani walikuwa na kanga yenye maneno *Usinitolee macho kilicho ndani si chako*. Tulipotaka kujua sababu yao kuinunua, wengi wao walidai kuwa waliinunua kutokana na 'kuvuma' kwake wakati ilipoingia sokoni mara ya kwanza. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa hawangeinunua bila sababu. Tulipodadisi zaidi, tuliambiwa kuwa kanga hii ilikuwa 'kiboko tosha' kwa watu wenye tabia ya kuchunguza maisha ya wenzao na kuyatangaza. Watafitiwa wetu walitueleza kuwa, tabia ya umbea ilikuwa imezidi na kanga yenye ujumbe huo ilipotokea, waliiona kama njia nzuri ya kuwagoa wadaku.

Wanawake wengine waliusimbua ujumbe huu vingine. Walidai kuwa walinunua kanga hii kuwakomesha wanaume wenye tabia ya kuwatongoza wake za watu. Hali hii inaeleza jinsi muktadha unaweza kuathiri ufasiri wa ujumbe. Kundi lililonunua kanga hii ili kuwakomesha wanaume wenye tabia ya kutongoza wake za watu walikumbwa na tatizo mahsusi na wakachagua ujumbe huo ili kuwasilisha hisia zao.

*Mgonjwa hupewa dawa je mdaku hupewa nini?* Hapa tabia ya udaku imefananishwa na ugonjwa. Tofauti iliyopo ni kuwa mgonjwa hutibiwa kwa dawa lakini mdaku hana dawa. Kanga yenye maneno haya hutumiwa kuonyesha kuchukizwa na tabia hii mbaya. Ni rahisi kufikiri kuwa udaku ni tabia inayokubalika miongoni mwa wapwani. Kuwepo kwa kanga hii madukani na manyumbani kulituonyesha kuwa ingawa tabia hii ipo, haikubaliki na inapingwa hata kwa kanga.

### 3.2.2 Mapenzi

Katika kila jamii, mapenzi ni kiungo mojawapo cha maisha ya kila siku. Miongoni mwa wapwani kuwepo kwa mapenzi huonekana bayana katika kanga ambapo majina mengi ya mapenzi yameandikwa kwa vazi hili. Majina haya hutumiwa kukiri mapenzi

kwa mtu fulani na kueleza hisia za kimapenzi. Maneno haya hujenga na kuendeleza uhusiano kwani katika mapenzi lazima kuwe na mawasiliano ya mara kwa mara.

Yafuatayo ni baadhi ya majina kuhusu mapenzi na ufafanuzi wa majina haya. *Penzi la dhati huwa ni la kila wakati:* Wapendanapo wawili, inatarajiwa kuwa watavumiliana wakati wa shida na raha. Aliyekuwa na kanga hii ni mwanamke mmoja wa umri wa miaka thelathini na tisa aliyekuwa ameolewa kwa miaka kumi na nane. Tulipomuuliza sababu yake ya kununua kanga hii, alituelezea kuwa, mumewe alipofutwa kazi, jamaa na marafiki walimhimiza awachane na mumewe eti hangemlisha wala kusomesha wanawe. Badala ya kufanya hivyo mwanamke huyu aliamua kuvumilia hali hiyo. Alianza kuzunguka mitaani akifulia watu na kuwafanyia kazi za nyumbani ili kupata pesa za chakula na mahitaji mengine huku mumewe akitafuta kazi nyingine. Ili kuwakomesha waliokuwa wakimhimiza amuache mumewe, alinunua kanga na kuhakikisha kuwa imesomwa na wote. Mbali na kuonyesha uwajibikaji, ni dhahiri kuwa mama huyu alimpenda mumewe.

Katika mfano huo, imani ya wapwani kuwa mke anafaa kulishwa na kuvishwa na mumewe inadhihirika wazi. Katika jamii hii, si kawaida mke alishe na kuvisha watoto kama mume wake yupo.

*Harufu yako yautuliza moyo wangu* na *Ua langu la moyoni lautuliza moyo wangu* ni majina yanayoweza kutumiwa kukiri mapenzi kwa mchumba au mpenzi.

*Penzi ni jani hunawiri likiwa moyoni*. Hapa mapenzi yamelinganishwa na jani. Kama jani, mapenzi yanahitaji kutunzwa (kutiliwa mbolea na maji) na ili mapenzi

yafanikiwe, lazima yawe ya kweli kutoka moyoni. Nyanya mmoja Mswahili akitupa wasia alituambia, “Ukitaka kufanikisha mapenzi yako, lazima unyenyekee, uwe mwaminifu na usichoke kumfurahisha mpenzi wako. Mkikosana, uombe msamaha na ukubali makosa yako. Mbembeleze mwenzio kwa maneno matamu. Kama utashindwa kusema kwa mdomo, mtandikie ama umvalie kanga yenye maneno matamu kama *Mapenzi yako ni matamu hayaishi hamu”.*

Ni dhahiri kuwa kwa wapwani mapenzi ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa, wawili wapendanapo kuna uwezekano kuwa wawili hawa wataoana na kuanza familia yao. Hivi, jamii itaendelea kukua na kuimarika.

### 3.2.3 Arusi

Wapwani, hasa Waswahili, wanaenzi sana ndoa kama asasi muhimu katika jamii yao. Mume na mke wanaopendana wanapoamua kuziacha familia zao na kuishi pamoja ili kuanza familia yao, huwa ni hatua muhimu kwani hivi, jamii ina hakika ya kuendelezwa. Wakati wa arusi umoja hudhihirika. Jamaa na marafiki huwasaidia maarusi kufanikisha siku yao kwa kushiriki katika sherehe, kupika, kumpamba bibi arusi, kuwashauri maarusi na kuwatakia mema. Katika hatua hii ya maisha ya mpwani, kanga hutumiwa kwa njia nyingi. Utawapata kina mama jikoni wakiwa wamejifunga kanga viunoni ili kuzuia nguo zao zisichafuke. Wakati wa kutoka, bibi arusi hutandikiwa kanga nyingi kama zulia kutoka kwa nyumba hadi kwenye gari linalompeleka msikitini ama kanisani ili asikanyage uchafu (Tazama picha 9 na 10).

Kanga zinazotumiwa wakati wa arusi huwa na majina yenye ujumbe wa kuenzi ndoa, kushauri maarusi kuhusu asasi ya ndoa, kueleza matarajio ya jamii kwa maarusi na

kuwapongeza maarusi. Ujumbe kama *Ndoa huozwa mbinguni* unaonyesha imani ya wahusika. Kwao, ndoa ni swala linalohitaji kuheshimiwa kwani ni takatifu.

Isitoshe, inatarajiwa kuwa jamaa na marafiki watawahimiza maarusi bila kuingilia maisha yao. Msemo *Nyumba ya wawili ni kivuli cha amani*, pia hutumiwa katika arusi ili kuwahimiza maarusi kuishi kwa amani.

Tulivyosema awali, jamii haiwezi kuendelea bila watoto. Wapwani wanaamini kuwa ili kuwe na jamii thabiti, lazima misingi ya kijamii kama ndoa iwe imara ndiposa kukawa na jina la kanga, *Arusi ni nguzo ya jamii.*

Kwa mujibu wa mama Fatuma, mmoja wa wasailiwa wetu, arusi ni sherehe isiyoweka mipaka ya kikabila wala kidini. Ni kawaida kuhudhuria arusi na kupata kuwa asili mia hamsini ya waliokuja hawakualikwa rasmi. Bi Fatuma alituambia, *"..Bora tu usikie kuna arusi wewe toka na uhudhurie. Utakula na kunywa bila kuulizwa. Hapa watu ni wakarimu sana. Jamani ukiwanyima watu arusi, kwako kutaingika?"* Kanga yenye jina *Karibuni wangwana kwa harusi ya mwana* inadhihirisha madai ya mama Fatuma. Kwa wapwani, arusi ni shughuli ya jamii nzima.

Watu wawili wanapooana na kuamua kuishi pamoja, inatarajiwa kuwa watu hawa watapendana daima na kutumikiana kama mke na mume. Kanga yenye ujumbe *Tuheshimu ndoa yetu* ni ushauri mwafaka kwa maarusi ili wadumishe heshima hii ili ndoa yao idumu. Kanga yenye ujumbe huu pia inaweza kutumiwa katika ndoa kuwasilisha malalamishi kwa mke ama mume anayeonekana kutoiheshimu ndoa yao.

### 3.2.4 Mawaidha

Chambilecho wahenga, usiache mbachao kwa mswala upitao. Kitambo, mababu zetu walitumia mafumbo, nyimbo, hadithi na vitendawili kuwashauri wanajamii. Hivi leo hali ni tofauti kwani hali ya maisha imefanya iwe vigumu kwa wazee wetu kuwafikia wajukuu wao. Hii ni kwa sababu watu wengi huishi mijini na huenda mashambani kwa muda mfupi sana na kuifanya iwe vigumu kuwa na maingiliano ya muhimu baina ya vizazi tofauti. Miongoni mwa wapwani kanga inatumiwa kuuziba mwanya huu kwani maneno ya ushauri huandikwa kwenye vazi hili.

Mawaidha kupitia kwa kanga hutolewa kwa mafumbo, kejeli na wakati mwingine kwa njia ya moja kwa moja. Kwa mfano, katika *Ukipenda waridi utavumilia miiba* wasia unatolewa kwa wanajamii kuwa, ili kufanikisha uhusiano wowote ule, lazima wahusika wavumilie kasoro za wenzao.

*Usizime kandili yako kwa taa ya mwenzako* ni jina lingine linalotumiwa kushauri wanajamii wasitegemee bahati ya wenzao na washukuru kwa kile kichache walichopewa badala ya kutamani kitu kikubwa cha wenyewe.

Katika jamii, kuna tabia za watu kutaka kujihusisha na makuu na kukataa kukubali hali zao. Ni kawaida kumsikia mwana akimkataa mama au babake kwa sababu ya ulemavu, uchafu ama umaskini. Kwa watu kama hawa, wasia *Mzazi ni mzazi hata kama hajiwezi* unatolewa. Katika jamii ya wapwani mzazi ni mtu anayeenziwa na aneyestahili kuheshimiwa hata kama ni kiwete, maskini ama mtu mchafu.

Kadri siku zinavyopita ndivyo maswala mapya yanavyozidi kuibuka na hivyo kuzua maswala mapya yanayohitaji kuwasilishwa kwa makundi tofauti. Miongoni mwa maswala haya ni magonjwa, ukosefu wa kazi, mabadiliko ya kisiasa, uraibu wa madawa ya kulevya na unyanyasaji wa wanawake na watoto. Ili kukabiliana na hali hizi mpya, kanga za mawaidha kama *Janjaruka uishi* na *Riziki ni kutafuta sio kurukaruka* zimeibuka. *Janjaruka uishi* ni ujumbe wa kuhimiza vijana wawe waangalifu maishani. Mbali na magonjwa hatari, kuna uwezekano wa kuathiriwa na hali ya maisha na kuwafanya wapate shida maishani. *Riziki ni kutafuta sio kurukaruka* ni jina linalohimiza watu wafanye bidii ili waweze kujimudu kimaisha.

### 3.2.5 Imani

Unapotangamana na watu wa jamii fulani kwa muda mfupi, ni rahisi sana kujua imani, mila na desturi zao kwa kuangalia wanavyoendeleza shughuli zao za kila siku. Katika muda tuliokuwa katika pwani ya Kenya, tuligundua kuwa mbali na kuwa wakarimu, wakaazi wengi wa pwani wameathiriwa pakubwa na dini ya Kiislamu. Kabla ya kuja kwa dini ya Kiislamu karne ya sita, Waswahili hawakuwa wakiabudu chochote. Hata hivyo walisifika kwa kuwa na uwezo wa kuwasiliana na majini. Wengine wao nao waliamini na bado wanaamini katika uganga na uchawi. Hali hii inaonekana wazi katika majina haya ya kanga:

a) *Mungu ni mwingi wa rehema*

b) *Tusafianeni nia Mola atatufungulia njia*

c) *Mungu ndiye mwongozi wa mambo yote*

d) *Hii ni bahati yangu si hirizi si makombe*

e) *Nenda ukaliwe pesa waganga haweshi*

Majina *a,b* na *c* yanaonyesha imani ya wanajamii. Watu hawa wanaamini kuwepo kwa Mungu mwenye rehema na uwezo wa kutenda yote. Majina ya mwisho mawili nayo yanaonyesha kuwa, ingawa kuna wale wanaokiri kumwamini Mungu, kuna wakaazi wa pwani wenye kushiriki ushirikina.

Tulipokuwa nyanjani tulikumbana na vioja vingi vilivyotokana na kuvaliana kanga zenye ujumbe tofauti tofauti. Mfano tusioweza kusahau ni wa majirani wawili waliokuwa wakiishi katika nyumba ya Kiswahili kwenye mtaa wa Majengo. Tulisimuliwa kuwa mmoja wao (tutamwita Riziki katika tasnifu hii kwa sababu za kumficha) alienda kwa mganga alipoona kuwa mwanawe alikuwa amepooza upande mmoja na madaktari wote walikuwa hawampi maelezo ya kuridhisha. Alipomtembelea mganga, alielezewa kuwa jirani yake mwembamba mrefu mwenye mazoea ya kukaa mlangoni ndiye alikuwa "amemchezea" mwanawe.

Riziki aliporudi kwake alitangazia kila mtu kuwa mchawi wake alikuwa ni mamake Ali na akaanza kuvaa kanga zenye kumchokoza mwanamke huyu. Angeonekana na kanga zenye majina kama: *Uhasidi wenu haunivunji, Hasidi nichukie roho yangu niwachie, Hasidi hana sababu,* na *Ujirani naupenda lakini tabia zimenishinda.* Kwa kuwa majirani wote walijua chanzo cha uhasama huo, walijua kuwa aliyekuwa akilengwa na kanga hizo alikuwa mamake Ali. Mamake Ali alikerwa sana na madai ya jirani yake kwani alijua kuwa ingawa yeye ni mrefu na alikuwa na mazoea ya kukaa mlangoni, hakuhusiana na ugonjwa wa mtoto wa jirani yake. Alipoona kuwa uchokozi kwa kanga umezidi, aliamua kutumia 'fimbo' hiyohiyo kwa kununua kanga iliyosema: *Nenda ukaliwe pesa waganga haweshi* na nyingine ya kusema *Pekepeke za jirani hazinitoi ndani*. Ili kumkera jirani yake, alihakikisha kuwa jirani huyu amezisoma. Alifanya hivi kwa kuzianika kanga zake hadharani jina likionekana na

alipitapita mbele yake kila wakati. Ingawa hatukupata fursa ya kuthibitisha kama kweli uganga upo, kuwepo kwa majina ya kanga yenye kuzungumzia maswala haya kunaonyesha kuwa wapwani wanaamina kwamba uchawi upo na unaweza kudhuru mlengwa.

### 3.2.6 Kumuenzi Mama

*Titi la mama litamu, hata likiwa la mbwa*

*Titi le mama litamu, jingine halishi hamu*[9]

Hii ni mishororo miwili kutoka kwa shairi la mwandishi mashuhuri Shaaban Robert, Kiswahili. Shaaban anathibitisha umuhimu wa mzazi huyu wa kike katika jamii.

Katika nchi za kimagharibi, mama huenziwa kwa kadi na nguo zenye ujumbe mahsusi wa kumsifu, kumshukuru na kumuenzi. Miongoni mwa wapwani, kanga hutumiwa kueneza ujumbe wa kutambua umuhimu wa mama. Kanga zenye ujumbe huu hutolewa kama zawadi kwa mama na wanawe, marafiki au hata majirani. Tulipokuwa tukifanya utafiti wetu, tuligundua kuwa, mama ni yeyote aliye na umri unaotosha kumfanya awe mama mtu na aliyeathiri maisha ya mhusika kwa njia moja au nyingine. Anaweza kuwa rafiki ya mamako, jirani yako, kungwi au mlezi wako. Kundi lifuatalo linawakilisha ujumbe unaomuenzi mama.

1. *Mama mlezi kukusahau siwezi*
2. *Ni wewe tu mama*
3. *Penzi la mama litamu haliishi hamu*
4. *Mama ni mama asiyejua mama hana maana*
5. *Nani kama mama*

[9] Shairi lililo kwenye Kusanyiko la mashairi yaliyokusanywa na Ali A Jahadhmy (1975) East African educational Publishers, Nairobi Kenya

Misemo *1), 2), 3), 4)* na *5)* inatumiwa kutambua umuhimu wa mzazi wa kike katika jamii. Aidha, misemo hii inaonyesha jinsi mama anavyoenziwa. Katika mfano wa kwanza, mtoto anaonekana akimhakikishia mamake kuwa daima hatamsahau. Tulifasiri ujumbe huu kumaanisha kuwa mtoto huyu angefanya kila jambo kuhakikisha kuwa mamake anaishi vizuri.

Majina *Ni wewe tu mama* na *Nani kama mama* yanaonyesha kuwa hakuna anayeweza kuchukua nafasi ya mama ilhali jina *Penzi la mama litamu haliishi hamu* linaonyesha kuwa hata mtu awe wa umri gani, penzi la mama ni la muhimu na daima mama hawachi kumpenda mwanawe hata kama ni mzee vipi.

Katika jamii, ni kawaida kupata watu wanaodharau na kutotambua umuhimu wa mama zao. Jina *Mama ni mama asiyejua mama hana maana* linaweza kutumiwa kumkumbusha mtu kama huyu kuwa hakuna mtu ama kitu kinachoweza kufananishwa na mama kwa hivyo hana budi kumheshimu mamake.

### 3.2.7 Msiba /maombolezi

Ama kwa kweli, furaha na msiba ndicho kidunia. Vivyo hivyo, kanga ina jukumu la kuwasilisha hali zote mbili na kukawa na kanga zenye maneno kama:

1. *Pole kwa yaliyokufika*
2. *Mti mkuu umeanguka ndege wa mashakani*
3. *Nafuta machozi na bado moyo wazidi kulia*
4. *Mpendwa wetu safiri salama*
5. *Furaha na msiba ndicho kidunia*

Matanga katika jamii ya wapwani ni shughuli ya kila mtu. Majirani, jamaa na marafiki hushirikiana katika kuwatuliza waliofiwa na kupanga mazishi. Ni kawaida kuwa na mikutano mahali pa maombolezi. Katika mikutano hii waombolezaji huchanga pesa na kuwa pamoja na waliofiwa. Umoja huu ulidhihirika katika matanga yote tuliyohudhuria.

Kanga za maombolezi zilikua chache mno.Tulifasiri hali hii kumaanisha kuwa kanga za maombolezo huwekwa kama kumbukumbu baada ya sherehe ya mazishi. Inawezekana pia kuwa si picha nzuri kuonekana na kanga ya maombolezo kwa siku ya kawaida. Kutumia kanga hii kunaweza kufasiriwa kama ‘kuita’ kifo.

### 3.2.8 Kauli

Kundi hili linajumuisha matamshi au usemi unaoeleza hisia na maoni ya mtu au watu kuhusu hali fulani. Katika pilkapilka za maisha, binadamu hujipata katika hali ya kutaka kujieleza hasa kuhusu mazingira yake na matukio ya kila siku. Kundi hili lina mada tofauti na hakuna mpaka dhahiri. Itaonekana kuwa maneno mengine katika kundi hili yanaweza kuwekwa katika makundi mengine na kusiwe na shida yoyote. Kauli hizi hutolewa na jirani kwa jirani, rafiki kwa mwenzake, adui kwa hasidi wake na wakati mwingine huwa ujumbe haukusidiwi kumlenga mtu maalum. Yaani, yeyote atakayeusoma ausome na kama utamfaa autumie. Usipomfaa aupuuze. Yafuatayo ni maneno yenye kuwasilisha kauli:

1. *Jirani mwema ni asiye kusengenya*
2. *Kuregarega sio kufa*
3. *Mzazi ni mzazi hata kama hajiwezi*

4. *Zawadi ni chochote kupokea usichoke*
5. *Neno jema halikosi kujibiwa*

### 3.2.9 Usemi wa Jumla

Kundi hili na lile la awali linakaribiana sana. Hata hivyo tuliamua kuyatenga kwa kuwa tofauti na kundi la kauli, kundi hili la usemi wa jumla linajumuisha maneno ya kutia moyo na kushauri na mara nyingi huwa katika mafumbo na huhitaji kufafanuliwa kwa undani. Hii sio kusema kuwa maneno katika kundi hili hayawezi kuwa na ujumbe wazi bali ni kusema kuwa mara nyingi ujumbe huwa fiche na wakati mwingine usemi mmoja unaweza kubeba maana zaidi ya moja. Kundi lifuatalo linawakilisha usemi wa jumla.

1. *Mapenzi hayana subira waridhianapo*
2. *Zawadi ni chochote kupokea usichoke*
3. *Subira nyumba ya neema*
4. *Neno jema halikosi kujibiwa*
5. *Sitasahau hisani uliyonitendea*

## 3.3 Kanga kama Makala ya Kusomeka

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* inaeleza vazi kama nguo, ngozi n.k. kinachotumiwa kwa kuvaa mwilini. Kanga ni vazi la kipekee kwani mbali na kutimiza haja ya mavazi mengine ambayo ni kusitiri uchi, vazi hili lina maandishi ambayo kwayo ujumbe hupitishwa kutoka kwa chanzo hadi kwa mpokezi/wapokezi wa ujumbe huo.

Beck (2001) anadai kuwa ni vigumu kusoma jina la kanga eti kwa sababu huwa imefungwa kiunoni au imetandwa mabegani na kuficha sehemu ya jina. Anazidi

kueleza kuwa, ni ujeuri kumtazama mtu hasa mwanamke kwa muda mrefu kwa hivyo kusoma jina la kanga ni kama ujeuri. Tulipokuwa nyanjani, wanawake walionekana kusoma kanga za wenzao bila shida yoyote. Isitoshe, hata bila kusoma jina la kanga fulani, uraibu wa kanga walionao wanawake wa pwani ya Kenya umefanya wengi wao kujua kila kanga inayoingia kwa jina na umaridadi wake. Ni muhimu kutaja hapa kuwa, kila mara kanga mpya inapoingia sokoni, gari aina ya 'Pick-up' huzunguka mitaani huku majina ya kanga hizi mpya yakitangazwa kupitia kipaza sauti. Mbali na kutangaza, kanga hizi huwa zimetundikwa kwenye vyuma vya gari hilo. Hali hii huchangia tabia ya wanawake wengi kujua majina ya kanga kwa kuyahusisha na umaridadi wake bila hata kusoma.

Ni kawaida kupata wanawake wasiojua kusoma wakishiriki katika mawasiliano kupitia kwa kanga. Mara nyingi, wao huenda dukani na kuulizia kanga ya kufaa muktadha fulani. La ajabu ni kuwa hata wao hujitahidi kuvaa kanga ya kufaa nyakati mahsusi. Tulipomuuliza Mama Khadija ni vipi aliweza kujimudu katika kuwasiliana kupitia kwa kanga bila kujua kusoma, alitueleza kuwa, kutokana na mazoea ya muda mrefu ya kutumia kanga, anaweza kutambua na kukariri jina la kanga kwa kuiona tu.
Ingawa umaridadi na rangi ya kanga ni vipengele muhimu vya kanga, maoni ya watafitiwa katika miktadha mbalimbali ya uchunguzi wetu yalionyesha kuwa, kanga haisifiki kwa ajili ya umaridadi wake wala rangi yake tu bali kwa maneno yake. Kati ya wanawake mia moja tuliohoji, ni asilimia nane (8%) tu waliokiri kuzingatia rangi na umaridadi wa kanga zaidi ya jina/ maneno. Ifuatayo ni mifano kumi ya majibu tuliyopata kwa swali: Je, unaponunua kanga huwa unazingatia nini?

1) Ninaponunua kanga la muhimu ni jina. Hapa kwetu waweza kununua kanga eti kwa kufurahia maua ama rangi kisha ujute miaka yote. Ni rahisi sana kusomwa visivyo.
2) Kuna wengine ambao huvutiwa na rangi, wengine wakavutiwa na ile michoro na wengine wakavutiwa na maandishi kimafumbo. Mimi binafsi hupendezwa na mafumbo kwa hivyo hununua kanga zangu si kwa rangi bali kwa mafumbo. Ingawa napenda rangi ya bluu nina kanga za rangi tofauti tofauti na kila kanga ina uzuri wake kutegemea jina lake.
3) Inategemea. Ikiwa nimetoka na nia maalum ya kunua kanga ya maneno fulani, basi nitatazama maneno kabla ya kuzingatia rangi. Wakati mwingine nikivutiwa na kanga kwa mbali tuseme kwa sababu ya umaridadi au rangi yake, naweza kuinunua mradi tu iwe na ujumbe ambao hautazua aibu. Juzi jirani yangu alinunua kanga bila kuisoma na kuitafakari. Alipojifunga kila mtu aliyemuona alimdhani kapumbaa. Hii ni kwa sababu kanga yenyewe ilikuwa na maneno, *Inua guu gongo laja.* Kwa hivyo hata nikipendezwa vipi na umaridadi lazima nitafakari ujumbe nisije nikajipaka tope.
4) Rangi na umaridadi ndio hunivutia kwanza. Hata hivyo, kanga si kanga bila jina. Kama ni rangi na umaridadi tu si basi ninunue kisutu[10] au kikoi!
5) Huwa naenda na wakati. Wakati mwingine mimi hununua kanga bila kujali jina ili nisikie majirani watasema nini. Labda hata sina nia ya kumchokoza mtu lakini nikiona kanga yangu imemchoma jirani naye labda anijibu na yake basi huwa nasikia raha sana. Tuseme napenda uchokozi hasa wa kutumia kanga. Kuna wanawake wanaojishuku kiasi cha kujipa 'presha' bure!

[10] Vazi kama kanga lisilo na maandishi. Huwa halina michoro maarufu katika kanga (maembe, korosho na mananasi) Inaaminika kuwa vazi hili hutumiwa na wachawi kupunga pepo.

*6)* Lazima nifurahishwe na rangi  na umaridadi kabla sijasoma jina. Ni baada ya kufurahishwa na rangi ndipo swala la jina hunijia.

7) Yote – rangi, jina na umaridadi. Nikinunua kanga , lazima iwe na rangi ya kuvutia na jina lake linifae. Yaani ujumbe huo uwe na maana maishani mwangu. Kwa mfano siwezi kununua kanga ya jina *Simtaki bwanako wangu ni mtamu* hata kama ina umaridadi wa aina gani kama sina vita na bibi ya mtu. Labda hata sina mchumba. Nikivaa kanga kama hii bila shaka nitadhaniwa kuwa 'mwizi' wa mabwana. Aidha, hata jina la  kanga linipendeze vipi, siwezi kununua kanga hiyo kama rangi yake haitanipendeza.

8) Rangi na umaridadi. Kanga zote madukani ni nzuri. Mafumbo yake hayaishi utamu na kama fumbo hilo halitakufaa kuwasilisha ujumbe leo, kesho utalihitaji. Mimi hununua kanga angaa kila mwezi . Kwa kuwa kanga hizo huwa za ujumbe sawa na rangi tofauti, mimi huchagua rangi ya kunipendeza.

9) Maandishi. Usipokuwa makini na maandishi, unaweza kununua kanga itakayokuaibisha.

10) Kanga ni vazi la kipekee kwani mbali na kuwa vazi, lina ujumbe. Kwangu, ujumbe huu ni muhimu zaidi ya rangi na umaridadi.  Si vizuri uvae kanga ya rangi nzuri lakini inabeba matusi. Afadhali uwe na kanga yenye rangi isiyopendeza lakini iwe inawakilisha fikra na imani yako.

Mifano hii inadhihirisha kuwa, kanga ni makala ya kusomeka na kuchangia mawasiliano; hasa tunapozingatia kuwa hata wale waliodai kununua kanga kwa kuzingatia rangi na umaridadi walikiri kutambua uzito/umuhimu wa maneno na mawasiliano ya kutokana na maneno haya. Mathalan ingawa mtafitiwa  nambari 8) anasema yeye huchagua kanga kutegemea rangi na umaridadi, anaashiria kuwa hata

yeye anatambua kuwa kanga ni ujumbe anaposema ".... mafumbo yake hayaishi utamu na kama fumbo hilo halitakufaa katika kuwasilisha ujumbe leo, kesho utalihitaji".

Anavyosema Brown (1995) ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Desturi ya kutumia kanga kama ishara ya kumkaribisha mgeni imekita mizizi na ni jambo la kawaida miongoni mwa Wapwani. Inatarajiwa kuwa mara tu mgeni wa kike anapoingia mwenyeji wake wa kike anafaa kumpa kanga ajifunge hata kabla ya kumpa maji wala chai. Hii ni ishara ya kuonyesha ukarimu na kumstarehesha mgeni. Hata bila kutumia maneno, mwenyeji anapompokea mgeni kwa kanga, mgeni huyu hujua kuwa amekubalika katika nyumba hiyo. Katika hali kama hii ni muhimu mwenyeji aisome kanga kabla ya kumpa mgeni wake. Itakuwa jambo la aibu kama mwenyeji huyo atampa mgeni kanga ya matusi kama ile yenye maneno:*Uhasidi wenu haunivunji* bila kukusudia.

### 3.4 Lugha katika Mawasiliano kupitia kwa Kanga

Wittgenstein (1989) anadai kuwa, mawazo yanaweza kuwasilishwa kwa ishara dhahiri (visible signs), kwa kuandika, kuzungumza au kuashiria tu. Katika mawasiliano kupitia kwa kanga, msimbaji ujumbe huwa na wazo la kuwasilisha, akalifikiria kisha akachagua maneno ya kuwasilishia ujumbe wake kupitia kwa kanga.

Huku Harris (1993) akisisitiza umuhimu wa nia/haja ya kusimba ujumbe katika mawasiliano, Poyatos (1983) anadai kuwa lugha ndio uti wa mgongo wa mawasiliano. Madai haya ya Poyatos yanafanana na yale ya Wittgenstein (ibid) anayefananisha lugha na sanduku la vifaa vya kazi "toolbox" huku akifananisha maneno na vifaa vya kazi "tools". Mwanafalsafa huyu anaamini kuwa, maana ya neno

imo katika matumizi yake kimuktadha na kuwa lugha haifuati mfumo maalum bali hubadilika kadri maisha yanavyobadilika. Madai haya ya Wittgenstein yanaelekea kukubaliana na nadharia inayouongoza utafiti huu kwamba, maana ya lugha imo katika matumizi yake kimuktadha.

Mtumiaji vifaa (fundi) ndiye huamua kifaa cha kuchukua kutoka kwa sanduku na kufanyia kazi fulani. Vivyo hivyo, ni mtumiaji maneno ndiye huchagua maneno ya kutumia kuwasilisha ujumbe anaokusudia. Hali hii ni dhahiri hata katika mawasiliano kupitia kwa kanga ambapo mtumaji ujumbe ndiye huchagua maneno ya kutumia ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano, wakati wa msiba, wanawake huvaa sare za kanga zenye maneno ya kuomboleza. Tulipokuwa nyanjani, tulihudhuria matanga mara tatu na sare zilizovaliwa zilikuwa na maneno:

- *Mti mkuu umeanguka ndege wa mashakani*
- *Mpendwa wetu safiri salama* na
- *Nafuta machozi na moyo wazidi kulia*

Katika mfano wa kwanza, mti mkuu unawakilisha mtu anayetegemewa. Hapa, aliyeaga alikuwa baba ya watoto wanne wenye umri mdogo mno. Mama ya watoto hawa alikuwa ashaaga dunia miaka miwili iliyopita kwa hivyo watoto hawa sasa walikuwa wamebaki mayatima. Watoto hawa ndio wanafananishwa na ndege kwani mti uangukapo, bila shaka ndege ambao hutegemea mti huo kwa makaazi yao, ndio huumia.

Mfano wa pili unafananisha kifo na safari. Ujumbe huu unaweza kutumiwa wakati wa safari ya kawaida ambapo labda mtu anasafiri kwenda ng’ambo ama mbali na pia

unaweza kutumiwa katika maombolezi ambapo kifo kinafananishwa na safari. Hii ni kuonyesha kuwa maneno hupata maana kutegemea muktadha wa matumizi.

Kwa kawaida moyo haulii lakini ujumbe wa tatu umetungwa kwa kutumia tashihisi kueleza uchungu wa kumpoteza mpendwa. Ujumbe huu unaeleweka kwani kanga yenye maneno haya ikivaliwa matangani, bila shaka maana itakayofasiriwa ni kwamba aliyeivaa kanga hiyo anashirikiana na waliofiwa katika kusikitishwa na kifo kilichotokea. Moyo kuzidi kulia kunasisitiza dhana ya uchungu anaohisi mhusika kwa kumpoteza mwenda zake.

Ujumbe pia huweza kuwasilishwa kwa kutumia kejeli. Kwa mfano jina *Muzidi kupalilia sisi yetu twajilia* linabeba ujumbe uliojaa bezo na stihizai huku likifumba ujumbe. Mzushi wa ujumbe huu anawaambia wagomvi wake kuwa matendo yao hayamdhuru wala hayampunguzii chochote. Wao wenye 'kumtafuta' watazidi kujiumiza na kujichosha bure.

*Uhasidi wenu haunivunji* ni msemo unaoweza kutumiwa na mtu kumlenga mwenzake au wenzake wasiomtakia mazuri. Mtoaji ujumbe huu anawakejeli mahasidi wake kwa kuwaambia kuwa chuki zao hazimdhuru.

Katika maisha ya mwanadamu ni kawaida kupinga na kupingwa. Huenda kukatokea hali ambapo watu wawili wanapendana na jamaa ama marafiki wanayapinga mapenzi yao kwa kusema kila aina ya uongo ili kuwatenganisha. Ikiwa mwanamke anayehusika anampenda mchumba wake kwa dhati, maneno *Mtasema mtachoka simuachi haniachi* yatatumiwa kueleza hisia zake. Ujumbe huu pia unaweza

kuwalenga watu wanaoeneza fununu za uongo kuhusu uhusiano wa watu wawili wapendanao na nia ya kuvunja uhusiano huo.

Visa vya majirani kugombana, kusengenyana na hata kupigana ni jambo la kawaida. Ikiwa mtu ni mwepesi wa roho, si rahisi avumilie kusikia jina lake likipakwa tope bila yeye kutoka kimasomaso kujitetea na kulisafisha jina lake. Hata hivyo maneno *Peke peke za jirani hazinitoi ndani* yanaonyesha kuwa mtu anaweza kupuuza kinachosemwa na aishi raha mstarehe. Maneno haya ya kupuuza yanayosemwa hutumiwa kuwaonyesha mahasidi kuwa kusemasema kwao ni kazi bure na maneno yao hayana nguvu za kudhuru.

Msemo *Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa* una uzito mkubwa kwani mbali na kutumia kejeli, msemo huu unadhalilisha majirani wanaolengwa kiasi cha kufanya mtunzi wa ujumbe huu kupenda paka zaidi yao.

Mara nyingi, lugha inayotumiwa katika kanga huwa ya kishairi na mtindo unaotumiwa kuwasilisha ujumbe unafanana sana na ushairi wa Kiswahili. Haya ni kwa mujibu wa Beck (2001). Tumepiga kistari chini ya vina vyenye urari katika majina tuliyokusanya ili kuonyesha kukubaliana kwetu na madai ya Beck. Kama katika ushairi, mada zinazozungumziwa katika kanga hujumuisha maswala yanayoikumba jamii kama ujirani, uke wenza, mapenzi, maswala ya kiuchumi, maswala ya kisiasa, magonjwa na kifo.

### 3.4.1 Uwasilishaji Ujumbe kwa Njia ya moja kwa moja

Yule (1985) anaeleza kuwa uamali hujishughulisha na jinsi lugha inavyotumiwa katika mawasiliano. Spencer-Oatey (1993) naye anasema uamali hujishughulisha na lugha kihusishi. Spencer-Oatey anashereheshea kwa kudai kwamba lugha hupata maana kutegemea muktadha, wahusika na utamaduni wa washiriki wa mawasiliano. Katika mawasiliano kupitia kwa kanga kinachozingatiwa sana ni utambuzi hasa baina ya mtunzi wa ujumbe na mpokeaji. Uamali hujihusisha zaidi na maana iliyodhamiriwa na mtunzi wa ujumbe na hudhihirika kwa kuhusishwa na muktadha maalum kimatumizi.

Uwasilishaji wa ujumbe kwa njia ya moja kwa moja hutumia maneno ya kawaida kupitisha ujumbe ulio wazi bila kuficha chochote. Kwa mfano, ikiwa mtu anataka kumshukuru mamake kwa kazi nzuri ya ulezi, na amnunulie kanga yenye ujumbe; *Mama mlezi kukusahau siwezi* ama *Titi la mama litamu haliishi hamu*, maana itasimbuliwa kwa njia ya moja kwa moja bila kutafuta maana fiche.

### 3.4.2 Ufumbaji katika Kanga

Beck (2005) anadai kuwa maswala yasiyoruhusiwa kuzungumzwa waziwazi miongoni mwa Waswahili huwasilishwa kutumia mafumbo yanayoandikwa katika sehemu ya chini ya kanga. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* inafafanua fumbo kama maneno yasiyojulisha maana wazi wazi ; kitu chochote kilichofichwa ili kisijulikane kwa urahisi, siri, methali, kitendawili. Katika muktadha huu, fumbo limechukuliwa kama jina lolote la kanga lisilopitisha ujumbe kwa njia ya moja kwa moja.

Danesi (2002) anaeleza kuwa, ujumbe huweza kufafanuliwa kwa njia ya moja kwa moja au kwa kutafuta maana fiche. Hali hii pia hujitokeza katika mawasiliano kupitia kwa kanga ambapo maneno yanayotumiwa huweza kuwasilisha ujumbe kwa njia ya moja kwa moja ama kwa kutumia mafumbo. Kwa mfano, mwanamke au mwanamme anayeshuku kuwa mpenzi wake ana uhusiano wa kimapenzi na mtu mwingine anaweza kutumia kanga yenye maneno *Utamaliza bucha nyama ni ile ile.* Hapa bucha inawakilisha wanawake au wanaume ilhali nyama ni huduma zinazotolewa na wanawake ama wanaume hawa. Kanga hii pia inaweza kuwasilisha ujumbe wa moja kwa moja kwa wateja wanaopenda kubadilisha badilisha bucha wanamonunua nyama. Hata hivyo, kanga hii ilionekana kutumiwa zaidi kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe wa kukataza wanaume na wanawake kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja.

Baadhi ya maneno yapatikanayo kwenye kanga hubeba ujumbe fiche. Mtu akiyasoma juujuu bila kutafakari zaidi huenda asielewe kilichokusudiwa na aliyeusimba ujumbe. Kwa hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa si kila wakati ambapo maana ni wazi na ya moja kwa moja. Ni sharti mhusika ajiulize ni kwa nini akavaliwa kanga hiyo, katika hali gani na ni yapi yalitangulia. Akielewa hali hii, bila shaka atasimbua ujumbe na apate maana iliyokusudiwa. Katika kutangamana na watafitiwa, tulikumbana na hali hizi halisi.

1. Mama mmoja alimnunulia mke mwenzake kanga yenye maneno: *Wimbo mbaya haumbembelezi mtoto.* Kwa mujibu wa mama huyu, mke mwenzake alikuwa akimchokoza kwa maneno tangu mume wao alipohamia kwake. Ili kumtia mke mwenzake adabu, alinunua kanga ya kumkejeli kwa kutomtunza vyema mume wao. Kwa maoni yake, mume hufugwa kwa chakula kitamu,

mapenzi na maongezi matamu kama mtoto. Ndiposa akamnunulia kanga yenye ujumbe huo.

Mtu wa kawaida asiye katika hali ya uke wenza atauelewa ujumbe tofauti na yule aliye katika uke wenza. Isitoshe, hata yule aliye katika uke wenza huenda asiuelewe ujumbe kama hatatumia jicho la ndani kuusimbua ujumbe huo. Hapa swala la muktadha katika kufasiri ujumbe linajitokeza. Ujumbe huo huo, ungeweza kutumiwa kama ushauri kwa mama aliyepata mtoto kama muktadha ungebadilika na wahusika pia wabadilike.

2. Hali nyingine kama hii ilijitokeza pale mtafitiwa mmoja alipotuonyesha kanga aliyonunuliwa na mamake. Kanga hii ilikuwa na maneno: *Usizime kandili yako kwa taa ya mwenzako*. Binti huyu alipomaliza masomo ya shule ya upili alienda kumsaidia kakake na wifi yake waliokuwa na watoto wadogo. Kwa kuwa maisha ya kwao yalikuwa magumu mno, alikataa kata kata kurudi kwao ili ajiunge na chuo cha kiufundi hapo kijijini. Mamake alipochoshwa na kumbembeleza, alimnunulia kanga hiyo na kumwambia atafakari kwa ndani maana ya ujumbe huo. Ingawa mwana aliupuuza wakati huo, alipata cha mtemakuni pale kakake na familia yake walipoamua kwenda ulaya. Kwa kuwa nauli haikuwa ya kutosha, ilimbidi arudi mashambani kwa mamake. Kisa hiki kilimfunza mengi na hadi leo ameweka kanga aliyonunuliwa na mamake. “Kandili yako” ina maana ya kile kidogo ulicho nacho ilhali “taa ya mwenzako” inamaanisha kitu kikubwa ambacho si chako.

3. *Ukipenda waridi utavumilia miiba*. Maneno haya yalikuwa katika sare ya harusi. Kanga yenyewe ilikuwa na michoro ya kuvutia ya maua ya waridi. Tulipotaka kujua kwa nini walichagua maneno haya, tuliambiwa kuwa, kanga hii ilikuwa ya kutoa ushauri kwa maarusi. Wawili hawa walitakiwa kuvumiliana kwa vyovyote vile. Waridi ni ua la kuvutia lakini lina miiba. Kwa hivyo kama waridi, kila mtu ana ubaya wake/ kasoro yake (miiba) na ili kuishi kwa amani, watu sharti wavumiliane.

Mifano hiyo mitatu inadhihirisha kuwa, ni muhimu kutumia jicho la ndani wakati wa kufasiri ujumbe. Tusipokuwa makini, huenda tukasimbua ujumbe visivyo na hivyo kukatiza mawasiliano.

## 3.5 Hitimisho

Sura hii imechanganua mawasiliano kupitia kwa kanga kwa kujikita katika kueleza mchakato wa kupitisha ujumbe kutoka kwa chanzo hadi kwa mpokezi huku ikitoa maelezo kuhusu dhana tofauti zinazohusu mawasiliano. Miongoni mwa nadharia zilizotuongoza ni nadharia ya simiotiki inayosema kuwa, kila ishara huwasilisha ujumbe fulani.

Aidha, tumeainisha na kujadili maswala tofauti yanayoikumba jamii kwa kuchanganua majina tuliyokusanya kutegemea wahusika wa mawasiliano haya, mandhari ambamo wahusika wamo, nia ya msimbaji ujumbe, usuli wa kimawasiliano na kimtagusano maishani mwa wahusika wa mawasiliano na mila na desturi zinazotawala mawasiliano kupitia kwa kanga.

Sura ya nne inatilia maanani umuhimu wa muktadha katika mawasiliano unavyodhihirika katika nadharia ya uamali. Ujumbe huweza kusimbuliwa kwa njia tofauti kutegemea mandhari, mila na desturi za wahusika na matukio ya wakati huo.

# SURA YA NNE

## *UAMALI WA KIJAMII KATIKA DISKOSI ZA KANGA*

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inazama katika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya mawasiliano ya kutokana na maandishi katika kanga na jamii zinamotumika kanga hizi. Katika kufafanua uamali, Leech (1983) anadai kuwa huu ni uchunguzi wa maana unaohusisha usemi na hali mahsusi. Madai haya yanatuongoza katika kufanya uchunguzi wa mawasiliano kupitia kwa kanga kwa kuhusisha mawasiliano haya na jamii yanamotumika.

### 4.1 Dhana ya Muktadha

Muktadha unaweza kufafanuliwa kama mazingira yanayomzunguka mtu katika hali fulani. Hapa muktadha wa kimawasiliano ni mazingira ambamo washiriki wa mawasiliano huwa. Mazingira haya hujumuisha mahali na hali mahsusi. Ufahamu wa mazingira mnamotukia mawasiliano ni muhimu mno. Mara nyingi mawasiliano huathiriwa na mifumo ya kijamii, jinsi watu wanavyohusiana na kaida zinazoongoza jamii husika. Katika kufafanua muktadha katika msingi wa mawasiliano kupitia kwa kanga, tumeainisha aina tatu za miktadha inayoathiri mawasiliano haya:

- Muktadha Kijamii
- Muktadha Kisaikolojia
- Muktadha Kifalsafa

Baadhi ya maswali tunayojibu ni:

1. Je, wanaowasiliana kwa kutumia kanga wamo katika mazingira yapi?
2. Ni nini usuli wa kimawasiliano na kimtagusano maishani mwa washiriki wa mawasiliano?

3. Nini mahusiano baina ya washiriki wa mawasiliano haya?

### 4.1.1 Muktadha Kijamii

Uchunguzi shirikishi ulituwezesha kuelewa jamii ya wapwani hasa maisha na maingiliano yao ya kila siku. Maswala makuu tuliogundua ni kuwa, watu wote wanatarajiwa kuheshimiana na salamu ni sehemu muhimu ya matukio ya kila siku; kila unapokutana na mtu unatarajiwa kumuamkua. Kama ni mkubwa wako sharti umpe shikamoo. Aidha, watu wote wanatarajiwa kuwa wakarimu. Tulivyotaja awali, nyumba nyingi katika pwani ya Kenya zimejengwa kwa mtindo wa Kiswahili na majirani wote wanatarajiwa kuishi kama jamaa na marafiki.

Mazingira haya huzua hali tofauti. Kwa mfano, ni wazi kuwa watu watakosana, wengine wataoneana wivu, kubishana kutaanza na masengenyo huenda yakazuka. Kwa jinsi hii, mada za kanga huchukua mwelekeo wa kijamii ambapo maswala yanayowakumba wanajamii ndio huwasilishwa. Haya yamethibitishwa katika sura ya tatu ambapo majina ya kanga yameainishwa kimada. Kuna majina ya mapenzi, kusutana, kusherehekea, kuomboleza, kushauriana na mengine ya kuonyesha imani ya washiriki wa mawasiliano kupitia kwa kanga.

### 4.1.2 Muktadha Kisaikolojia

Mara nyingi wahusika wa mawasiliano husukumwa na nafsi zao kutekeleza haja za kimawasiliano. Pengine mwana amemkosea mama na hana njia nyingine yoyote ya kuomba msamaha. Ikiwa atamnunulia mamake kanga yenye ujumbe: *Radhi ya mama ni stara kwa mwana* au *Mama ni mama asiyejua mama hana maana*, bila shaka mamake ataelewa haja ya mwanawe kuomba radhi na ataonyesha ishara ya

kumsamehe kama kumuita na kumwambia kuwa hakuna neno amemsamehe ama amketishe na wazungumze kama mama na mwanawe.

Fauka ya hayo, katika mawasiliano kupitia kwa kanga ufasiri wa maana hutegemea vipengele vingi. Miongoni mwavyo ni kuelewa hali zilizotangulia mawasiliano ama hali zilizosababisha mawasiliano hayo. Vile vile, ni kuelewa sababu za mtunzi wa ujumbe kuchagua njia aliyotumia kufikisha ujumbe wake badala ya kuchagua njia nyingine.

Kwa mfano wakati wa maombolezi kanga zenye ujumbe kama *mti mkuu umeanguka ndege wa mashakani* na *mpendwa wetu safiri salama* hutumiwa. Jumbe kama hizi hutumiwa kufariji waliofiwa na kuonyesha umoja wakati wa maombolezi. Mfano wa kwanza unaonyesha hali ya kutojiweza kwa wale waliofiwa. Labda ni baba au mama aliyetegemewa na familia yake kwa hali na mali. Mtu asiyeelewa hali hiyo huenda asielewe maana ya kanga hiyo. Katika mfano wa pili, imani ya wanaoshiriki mawasiliano inajitokeza pale ambapo maombolezi yanaambatana na imani kuwa, kifo ni safari. Ikiwa mpita-njia ataona wanawake wamejifunga kanga yenye jina hili huenda akadhani kuwa kuna sherehe ya kuaga mtu anayesafiri.

### 4.1.3 Muktadha Kifalsafa

Kama jamii zingine zote, jamii ya wapwani ina mielekeo yake, matarajio na falsafa zake. Hali hii inadhihirika wazi katika mawasiliano kupitia kwa kanga ambapo majina mengi hueleza maingiliano na maisha ya wapwani. Mathalan jina *Pendo la dhati ni la kila wakati* linaonyesha imani na matarajio ya wapwani kuhusu mapenzi. Kwao, pendo la kweli linafaa listahimili shida; wapendanao wavumiliane wakati wa shida na

raha. Kanga yenye ujumbe huu huweza kutumiwa kumpa moyo mtu anayepitia shida fulani katika ndoa ama uchumba.

Majina *kuolewa ni sheria kuzaa ni majaliwa* na *mme ni kazi mke ni tabia* ni mifano mizuri ya jinsi kanga zinavyoeleza falsafa zinazoongoza maisha ya wapwani. Mfano wa kwanza unaonyesha imani ya wapwani kuwa lazima mwanamke aolewe. Hata hivyo, ingawa inatarajiwa kuwa ndoa huja na watoto, binadamu hana uwezo wa kulazimisha kuja kwao bali ni Mungu tu mwenye uwezo wa kupeana watoto. Katika mfano wa pili tunakumbana na matarajio ya jamii hii kuhusu jinsia tofauti. Mwanamke husifika kwa tabia nzuri ilhali hadhi ya mwanamme hupimwa kwa kazi yake. Isitoshe, jina hili *Mme ni kazi mke ni tabia*, linaweza kufasiriwa kwa njia tofauti kutegemea hali tofauti. Kwa mfano:

a) Kama mwanamme anaonekana kuwa mvivu na anashindwa hata kulisha familia yake, basi mkewe anaweza kutandika ama kujifunga kanga yenye maneno haya ili kuonyesha kero kwa tabia ya mumewe. Ikiwa mwanamme anayelengwa na ujumbe huu anashiriki utamaduni sawa na mkewe, basi ataelewa ujumbe uliokusudiwa kufikishwa.

b) Kanga yenye ujumbe huo pia inaweza kuvaliwa kama sare ya arusi ili kuwahimiza maarusi na kuwakumbusha matarajio ya wanajamii. Katika ndoa, mke anatarajiwa kuwa na mienendo inayokubalika katika jamii huku mume akitarajiwa afanye kazi kwa bidii ili awalishe wote wanaomtegemea.

c) Ujumbe huu pia unaweza kufasiriwa kama usemi wa jumla unaoelezea mila, desturi na imani za wapwani ambapo mwanamme anaheshimika kutokana na uwezo wake wa kujimudu kimaisha.

Mifano a), b) na c) inathibitisha kuwa mandhari, mila na desturi za washiriki wa mawasiliano huathiri jinsi ujumbe unavyofasiriwa. Vile vile, tumebainisha kuwa ni muhimu kuelewa maana na sababu ya mambo katika jamii hii ya Wapwani ili kuelewa mchakato wa mawasiliano kupitia kwa kanga; mwendo wa maisha yao na maelezo ya vitendo vya wanajamii. Kwa mfano, kwa nini jeneza la mwanamke Muislamu lifungwe kwa kanga na la mwanamme lisifungwe? Kwa nini mwanamme aliyeoa aruhusiwe kuvaa kanga anapolala usiku na kapera asiruhusiwe kuvaa kanga? Kwa nini mwanamke kumtupia kanga mwanamme anayegombana naye ni ishara ya dharau kwa mwanamme huyo? Tunapoelewa mambo haya tunajipata katika nafasi nzuri zaidi ya kueleza matukio yanayoenda sambamba na mawasiliano.

## 4.2 Mitagusano baina ya Washiriki wa Mawasiliano

Mfumo wa maisha ya wapwani umewafanya wawe katika hali ya kukutana na kutagusana kila mara na umezua kuzoeana na kufanya watu waanze kupishana kimavazi, kiupishi, kimapenzi na kimaisha kwa jumla. Aghalabu tabia hii huleta migongano katika jamii na kuzua kuzoeana. Miongoni mwa mbinu zinazotumiwa kuchokozana na kupishana ni kupitia kwa kanga ambapo majina kama haya hutumiwa:

- *Mtasema mtachoka simuachi haniachi*
- *Muzidi kupalilia sisi yetu twajilia*
- *Pekepeke za jirani hazinitoi ndani*
- *Wangeweka vikao vitawadhuru wao*
- *Kama unaweza mtie kamba mumeo*

Sifa nyingine bayana ni kuwa nyumba nyingi katika Pwani ya Kenya zimejengwa kwa mtindo wa Kiswahili ambapo milango inaangaliana. (Tazama picha 16) Isitoshe, wengi wa wakaazi wa pwani wamekuzwa na imani kuwa wao ni jamii moja. Kwa mfano, utapata mtoto wa Kigunya akimheshimu na kumchukua mama Mgiriama[11] kama mamake mzazi. Wakati mwingine, jirani mmoja anapopika chakula maalum kama chapati, pilau ama biriani huwajibika kuwagawia majirani ili kuendeleza udugu na ujirani. Ili kuthibitisha haya, msaidizi wetu mmoja (Fatma), alitupeleka katika nyumba kadhaa ambapo wapangaji wote walipika na kula pamoja. Kila nyumba (familia) ina zamu ya kupika chakula kinacholiwa na wakaazi wote wa nyumba hiyo. Tukizingatia haya, tunagundua kuwa tabia ya majirani kutaka kujua maisha ya wenzao ni jambo linalotarajiwa kutokana na kutangamana kwa kila siku miongoni mwa wanajamii.

### 4.3 Mitagusano baina ya Wauzaji na Wanunuzi wa Kanga

Wauzaji wa kanga walithibitisha madai kuwa jina la kanga ni muhimu zaidi ya rangi na umaridadi. Walituambia kuwa wateja huzingatia zaidi ujumbe na wengi wao huangalia swala la rangi baada ya kuchagua maneno. Hali hii imewalazimu kujua maneno ya kanga zote ili waweze kuwasaidia wanunuzi kufanya uamuzi kuhusu kanga ya kununua. Yafuatayo ni madondoo ya mazungumzo tuliyosikia baina ya wauzaji na wanunuzi wa kanga.[12]

***Dondoo I***

*Mnunuzi: Asalam aleikum*

*Muuzaji: Aleikum salaam*

*Mnunuzi: Una ipi ya zawadi ya arusi?*

---

[11] Wagunya na Wagiriama ni miongoni mwa wakaazi wa Pwani ya Kenya

[12] Watafiti wamenakili mazungumzo haya kwa kubadili lahaja.

*Muuzaji: Tuna nyingi sana (anajibu huku akitoa rundo la kanga kisha anaanza kumsomea moja baada ya nyingine) Utachukua ipi?*

*Mnunuzi: Nipe Hiyo inayosema Ndoa huozwa mbinguni*

*Muuzaji anamtolea kanga nne za rangi tofauti. Mwanamke huyu (mnunuzi) anachagua ile ya kijani kibichi kisha anailipia na kuondoka.*

***Dondoo II***

*Muuzaji: Hujambo*

*Mnunuzi: Sijambo, nataka 'latest', ni zipi zilizoingia*

*Muuzaji : Kuna 'Mulidhani nitadhirika kumbe Nimetajirika, Sitoi neno jicho latosha, Nyumba yenye upendo haikosi visiki, Radhi ya mama ni stara kwa mwana na Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa (zote zinatandazwa mezani)*

*Mnunuzi: Hewala! (Anasema kisha anaangua kicheko)Nipe hiyo ya mwisho*

*Muuzaji: Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa?*

*Mnunuzi: Eee hiyo*

*Muuzaji: Ipi?*

*Mnunuzi: Nipe nyekundu na 'brown' na zote ziwe nzito.*

*Anafungiwa kanga zake na kuondoka.*

***Dondoo III***

*(wanawake wawili wasiozidi miaka ishirini na mbili wanaingia dukani)*

*Muuzaji: Vipi*

*Wanunuzi: Poa. Tunatafuta sare ya arusi.*

*Muuzaji: Aa! Nani yuaolewa?*

*Mmoja wa wanunuzi: Aaa nawe wacha udaku. Hebu tupe majina ya arusi tuone?*

*Muuzaji: (Anawatajia majina mengi ya arusi kisha anawatolea kanga yenye waridi) pia kuna hii lakini imefungwa hadi mwisho wa mwezi huu.*[13]

*Mnunuzi mmoja: Hebu tuone maneno*

*Muuzaji: Inasema ' Ua langu la moyoni lanipa raha maishani' Mwaionaje?*

*Mnunuzi mmoja: Ni nzuri sana. Naona pia nasi tutaifungisha. Arusi yangu ni ya jumamosi ya kwanza ya mwezi ujao. Na nimeamua hiyo ndio sare yangu. Tulipe sasa ama tulipe tukija wiki ijayo?*

*Muuzaji: Chaguo ni lako, lakini afadhali ulipe sasa kama una pesa ndio ukija iwe ni kuchukua tu.*

*Wanawake hawa wanaondoka wakiwa wameagiza gora thelathini.*

Mifano hii mitatu inathibitisha na kuwakilisha hali tuliyokumbana nayo katika maduka yote ya kuuza kanga tuliyotembelea. Mtindo wa kununua kanga ulihusu wanunuzi kuulizia jina la kanga kabla ya kuzingatia rangi wala umaridadi. Hii inaonyesha kuwa, ujumbe wa kanga ni muhimu zaidi ya rangi na umaridadi.

Hali ya wauzaji kuwasaidia wateja wao kufanya uamuzi kuhusu kanga za kununua inaonyesha kuwa, wauzaji wa kanga wana dhima maalum ya kufasiri, kusimbua na kuweka katika muktadha mahsusi mahitaji ya wanunuzi.

Aidha tuligundua kuwa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi yalijaa ucheshi, utani na udadisi . Wauzaji walionekana kuelewa wateja wao na walibadilisha lugha kutegemea umri na hadhi. Kwa mfano, tunaona katika dondoo la tatu kuwa kubadilisha msimbo kunatokea na badala ya salamu rasmi, muuzaji anawasalimia

---

[13] Kufungwa kwa kanga kuna maana kuwa, muuzaji hawezi kuuza kanga yenye maneno fulani hadi sherehe iliyosababisha kanga hiyo itengenezwe iishe.

wanunuzi wake kwa kusema “Vipi!” nao wanajibu kutumia lugha hiyohiyo kwa kusema “poa”. Katika mfano huo huo, tunaona mnunuzi akionyesha hali ya kutaka kujua zaidi namna kanga itakavyotumiwa. Tulipomuuliza baadaye kwa nini alionyesha hamu ya kujua zaidi, alitueleza kwamba kazi yake ilihusu kutangamana na watu tofauti na lazima aonyeshe kila mteja kuwa anamjali.

### 4.4 Kanga kama Utanzu wa Fasihi

Majina ya kanga hushughulika na maisha ya wanajamii na huchota taarifa na mada zake kutoka kwa matukio ya jamii ya wapwani. Majina ya kanga yanaweza kutumiwa kama kumbukumbu za utamaduni wa wanajamii kwani fasihi inazidi kupoteza hali yake ya kiusimulizi kadri jamii inavyozidi kujiimarisha katika nyanja za teknolojia mpya kama vile tarakilishi, runinga, simu za rununu, redio, na sinema. Kwa hivyo, ni muhimu kuzindua fasihi mpya, tanzu mpya zenye kitambulisho cha Kiafrika (riwaya, tamthilia, mashairi na mavazi ya kisasa yenye uhalisia wa Kiafrika).

Fasihi ina jukumu la kuweka wazi maadili, falsafa, imani na utamaduni wa jamii husika. Mathalan katika hadithi fupi, riwaya, mashairi, tamthilia na fasihi simulizi jamii huelimika na kuburudika. Mbali na hayo, maadili, falsafa, imani na utamaduni wa jamii husika hudhihirika. Vivyo hivyo kanga ina uwezo wa kufanya kazi hizi za fasihi. Miongoni mwa majina ya kanga yanayoweza kutumiwa kuthibitisha madai yetu ni: *Jirani mwema ni asiye kusengenya, Furaha na msiba ndicho kidunia, Nani kama mama, Janjaruka uishi, Ndoa huozwa mbinguni* na *Mungu ndiye mwongozi wa mambo yote.*

Mbali na uwezo wa kanga kuhifadhi mila na desturi za wapwani, majina yaliyo kwenye kanga ni hifadhi ya kisanii. Mengi ya majina tuliyokusanya yameandikwa

kwa usanii na ubunifu wa hali ya juu. Kama tulivyotaja awali, mengi yao yaliandikwa kishairi – yana mahadhi na mdundo wa kuimbika na vina vyake vina urari.[14] Isitoshe, maudhui yanayozungumziwa katika kanga huwa yanalenga jamii na huwa yamewasilishwa kimafumbo na wakati mwingine huandikwa kwa kutumia lugha ya moja kwa moja.

## 4.5 Hitimisho

Sura ya nne imezama katika kubainisha umuhimu wa muktadha katika uchunguzi wowote wa kimawasiliano. Sura hii imeonyesha umuhimu wa kuzingatia wahusika, mazingira mnamotokea mawasiliano, wakati mawasiliano haya yanafanyika na hali iliyotangulia mawasiliano hayo. Hali hii inatokana na haja ya kufanya ufasiri unaofaa hasa ikizingatiwa kuwa, jina la kanga moja linaweza kubeba ujumbe tofauti kutegema mandhari, wahusika, wakati na hali iliyotangulia mawasiliano hayo.

Sura ya tano inatoa muhtasari wa tasnifu huku ikiwasilisha matokeo, mapendekezo na hitimisho la tasnifu.

[14] Tumepiga kistari chini ya sehemu za majina ya kanga ili kudhihirisha dai hili.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Azma ya tasnifu imekuwa kufafanua kanga kama chombo cha mawasiliano huku tukichunguza jinsi mawasiliano kupitia kwa kanga hufanyika. Mbali na kusitiri uchi vazi hili limeimarika kama chombo muhimu katika ulingo wa mawasiliano miongoni mwa wapwani.

Mbali na hayo, madhumini ya tasnifu hii yamekuwa kuchunguza kanga kama makala ya kisanii inayosomeka na kufasirika. Aidha, tumekuwa tukitathmini dhima ya kanga katika mikakati ya ufumbaji na pia tumebainisha dhima za kiisimu jamii za kanga katika miktadha ambamo wanawake wapwani huwa na mazoea ya kuitumia.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete hizi:

i. Kanga ni makala ya kisanii inayoweza kusomeka na kufasiriwa.

ii. Maandishi yaliyo kwenye kanga huwa na maana fiche.

iii. Hakuna jambo katika jamii lisiloweza kuwasilishwa kupitia kwa kanga.

iv. Wapwani hutumia kanga zao kwa kuzingatia jina, rangi na umaridadi

Kati ya nadharia tete tulizotaja ni nadharia i) na iii) ambazo zilidhihirika kuwa ukweli. Tumegundua kuwa si jumbe zote zilizo kwenye kanga zenye maana fiche bali kuna majina kadhaa ya kanga yanayobeba ujumbe wazi. Vile vile, utafiti huu umedhihirisha kuwa, jina la kanga ni muhimu zaidi ya rangi na umaridadi. Matokeo ya utafiti yamelandana na nadharia zilizoongoza utafiti huu kwani tumebainisha

kuwa, kanga maalum huvaliwa wakati maalum kutegemea muktadha unaoingiana na jina la kanga husika. Isitoshe, majina yote ya kanga huwa na maana maalum.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Katika sura ya kwanza, tulitoa msingi wa tasnifu yetu kwa kueleza usuli wa utafiti, kulifafanua suala la utafiti na kueleza madhumuni na umuhimu wa utafiti wetu. Aidha, sura hii iliwasilisha nadharia na nadharia tete zilizoongoza utafiti huu. Watafiti pia wameeleza jinsi walivyokusanya na kisha kuchanganua data. Mbali na hayo, maandishi ya watafiti wa awali yalihakikiwa katika sura hii ya kwanza.

Sura ya pili imejadili asili na dhima za kanga huku ikionyesha jinsi wapwani wanavyofaidika kwa vazi hili katika maisha yao ya kila siku. Dhima ya kimawasiliano imejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu.

Sura ya nne imeshughulikia kanga kama kioo cha jamii ya wapwani. Sura hii imetuonyesha kuwa majina ya kanga huchotwa kutoka kwa matukio ya kila siku katika jamii. Isitoshe, majina haya huwasilisha tabia, imani, mila na desturi za wanajamii.

Sura ya tano imenuiwa kuhitimisha tasnifu hii kwa kuwasilisha muhtasari wa matokeo na kutoa mapendekezo katika muktadha wa utafiti huu.

Mawasiliano miongoni mwa wanajamii ni kiungo muhimu sana cha kudumisha uhusiano mwema. Katika jamii ya wapwani, mawasiliano kupitia kwa kanga yamekita mizizi. Mbali na kuwa vazi linalothaminiwa kwa uamilifu wake wa kusitiri uchi,

maandishi yaliyo upande wa chini wa vazi hili hutumiwa kuwasilisha ujumbe kuhusu mada mbalimbali. Mara nyingi mada hizi hueleza hisia za wanajamii kuhusu hali kama mapenzi, misiba, hasira na chuki. Mbali na hayo, kanga hubeba jumbe za kushauri na kueneza habari kuhusu maswala yanayoikumba jamii kama uraibu wa madawa ya kulevya, maradhi, haki za wanawake na watoto, umuhimu wa elimu na umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

Tasnifu hii imebainisha kuwa, mawasiliano kupitia kwa kanga huathiriwa na vigezo vifuatavyo:

- Mila na desturi za washiriki wa mawasiliano
- Miktadha mnamotokea mawasiliano hayo – uhusiano wa wanaohusika, hali ambayo washiriki wa mawasiliano wamo, hali iliyotangulia na kusababisha haja ya kuwasilisha ujumbe na lugha inayotumiwa.
- Wakati mawasiliano yanapofanyika.
- Misukumo ya kijamii, kidini na kiuchumi.

Tofauti na nyenzo zingine za mawasiliano, kanga huwasilisha ujumbe kwa kutumia majina yaliyochotwa kutoka kwa jamii yaani ni zao la jamii na huandikwa kwa lugha inayoeleweka na watu wengi – Kiswahili. Hali hii inafanya nyenzo ya kuwasiliana kwa kanga kuwa ya kufaa zaidi.

Mbali na kutimiza madhumuni ya utafiti, tumetambulisha kanga kama kioo cha jamii kinachoweza kutumiwa kujenga na kurekebisha jamii husika.

## 5.2 Mapendekezo

Utafiti huu umeonyesha kuwa kuna haja ya kutambua kanga kama chombo cha mawasiliano katika jumuiya kubwa zaidi nchini Kenya kwani kadri miaka inavyozidi kwenda, ndivyo mbinu hii ya mawasiliano inavyozidi kuimarika na kukita mizizi.

Mashirika yasiyo ya kiserikali na makundi yanayojishughulisha na maswala yanayoikumba jamii, yatumie kanga ili kufikia hadhira kubwa zaidi. Mbali na kuwasaidia walengwa wao kujisitiri, watakuwa wanarahisisha mawasiliano kwani majina ya kanga huandikwa kwa Kiswahili – lugha inayofahamika na kutumiwa na Wakenya wengi.

Kwa kuchukulia mazao ya utamaduni kama matini, tunapata mfumo mzuri wa kufafanua mawasiliano ya binadamu kwa kuhusisha vitendo vyao, mandhari yao, lugha yao na jinsi wanavyowasilisha maswala yanayowakumba katika jamii. Kanga inaweza kutumiwa kupiga vita matatizo yafuatayo: Uraibu wa madawa ya kulevya, unyanyasaji wa wanawake na watoto, ukahaba na ukosefu wa maadili katika jamii, magonjwa, ukosefu wa elimu, tohara ya wanawake na kupinga kuozwa kwa watoto wadogo. Ni muhimu tufungamanishe utamaduni wetu na maswala mengine yanayoikumba jamii yetu.

Tasnifu hii pia inapendekeza kutambuliwa kwa kanga kama sanaa mojawapo inayoweza kuimarisha fasihi za Kiafrika na kuwatambulisha Waafrika.

Tasnifu hii imethibitisha kuwa, mavazi yanaweza kuwa mbinu faafu ya mawasiliano. Watafiti wa baadaye wanaweza kuifaidi jamii zaidi kwa kuchunguza mkondo huu mpya wa kuwasilisha ujumbe kupitia kwa mavazi.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

i. Kuchunguza kanga kama makala ya kisanii inayosomeka na kufasirika

ii. Kutathmini dhima ya kanga katika mikakati ya ufumbaji

iii. Kubainisha dhima za kiisimu- jamii za kanga katika miktadha ambamo wanawake wapwani huwa na mazoea ya kuitumia.

Tumethibitisha katika tasnifu hii kuwa, kanga ni vazi lenye maandishi yanayobeba ujumbe. Tumedhihirisha kuwa maandishi haya ni muhimu kuliko rangi na umaridadi kutokana na uvumbuzi kwamba wanawake wapwani hununua na kutumia kanga zao kutegemea jina wala si rangi ama umaridadi. Pia tumebainisha kuwa, ujumbe unaobebwa na kanga huweza kufasiriwa kwa njia tofauti kutegemea tajriba za wanaoshiriki mawasiliano na muktadha mnamotokea mawasiliano hayo.

Ingawa nadharia tete (ii) ilionyesha kuwa maandishi yaliyo kwenye kanga huwa na maana fiche. Imebainika wazi katika tasnifu hii kuwa kuna kanga zinazowasilisha ujumbe kwa njia ya moja kwa moja na kuna zile zinazotumia mbinu ya ufumbaji.

Isitoshe, tasnifu hii imeangazia dhima za kiisimu – jamii za kanga ambapo wanajamii hutumia vazi hili lenye maandishi kuelimishana, kukosoana, kueleza hisia zao, kuhifadhi mila na desturi za jamii na kueleza mielekeo na falsafa za jamii husika. Aidha, tumetambulisha umuhimu wa utamaduni mkongwe unavyobainika katika matumizi na mawasiliano kupitia kwa kanga.

**MAREJELEO**

Abdulaziz, M. H**.** (1979). *Muyaka: Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Alford, R. (1996). *"Adornment" in Levinson D. & Ember M. (whrr) Encyclopedia of Cultural Anthropology.* New York: Henry & Holt Company.

Audi, R (mhariri) (1999). *The Cambridge Dictionary of Philosophy 2nd edition. Cambridge*: The Cambridge University Press.

Barbra, M. M. na Pugh (1987). *Women in their Speech communities, Language, Communication and Education.* Sydney: Groom Herb.

Brown, G. (1995). Speakers, Listeners and Communication: *Explorations in discourse analysis.* New York: Cambridge University press.

Chukwu, N. C. (2002). *Introduction to Philosophy in an African Perspective*. Eldoret: Zapf Chancery Research Consultants and Publishers.

Coulthard, M. (1985). *An Introduction to discourse Analysis 2nd edition.* England: Pearson Education Limited.

Danesi, M. (2002). *Understanding Media semiotics.* New York: Oxford University Press.

Eliot, T. S. (1988). *Notes towards the Definition of Culture.* Bungay: Richard Clay Limited.

Ellis, R na McClintock A. (1990). If You Take my Meaning: *Theory into Practice in Human Communication.* New York: Edward Arnold, a Division of Hodder and Stoughton

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. UK: Longman Group.

Fairclough, N. (1992). *Discourse and Social Change*. Cambridge: Polity Press.

Fisher, A. (1984). *Africa Adorned*. London: Collins and Grafton Street.

Griffen, E. M. (1997). *A First Look at Communication Theory*. The McGraw – Hill Companies Inc.

Halliday, M. A. K. (1978). Language as Social Semiotic: *The Social Interpretation of Language and Meaning.* New York: Edward Arnold, a Division of Hodder and Stoughton.

Hanby J. na Bygot D. (1984). *Kanga 101 uses*. Nairobi: Lino typesetters (K) Ltd.

Hansen, A. na wenzake (1998). *Mass Communication research Methods.* Newyork: Palgrave, Houndmills basingstroke.

Harris, S. (1993). *Human Communications* 3rd edition. England: NCC Blackwell Limited.

Hawkes, T (1977). *Structuralism and Semiotics*. London: Routledge.

Heaton, J. na Groves J. (1999). *Introducing Wittgenstein*. UK: Icon Books LTD.

Hodge, R. na Kress G. (1988). *Social Semiotics*. UK: Polity Press.

Jahadhmy, A. A. (1975). Kusanyiko la Mashairi *Anthology of Swahili Poetry*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Levine, R.A (1973). *Culture, Behaviour and Personality*. Chicago: Aldine Publishing Company.

Luzbetak, L. J. (1970). *The Church and Cultures*. Illinois: Divine word Publications.

Mazrui, A. (1982). The African Condition: *The Reith Lectures*. Heinemann Educational Books Ltd.

Middleton, J. (1992). *The World of the Swahili, An African Mercantile Civilization*. London: Yale University Press.

Okot, P'Bitek (1986). Artist the Ruler: *Essays on Art, Culture and Values*. Nairobi: Heinemann Kenya Limited.

Poyatos, F. (1983). New Perspectives in Nonverbal Communication: *Studies in Cultural anthropology, Social Psychology, Linguistics, Literature and Semiotics*. New York: Pergamon Press.

Tannen, D. (1995). *Gender and Discourcse*. Oxford: Oxford University Press.

Warren, B. A C (1988). *Gender Issues in Field Research*. California: Sage Publications.

Wittgenstein, L. (1989). *Tractatus Logico – Philosophicus.* London: Routledge.

Woodward, K (2002). *Understanding Identity.* New York: Oxford University Press.

Yule, (1985). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

**Tovuti**

http://www.anthrosource.net/doi/pdf/10.1525/ahu.1981.6.1.2

http://www.columbia.edu/cu/web/data/indiv/area/idass/Beck_Marie%20htm%2022/5/002 Indirect? Ambiguous communication, kanga /leso, comics, Popular Culture

http://www.ifeas.uni-mainz.de/swaFo/Beck.htm (2001) On Communication with Kanga' Swahili Forum 8 (= AAP 68) 157-169.

http://oak.cats.ohiou.edu/~mv537899/sc.htm (27/4/2006) Krawsczyn E. A Critique of Roland Barthes' Semiotics theory.

LHP://ww.g/ww.g/com.com/hassan/kanga.html-- > 17.11.2002.

http://www.glcom.com/hassan/kanga/kanga1.html (2004).

http://www.glcom.com/hassan/kanga_history.html (2004).

http://www.kristisiegel.com/theory.htm (22/4/2006) Introduction to Modern Literature.

http://www///wiki/semiotics (27/4/2006) Wikipedia the free encyclopedia.

http://www.yale.edu/hraf/publications_body_encyclopedias.htm.

**Kamusi**

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981) Taasisi ya Uchanganuzi wa Kiswahili, Dar-es-TUKI: Saalam

Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili (2000) Tolea la pili. Dar es Salaam

**Majarida na Makala Mengine**

Abdulqadir, M. (2007) Leso and Its Social Functions among the Swahili (haijapishwa).

Akong'a, J.J. (1980) "Social Training Strategies: *The Swahili of Old Town. Mombasa, Kenya*" Institute of African Studies U.O.N Paper no 132.

Beck, R. M (2000) Aesthetics of Communication: texts on textiles (kanga) from the East African Coast (Swahili) in: Journal of Research in African Literatures vol. 31 No. 4:104 -124.

Beck, R. M. (2005) Texts on Textiles: Proverbiality as Characteristic of equivocal communication at the east African Coast (Swahili) in: Journal of African Studies, Vol. 17 No. 2: 131-160.

Kariuki, J. "What it takes to be a winner: Poll-Smart Candidates, Saying it with Clothes" Election 2002 Column, Nairobi, Thursday Nation, November 28, 2002.

Mayoyo, P. "Leso Takes Centre Stage in Hunt for Coast Votes" Election 2002 Column, Nairobi, Thursday Nation, November 14, 2002.

Spencer-Oatey, H. (1993) Conceptions of Social- relations & Pragmatic research. in: Journal of Pragmatics Vol.20: 27- 47.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO I

**<u>Ratiba ya kazi</u>**

| | |
|---|---|
| Old Town | Wiki ya kwanza |
| Mwembe Tayari | Wiki ya pili |
| Bondeni | Wiki ya tatu |
| Mwembe Kuku | Wiki ya nne |
| Tononoka | Wiki ya tano |
| Sabasaba | Wiki ya sita |
| Bombolulu | Wiki ya saba |
| Kisauni | Wiki ya nane |
| Makaburini | Wiki ya tisa |
| Majengo | Wiki ya kumi |

Wiki za mwisho mbili zilitumiwa katika maktaba ya jumba la makumbusho la Mombasa.

**KIAMBATISHO II**

**Baadhi ya maswali yaliyoongoza usaili**

**a) Kwa watumiaji Kanga**

1 Je, unaponunua kanga huwa unazingatia nini? (Rangi, maandishi au umaridadi)

2 Je, Kuna mtu au jambo lolote linalokushurutisha kutumia kanga?

3 Kwa maoni yako, kanga inachangia vipi mawasiliano miongoni mwa wanajamii?

4 Je, kuna wakati wowote maishani mwako ambapo umetumia kanga kuwasilisha ujumbe kwa mtu maalum? Ikiwa upo, ulifaulu au la?

**b) Kwa wauzaji na watengenezaji Kanga**

1 Je wateja wako huzingatia nini wanaponunua kanga?

2 Wateja wako ni wanawake au wanaume?

3 Je kuna wakati maalumu ambapo unauza kanga nyingi zaidi ya wakati mwingine? Kama upo ni wakati upi?

4 Je huwa unachagua maandishi ya kuweka kwa kanga vipi?

5 Kwa maoni yako, maandishi yaliyo kwenye kanga huwa yanafaulu katika kuufikisha ujumbe uliokusudiwa?

**KIAMBATISHO III**

**Nakala za baadhi ya Barua pepe Tulizotuma na Kupokea**

***Baruapepe A***

*Hallo Clarissa,*

*My name is Julie Wacharo from Eldoret Kenya. I got your address through Prof. Naomi Shitemi who is my supervisor. Im currently doing my masters in Kiswahili and my research topic is Kanga - sajili maalum ya Kisanii na kimawasiliano (Kanga a piece of art and a tool of communication)*

*Professor says you had a very successful exhibition on the same. Kindly tell me how your people reacted to the exhibition and if you have any materials on the same, I'll really appreciate if you shared it with me.*

*Asante sana (thanks a lot)*

*Julie*

***Baruapepe B***

*Wednesday, March 26, 2008 4:02 AM*

*"Clarissa Vierke" <clarissa.vierke@gmx.de>*

*To:*

*"'julia wacharo'" <jwacharo@yahoo.com>*

*Cc:*

*"'NAOMI LUCHERA SHITEMI'" <nluchera@gmail.com>*

*Mpendwa Julie,*

*Asante kwa baruapepe yako. Prof. Naomi Shitemi alikuwa ameshaniambia kwamba utaniandikia baruapepe. Kwa kweli tulikuwa na maonyesho juu ya leso hapa bayreuth katika kituo cha sanaa ya kiafrika kinachoitwa Iwalewa-Haus. Watu walikuwa waliyapenda maonyesho hayo kwa sababu tofautitofauti: Kwa kwanza, kwa sababu ya "designs", mapambo ya leso, rangi zao na mitindo yao zilizo za kuvutia.*

*Tena, leso, haswa leso zilizotoka kwa ukumbusho wa sherehe fulani, (anniversary fulani), ni kama shahada za kihistoria ama kioo cha matokeo katika jamii na historia yake. Tena, Watu walipenda majina ya leso: fikra ya kuwasiliana kwa njia hiyo ni kitu kigeni kwetu. Katika utamaduni wetu (na katika utamaduni wenu huko Kenya pia), siku hizi, watu wengi wanavaa Tshirts, Tshirts za football, Tshirts za chama fulani*

*n.k. kwa ajili ya kijitumbulisha - ni swala la "identity" lililo muhimu sana. Kwa hivyo, kwa kipengele fulani - unaweza kulinganisha leso na Tshirts.*

*Lakini, vilevile ziko tofauti: Leso zinaingia na zinatumika kitaka mawasiliano ya kila siku; unaweza kutumia leso ikiwa una ujumbe fulani kwa mtu fulani. Kwa hivyo, a leso is often more specfic (for a specific aim of communication) than a TShirt. Halafu, leso zinatumia mithali zaidi.*

*Kwa kusema la kweli, sina mengi ya kusema kuhusu mada hiyo: mimi sikuwa na mchango katika maonyesho hayo. Yalikuwa maonyesho ya mtu kutoka mji mwingine anayependa leso na anayekusanya leso. Tena hakuna materials nyingine kuhusu maonyesho hayo: hakuna "catalogue".*

*Lakini, wapo wataalamu ambao wamefanya utafiti kuhusu leso. Mmojawapo ambaye aliandika PhD yake kuhusu leso anaitwa Rose Marie Beck. Kitabu chake cha PhD ni kwa Kijerumani kwa hivyo hakina maana kwako. Lakini vilevile, ameandika baadhi ya makala kwa Kiingereza kama zifuatazo:*
*2001.a 'Ambiguous signs. On communication with kanga', Swahili Forum 8 (=AAP 68): 157 - 169. 2000. A 'Aesthetics of communication: Texts on textiles (leso) from the East African Coast (Swahili)', special issue on the verbal and the visual arts, hg. v. Mineke Schipper, Research in African Literatures 31, 4: 104-124.Pamoja na Frank Wittmann alitoa kitabu kinachoitwa "African Media Cultures.Transdisciplinary Perspectives – Cultures de Médias en Afrique.Perspectives Transdisciplinaires."*

*Sijui ikiwa vitabu na makala zipo ndani ya maktaba yenu. Labda Professa wako, Prof. Naomi Shitemi ama Nathan Ogechi wanazo. Uzungumze nao. Ikiwa hawana naweza kukupostia copies za makala kwa njia ya posta (ama kwa njia ya email). Tafadhali, unipe anwani yako ya posta ama ile ya idara ya Kiswahili ya chuo kikuu. Tena, nakupa shauri ya kuzungumza na Rose Marie Beck mwenyewe: r.m.beck@em.uni-frankfurt.de Yeye ni mtu mzuri sana, kwa hivyo usiogope kuzungumza naye.*
*Salamu nyingi kutoka Ujerumani,*
*Clarissa*

***Barua pepe C***

*Jambo Profesa Marie,*

*My name is Julie Wacharo from Moi University Kenya. I got your address from Clarissa after inquiring about an exhibition on the kanga that was held in Bayreuth. I am doing my Masters in Kiswahili at Moi University - Kenya and my research topic is Kanga - Sajili Maalum ya Kimawasiliano na Kisanii (Kanga as a tool of Communication and as a piece of art.) I am sure you have a lot you can offer in the area. Clarissa says you have done a lot of research on the topic. Kindly send me any reference material that can be of help.*

*Asante sana*

*Wacharo*

***Baruapepe D***

*Sunday, April 13, 2008 12:06 PM*

*From:*

*"Rose Marie Beck" <r.m.beck@em.uni-frankfurt.de>*

*Add sender to Contacts*

*To:*

*"julia wacharo" <jwacharo@yahoo.com>*

*Message contains attachments*

*SF8Beck.pdf (161KB), Beck 2005 Journal of African Cultural Studies.pdf (167KB)*

*Mpendwa Julie Wacharo,*
*natumai hujambo. Naona jina lako ni jina la pwani, au siyo? Hongera na utafiti wako na jambo la umuhimu kabisa! Appended to this mail I send you two articles of mine concerning the subject, where you should also be able to find most of the literature I have complied with regard to the leso. I do also have some odd notes here and there on the iconography of the leso, but this I would prefer to talk about, and not send it (as it is not finished at all). Unfortunately most of what I have written about the topic, including my Ph.D. is in German. I expect to be in Kenya sometime this year, either July or August, and I will come to Eldoret anyway. I'll let you know, hopefully If I can help more, please don't heistate to let me know.*

*Kind regards Rose Marie*
*Dr. Rose Marie Beck*
*Institut für Afrikanische Sprachwissenschaften*
*Universität Frankfurt*
*Dantestr. 4-6*
*60054 Frankfurt*

***Baruapepe E***
*Thursday, June 19, 2008 2:10 AM*
*From:*
*"Saadu Hashim" <saaduhashim@yahoo.com>*
*To:*
*jwacharo@yahoo.com*
*Message contains attachments*
*Kanga history.htm (41KB), khanga.doc (66KB)*

*Hallo!*
*Sorry for silence for a while- i was down with malaria so had been at home for over a week. I got some info from Mbarak on khanga, I have attached it and it has a link where you can open to see pictures of khanga. Infact it is a website on khanga. Really sorry for the delay and I do hope it is not too late for your research.*

*PPS. We are eagerly awaiting for a copy of your research doc so as to keep in our library!*

*Saadu Rashid*
*Fort Jesus*

***Barua F***
*From: julia wacharo <jwacharo@yahoo.com>*
*Subject: Re: EXHIBITION PHOTOs*
*To: "Saadu Hashim" <saaduhashim@yahoo.com>*
*Date: Tuesday, June 24, 2008, 2:43 AM*
*Hallo Saadu,*
*Hope you are fine. Eldoret is ok but very cold. How is*
*Mombasa?*

*The documents you sent me were very helpful especially the one by Mubarak.*
*Was wondering if you got the "Swahili Attire exhibition" photos. If you get them, kindly mail them to me Since I have some gaps to fill.*
*I wish you good health.*

*With regards,*
*Wacharo*

***Barua G***
*Re: EXHIBITION PHOTOs*
*Wednesday, June 25, 2008 11:37 PM*
*From:*
*"Saadu Hashim" <saaduhashim@yahoo.com>*

*To:*
*jwacharo@yahoo.com*
*Cc:*
*"mbarak abdallah" <abuamar02@hotmail.com>*

*Hallo to you too. Am much better now. Infact back in the office.*

*I will forward your email to Mbarak so that he can check but I dont think we do have any photos.*

*Any response from him, I will get back to you. All the best in your studies and research- please dont forget to send us a copy of your research project- so we can keep it in the library as a reference for others.*

*Saadu*

**KIAMBATISHO IV**

**Majina Yote Yaliyokusanywa**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Hii ni bahati yangu si makombe si hirizi | **E** |
| 2. | Ulijuaje kama si umbea | **A** |
| 3. | Jirani mwema ni asiye kusengenya | **H** |
| 4. | Usinitolee macho kilicho ndani si chako | **A** |
| 5. | Pendo la dhati huwa ni la kila wakati | **B** |
| 6. | Moyoni nina huzuni waniumiza mwendani | **H** |
| 7. | Mgonjwa hupewa dawa je mdaku hupewa nini | **A** |
| 8. | Yenu siyaulizi je yangu mwayatakiani | **A** |
| 9. | Mungu ni mwingi wa rehema | **E** |
| 10. | Nimepata jibaba lijualo mahaba | **H** |
| 11. | Kukukumbuka sichoki | **H** |
| 12. | Mama mlezi kukusahau siwezi | **F** |
| 13. | Muzidi kupalilia sisi yetu twajilia | **A** |
| 14. | Mama tuzo lako ni pepo kesho akhera | **F** |
| 15. | Harufu yako yautuliza moyo wangu | **B** |
| 16. | Ua langu la moyoni lanipa raha maishani | **B** |
| 17. | Uhasidi wenu haunivunji | **A** |
| 18. | Pole kwa yaliyokufika | **G** |
| 19. | Mti mkuu umeanguka ndege wa mashakani | **G** |
| 20. | Penzi la mama litamu haliishi hamu | **F** |
| 21. | Ukipenda waridi utavumilia miiba | **D** |
| 22. | Tusafianeni nia Mola atatufungulia njia | **E** |
| 23. | Mungu ndiye mwongozi wa mambo yote | **E** |

| | | |
|---|---|---|
| 24. | Penye mema Mungu huzidisha rehema | **E** |
| 25. | Tupendane rafiki Mungu atatuafiki | **E** |
| 26. | Kuregarega sio kufa | **H** |
| 27. | Umesema nimesikia nikikujibu vumilia | **A** |
| 28. | Usizime kandili yako kwa taa ya mwenzako | **D** |
| 29. | Mtasema mtachoka simuachi haniachi | **A** |
| 30. | Ndoa huozwa mbinguni | **C** |
| 31. | Nyumba ya wawili ni kivuli cha amani | **H** |
| 32. | Arusi ni nguzo ya jamii | **C** |
| 33. | Mapenzi hayana subira waridhianapo | **H** |
| 34. | Karibu wangwana kwa arusi ya mwana | **C** |
| 35. | Simtaki bwanako wangu ni mtamu | **J** |
| 36. | Mzazi ni mzazi hata kama hajiwezi | **D** |
| 37. | Hasidi nichukie roho yangu niwachie | **A** |
| 38. | Zawadi ni chochote kupokea usichoke | **H** |
| 39. | Umetuachia kilio na majonzi kutuacha | **G** |
| 40. | Hii ni bahati yangu Mungu kanijalia | **E** |
| 41. | Subira nyumba ya neema | **H** |
| 42. | Neno jema halikosi kujibiwa | **H** |
| 43. | Janjaruka uishi | **D** |
| 44. | Sitasahau hisani uliyo nitendea | **H** |
| 45. | Kuomba si kupata Mungu akitaka atakupa | **E** |
| 46. | Kuolewa ni sheria kuzaa ni majaliwa | **E** |
| 47. | Penzi ni jani hunawiri likiwa moyoni | **B** |
| 48. | Ingawa mmetuondokea hatuchoki kuwaombea | **G** |

| | | |
|---|---|---|
| 49. | Tumpe Mungu shukurani | **E** |
| 50. | Riziki ni kutafuta sio kurukaruka | **D** |
| 51. | Ya wenzenu mdomoni yenu moyoni | **B** |
| 52. | Wema alionifanyia sitoweza kumuacha | **H** |
| 53. | Mpenzi wangu nakupa mkono wa idi | **H** |
| 54. | Si neno nitasubiri | **H** |
| 55. | Wa kukupinga hayuko wala hatachomoka | **H** |
| 56. | Kipi kiliwachoma moyo mpaka mkaniwekea baraza | **A** |
| 57. | Pekepeke za jirani hazinitoi ndani | **A** |
| 58. | Heshima tukipeana daima tutapendana | **J** |
| 59. | Furaha na msiba ndicho kidunia | **G** |
| 60. | Nilikupenda ukajishaua mwenzio yuala maua | **J** |
| 61. | Nipambe nipendeze waigao wasiweze | **H** |
| 62. | Mulidhani nitadhirika kumbe nimetajirika | **J** |
| 63. | Nasononeka moyoni kwa yaliyotufika | **G** |
| 64. | Pekepeke mwisho utabaki peke yako | **A** |
| 65. | Utamaliza bucha zote nyama ni ile ile | **J** |
| 66. | Inua guu gongo laja | **J** |
| 67. | Sitoi neno jicho latosha | **A** |
| 68. | Kama wewe sabasi kwa nini hufanikiwi | **A** |
| 69. | Mapenzi yako ni matamu hayaishi hamu | **B** |
| 70. | Mama ni mama asiyejua mama hana maana | **F** |
| 71. | Mimi na wewe hatuwachani | **H** |
| 72. | Nani kama mama | **F** |
| 73. | Uzuri wa mja ni vitendo vyake | **H** |

| | | |
|---|---|---|
| 74. | Pendo ni mlango wa heri | **H** |
| 75. | Penzi letu waja wasituingilie | **B** |
| 76. | Hata nikitenda wema hamuachi kusema | **A** |
| 77. | Tukiwa na imani daima tutasikizana | **H** |
| 78. | Heri kumfadhili mbuzi kuliko jirani wa hapa | **H** |
| 79. | Subiri kwa Mola wako utapata utakacho | **E** |
| 80. | Nafuta machozi na bado moyo wazidi kulia | **G** |
| 81. | Kaeni mtuwe mimi nina mwenyewe | **H** |
| 82. | Kila jambo tumshukuru Mungu | **E** |
| 83. | Tuheshimu ndoa yetu | **C** |
| 84. | Moyo hausemezeki kwa kitu nikipendacho | **B** |
| 85. | Nyumba ikiwa shwari upendo huzidi nyumbani | **C** |
| 86. | Penzi halina kabila wala mila | **H** |
| 87. | Msihangaike na ulimwengu mtowaji ni Mungu | **D** |
| 88. | Mama nilee vyema uepuke lawama | **F** |
| 89. | Ukipata mshukuru Mungu | **E** |
| 90. | Nyumba yenye upendo haikosi visiki | **D** |
| 91. | Wewe ni wangu wa daima | **B** |
| 92. | Kwenye mapenzi hapakosi fitina | **H** |
| 93. | Maziwa ya mama ni tamu | **F** |
| 94. | Hasidi hana sababu | **A** |
| 95. | Si neno bora uzima | **H** |
| 96. | Wajua tamu yaua sumu umenipeani | **H** |
| 97. | Tupendane duniani tupate amani | **H** |
| 98. | Nia zikiwa pamoja udugu hufana | **H** |

99. Tuombeane kheri kwa siku hii njema **H**

100. Mengine yatawashinda **A**

101. Siadhiriki mimi mja wa stara **A**

102. Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa **J**

103. Ingawa sisemi ujuwe hamuniwezi **J**

104. Penye neema baraka huenea **E**

105. Ingawa kichache tunu ya kutunukiwa **H**

106. Mume ni kazi mke ni tabia **E**

107. Dunia ni mapito binadamu acha maringo **E**

108. Daima u mawazoni naikumbuka yani shani **H**

109. Nenda ukaliwe pesa waganga haweshi **J**

110. Mtu ni tabia yake **H**

111. Ujirani naupenda lakini tabia zimenishinda **J**

112. Kama unaweza mtie kamba mumeo **J**

113. Moyo wa hasidi hauna dawa **J**

114. Wangaeka vikao vitawadhuru wao **A**

115. Si hirizi si mizizi bali ni moyo kupenda **B**

116. Radhi ya mama ni stara kwa mwana **F**

117. Mpendwa wetu safiri salama **G**

118. Ahadi haivunjwi **D**

119. Raha ya dunia ni watoto **H**

120. Yataka tuwe na imani dunia ina mitihani **D**

121. Mwenye huba hafichiki **B**

122. Muungwana hafichiki **H**

123. Hodi hodi naziishe mwaka huu naolewa **A**

| | | |
|---|---|---|
| 124. | Mtenda mema hasahauliki | **H** |
| 125. | Sauti yako yanipumbaza | **B** |
| 126. | Nimechagua kuishi na wewe | **B** |
| 127. | Wimbo mbaya haumbembelezi mtoto | **H** |
| 128. | Wangapi walisema na sasa wako wapi | **J** |
| 129. | Nyumba hujengwa na mke | **D** |
| 130. | Mama astahili sifa na shukrani | **F** |

**KIAMBATISHO V**

**<u>Majina Yaliyoainishwa Kimada</u>**

Kukomesha Udaku **(A)**

i. Ulijuaje kama si umbea
ii. Usinitolee macho kilicho ndani si chako
iii. Mgonjwa hupewa dawa je mdaku hupewa nini?
iv. Yenu siyaulizi yangu mwayatakiani?
v. Muzidi kupalilia sisi yetu twajilia
vi. Uhasidi wenu haunivunji
vii. Umesema nimesikia nikikujibu vumilia
viii. Mtasema mtachoka simuachi haniachi
ix. Hasidi nichukie roho yangu niwachie
x. Ya wenzenu mdomoni yenu moyoni
xi. Kipi kiliwachoma moyo mpaka mkaniwekea baraza
xii. Pekepeke za jirani hazinitoi ndani
xiii. Pekepeke mwisho utabaki peke yako
xiv. Sitoi neno jicho latosha
xv. Kama wewe sabasi kwa nini hufanikiwi
xvi. Hata nikitenda wema hamuachi kusema
xvii. Hasidi hana sababu
xviii. Mengine yatawashinda
xix. Siadhiriki mimi mja wa stara
xx. Wangaeka vikao vitawadhuru wao
xxi. Chaunabe utabaki kunawa na kula huli

Mapenzi **(B)**

i. Pendo la dhati huwa ni la kila wakati
ii. Harufu yako yautuliza moyo wangu
iii. Ua langu la moyoni lanipa raha maishani
iv. Penzi ni jani hunawiri likiwa moyoni
v. Mapenzi yako ni matamu hayaishi hamu
vi. Penzi letu waja wasituingilie
vii. Moyo hausemezeki kwa kitu nikipendacho
viii. Wewe ni wangu wa daima
ix. Si hirizi si mizizi bali ni moyo kupenda
x. Mwenye huba hafichiki
xi. Sauti yako yanipumbaza
xii. Nimechagua kuishi na wewe

Arusi **(C)**

i. Ndoa huozwa mbinguni
ii. Arusi ni nguzo ya jamii
iii. Karibuni wangwana kwa harusi ya mwana
iv. Tuheshimu ndoa yetu
v. Nyumba ikiwa shwari upendo huzidi nyumbani

Mawaidha **(D)**

i. Ukipenda waridi utavumilia miiba
ii. Usizime kandili yako kwa taa ya mwenzako
iii. Mzazi ni mzazi hata kama hajiwezi

iv. Janjaruka uishi
v. Riziki ni kutafuta sio kurukaruka
vi. Msihangaike na ulimwengu mtoaji ni Mungu
vii. Nyumba yenye upendo haikosi visiki
viii. Ahadi haivunjwi
ix. Yataka tuwe na imani dunia ina mitihani

Imani **(E)**

i. Hii ni bahati yangu si makombe si hirizi
ii. Mungu ni mwingi wa rehema
iii. Tusafianeni nia  Mola atatufungulia njia
iv. Mungu ndie mwongozi wa mambo yote
v. Penye mema Mungu huzidisha rehema
vi. Tupendane rafiki Mungu atatuafiki
vii. Hii ni bahati yangu Mungu kanijalia
viii. Kuomba si kupata akitaka atakupa
ix. Kuolewa ni sheria kuzaa ni majaliwa
x. Tumpe Mungu shukrani
xi. Subiri kwa Mola wako utapata utakacho
xii. Kila jambo tumshukuru Mungu
xiii. Ukipata mshukuru Mungu
xiv. Penye neema baraka huenea
xv. Mme ni kazi mke ni tabia
xvi. Dunia ni mapito binadamu acha maringo

Kumuenzi Mama **(F)**

i. Mama mlezi kukusahau siwezi
ii. Mama tuzo lako ni pepo kesho akhera
iii. Penzi la mama litamu haliishi hamu
iv. Mama ni mama asiyejua mama hana maana
v. Nani kama mama
vi. Mama nilee vyema uepuke lawama
vii. Maziwa ya mama ni tamu
viii. Radhi ya mama ni stara kwa mwana
ix. Mama astahili sifa na shukrani

Maombolezi **(G)**

i. Pole kwa yaliyokufika
ii. Mti mkuu umeanguka ndege wa mashakani
iii. Umetuachia kilio na majonzi kutuacha
iv. Ingawa mmetuondokea hatuchoki kuwaombea
v. Furaha na msiba ndicho kidunia
vi. Nasononeka moyoni kwa yaliyotufika
vii. Nafuta machozi na bado moyo wazidi kulia
viii. Mpendwa wetu safiri salama

Kauli **(H)**

i. Jirani mwema ni asiye kusengenya
ii. Moyoni nina huzuni waniumiza mwendani
iii. Nimepata jibaba lijualo mapenzi

iv. Kukukumbuka sichoki

v. Kuregarega sio kufa

vi. Nyumba ya wawili ni kivuli cha amani

vii. Simtaki bwanako wangu ni mtamu

viii. Zawadi ni chochote kupokea usichoke

ix. Subira nyumba ya neema

x. Neno jema halikosi kujibiwa

xi. Sitasahau hisani uliyo nitendea

xii. Wema alionifanyia sitoweza kumuacha

xiii. Si neno nitasubiri

xiv. Wa kukupinga hayuko wala hatachomoka

xv. Heshima tukipeana daima tutapendana

xvi. Nipambe nipendeze waigao wasiweze

xvii. Mimi na wewe hatuwachani

xviii. Pendo ni mlango wa heri

xix. Tukiwa na imani daima tutasikizana

xx. Heri kumfadhili mbuzi binadamu ana maudhi

xxi. Kaeni mtue mimi nina mwenyewe

xxii. Penzi halina kabila wala mila

xxiii. Kwenye mapenzi hapakosi fitina

xxiv. Si neno bora uzima

xxv. Tupendane duniani tupate amani

xxvi. Nia zikiwa pamoja udugu hufana

xxvii. Tuombeane kheri kwa siku hii njema

xxviii. Raha ya dunia ni watoto

xxix. Muungwana hafichiki

xxx. Mtenda mema hasahauliki

xxxi. Wimbo mbaya haumbembelezi mtoto

xxxii. Uzuri wa mja ni vitendo vyake

xxxiii. Ingawa kichache tunu ya kutunukiwa

xxxiv. Daima u mawazoni naikumbuka yani shani

Usemi wa jumla **(J)**

i. Simtaki bwanako wangu ni mtamu

ii. Nilikupenda ukajishaua mwenzio yuala maua

iii. Mulidhani nitadhirika kumbe nimetajirika

iv. Utamaliza bucha zote nyama ni ile ile

v. Inua guu gongo laja

vi. Afadhali kuishi na paka kuliko jirani wa hapa

vii. Ingawa sisemi ujuwe hamuniwezi

viii. Nenda ukaliwe pesa waganga haweshi

ix. Ujirani naupenda lakini tabia zimenishinda

x. Kama unaweza mtie kamba mumeo

xi. Moyo wa hasidi hauna dawa

xii. Wangapi walisema na sasa wako wapi

## KIAMBATISHO VI

**Picha**

- **1 – 7** ni picha zilizopigwa wakati wa maonyesho ya ‘Swahili Attire’ katika Jumba la Makumbusho la Fort Jesus.
- Katika picha **8**, mtoto mchanga anapokelewa kwa kanga na nyanya zake.
- **9** Kanga zikiwa zimetandikwa sakafuni ili bibi arusi na msafara wake wazikanyage wakitoka nyumbani kwao bibi arusi.
- **10** Bibi arusi na msafara wake wakikanyaga kanga.
- **11-15** Mitindo tofauti ya kuvaa kanga.
- **16** Nyumba za kipwani
- **17** Mtafiti akiwa jikoni mwa mmoja wa wenyeji wake


KARIBUNI TUF
HI YA MAMA K
USIWE NA KIWEWE
BASAMU YAKO NI
YUKO MOYONI
YUKO MOYONI
KARIBUNI TUFUR
KARIBUNI TUFU

1


KANIKI
KANIKI

2




3



4



5



6




7

8






9



10



11




12



13



14



15



16




17